# Nipashe

Jumatatu Septemba 9, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580018

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Imani Asia inavyomaliza wanyamapori wa Afrika

UKURASA 4



NIPASHE JUMATATU SEPTEMBA 9, 2019

Nipashe Spotika

NYOTA 7 WANAOVAA NA KUITENDEA HAKI JEZI NA. 7 UK. 20

ISIKUPITE

Harry Kane amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 25 na zaidi (25+), katika mechi 40 za kwanza alizocheza timu ya Taifa ya England tangu Gary Lineker alipofunga mabao 27. Na hat-trick aliyofunga dhidi ya Bulgaria juzi ni ya 13 kwake katika klabu na timu ya taifa (Spurs 11, na England hat-trick mbili).

FURUKUTA...

Mshambuliaji wa England, Marcus Rashford (katikati), akihaha kumpita beki wa Bulgaria, Nikolay Bodurov kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa Wembley na wenyeji kushinda 4-0. HABARI UK. 30

UKURASA 13

# Mbivu, mbichi Lissu, Ndugai leo

- **Mahakama** kumaliza ubishi wa mawakili
- **Atoa** kauli nzito sakata la kushambuliwa akisema... *Ukurasa 2*



Dereva wa guta akiwa amelisheheni mzigo wa vipande vya magodoro katika Barabara ya Sam Nujoma, eneo la Mwenge, jijini Dar es Salaam jana, hivyo kumfanya ashindwe kuona magari yanayokuja nyuma, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Msako mashine 10,000 kamari

UKURASA 3



## Serikali, familia wavutana vikali maziko ya Mugabe

UK.3

**MICHEZO** **AUSSEMS: MZAMIRU ANAIBEBA SIMBA** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Naibu Waziri wa Kwanza wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Cuba, Marcelino Medina Gonzalez, alipofika Ikulu Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Uamuzi mchuano Lissu, Ndugai leo

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMA ya maombi ya mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, kupata kibali cha Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam cha kusikilizwa maombi yake ya kuvuliwa ubunge pamoja na kutoa zuio la muda la kuapishwa mbunge mteule Miraji Mtaturu au la itajulikana leo.

Uamuzi huo umepangwa kutolewa leo baada ya mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Sirilius Matupa kusikiliza hoja za mawakili wa pande zote mbili kuhusu Lissu kupata au kutokupata kibali hicho.

Pamoja na mambo mengine, Lissu ameiomba mahakama kutoa zuio la muda kwa mlalamikiwa wa kwanza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Job Ndugai, kusitisha tukio la kumwapisha Mtaturu katika Mkutano wa Bunge ulioanza Jumanne iliyopita jijini Dodoma.

Hata hivyo, kutokana na Mahakama kuahirishwa jioni ya Agosti 29, mwaka huu bila kutoa uamuzi, Bunge lilimwapishwa mbunge mpya wa jimbo hilo, Miraji Mtaturu, aliapishwa siku hiyo kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa na Bunge ya mkutano huo.

Katika maombi hayo namba 18 ya mwaka 2019, dhidi ya Spika Job Ndugai na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Lissu anaomba kibali cha kufungua shauri la maombi maalum ikiwamo kumtaka Spika awasilishe mahakamani taarifa aliyoitoa bungeni ya kumvua ubunge ili iweze kupitiwa na Mahakama na kufanyiwa maamuzi.

Kwa mujibu wa hati ya maombi hayo mlalamikaji anaomba mahakama kuitisha uamuzi uliofanywa na Spika, kuufanyia uchunguzi na kukiwasilisha.

Wakili Peter Kibatala alidai kuwa sababu kubwa ya kuomba kibali ni kutokana na kazi ya mahakama kupitia nyaraka kama zinafaa kusikilizwa kama mlalamikaji anavyoomba.

"Katika kipindi cha miaka saba iliyopita Lissu alikuwa anafanyakazi zake za uwakili wa wananchi vyema, lakini alishambuliwa kwa risasi na kutibiwa jijini Nairobi, nchini Kenya na baadaye akahamishiwa Ubelgiji."

Akifafanua zaidi wakili alidai kuwa Lissu hakuwahi kupewa taarifa za kutenguliwa ubunge wake amesikia barabarani. Mawakili wa walalamikiwa mawakili wa serikali wakuu, Vincent Tangoh, Lucas Malunde na Abubakar Mrisha kwa nyakati tofauti walipinga mahakama kukubali ombi la Lissu kwa kuwa yana mapungufu ya kisheria.

Tangoh alidai kuwa kiapo cha mlalamikaji hakina miguu ya kusimamia kwa sababu hakijaambatanishwa na nyaraka muhimu za kisheria.

Mrisha alidai kuwa hoja zote za Lissu hazina mashiko mahakama itupilie mbali ikatae kuzisikiliza.

Katika maombi ya msingi, maombi hayo ya kuvuliwa ubunge yalifunguliwa na aliyekuwa Lissu kupitia mawakili wake hao, chini ya hati ya dharura, kupitia kwa kaka yake Wakili Alute Mughwai, ambaye amempa mamlaka ya kisheria kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa maombi namba 18 la mwaka 2019, Lissu anaiomba mahakama hiyo, impe kibali cha kufungua kesi ili mahakama hiyo itoe amri ya kumtaka Spika Ndugai ampe (Lissu) taarifa yake ya kumvua ubunge.

Hivyo anadai atakuwa ameathirika kwa kuwa atapoteza haki zake zote, kinga na maslahi yake yote yanayoambatana na wadhifa wake huo wa ubunge. Uamuzi wa kumvua ubunge ulitangazwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, Juni 28, 2019, wakati akiahirisha mkutano wa 15 wa Bunge, huku akitaja sababu mbili.

Ndugai alizitaja sababu hizo kuwa ni kushindwa kuhudhuria vikao vya bunge kwa muda mrefu bila kumjulisha spika kwa maandishi mahali aliko na sababu ya pili ikiwa ni kutokuja taarifa za mali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Hata hivyo Spika Ndugai alijitetea kuwa si yeye aliyemvua ubunge bali ni katiba ya nchi.

**LISSU ASHANGAA**

Katika hatua nyingine, Lissu amesema anashangaa watu waliomshambulia kwa risasi Septemba 7 mwaka Juzi nyumbani kwake jijini Dodoma wakati akirejea katika mkutano wa bunge kutojulikana mpaka leo.

Katika taarifa yake, amesema ingawa watu hao wameshindwa kutekeleza azma ya kuondoa uhai wake, lakini alitarajia kuwa wangekuwa wameshakamatwa na Jeshi la Polisi na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

"Ijapokuwa ilikuwa mchana kweupe katika mji wa kawaida wa Dodoma, leo hii miaka miwili baadae Serikali yetu bado inawaita washambuliaji hao watu wasiojulikana," Lissu alisema jana.

Akizungumzia kuhusu safari ya miaka miwili ya matibabu yake Lissu alisema kwa kiasi Kikubwa amepona licha ya kudai kunyimwa fedha za kugharamia matibabu yake na Bunge kwa sababu aliazoziita 'zisizojulikana'.

Lissu alisema ameacha kutumia magongo tangu Juni 29, mwaka huu, na pia sindano na dawa alizokuwa akipewa na madaktari kuzitumia tangu Julai 30, mwaka huu akifahamisha pia kwamba mifupa yake iliyovunjwa kwa risasi kwa sasa imeunga na kupona vizuri.

Kuhusu kurejea nchini, alisema anaendelea kushauriana na viongozi wa chama chake (Chadema) pamoja na familia yake ili kupata muafaka wa tarehe ya kurejea nchini huku akiahidi kutokuifanya kuwa siri.

"Mimi sio mhalifu kwa hiyo siwezi kurudi nyumbani kwetu kwa kificho badala yake nitarudi nyumbani kwetu mchana kweupe mbele ya macho ya Watanzania na dunia nzima," Lissu alisema.

Septemba 7 Mwaka Juzi Lissu alishambuliwa kwa kwa kupigwa risasi zaidi ya 30 na watu wasiojulikana karibu na nyumbani kwake Area 'D' mjini Dodoma akiwa ndani ya gari lake wakati akitoka katika kikao cha Bunge.

Baada ya shambulio hilo safari ya matibabu yake ilianzia katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma na baadae alihamishiwa katika hospitali ya Nairobi nchini Kenya ambako alikaa kwa siku 121 kabla ya Kupelekwa Ubelgiji Januari 6, mwaka jana hadi sasa kwa ajili ya matibabu zaidi.

***Imeandikwa na Hellen Mwango na Enock Charles***

## Hapa ndipo ilipo miujiza ya JPM

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KATIKA miezi 47 aliyoiongoza Tanzania, Rais John Magufuli anaelezwa kuwavutia wengi kutokana na mambo makubwa anayoyafanya.

Baadhi ya wachambuzi wa masuala ya kiuchumi na kisiasa wamesema Dk. Magufuli ni Rais wa miujiza kutokana na wananchi wa mataifa mengine barani Afrika wangependa kuwa naye.

Mwanazuoni maarufu kutoka Kenya, Prof. Patrice Lumumba, katika moja ya mihadhara yake alitamani kitu alichokiita 'Magufulification of Afrika' akimaanisha Bara la Afrika liongozwe kwa namna Rais Magufuli anavyoiongoza Tanzania. Bila shaka, ni kutokana na moyo wa kizalendo na shauku ya Rais Magufuli kuona Tanzania inapiga hatua kubwa kimaendeleo, ilimsukuma msomi huyo kutoa kauli hiyo.

Katika kipindi hicho cha takribani miezi minne kwenye madaraka ya urais, Dk. Magufuli ametekeleza miradi mikubwa kwa lengo la kufungua fursa za kiuchumi na mingine inaendelea kutekelezwa.

Miradi iliyotekelezwa na mingine iko kwenye utekelezaji ni pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) Sh. trilioni 7.5, ufuaji wa umeme wa maji katika Bonde la Mto Rufiji, maarufu Stiegler's Gorge Sh. trilioni 6.5 na ujenzi wa barabara za juu Ubungo Sh. bilioni 247.

Mingine ni ujenzi wa Daraja la Kigongo-Usisi litakalokuwa refu zaidi Afrika Mashariki na Kati Sh. bilioni 696, Daraja la Salender Sh. bilioni 270 na barabara ya Kimara-Kibaha Sh. bilioni 140. Katika miaka minne ya uongozi wake madarakani, Rais Magufuli pia anatekeleza ujenzi wa barabara zenye urefu wa Km 2,115 kwa kiwango cha lami Sh. trilioni 4.37, ukarabati wa viwanja vya ndege 15 Sh. trilioni 1.868 na ununuzi ujenzi wa rada nne kwa ajili ya mikoa ya Mbeya, Dar es Salaam, Mwanza na Kilimanjaro Sh. bilioni 67.3.

Serikali yake pia inatekeleza mradi wa ujenzi na ukarabati wa meli mbili Ziwa Victoria Sh. bilioni 172.3, upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mtwara na Tanga Sh. trilioni 1.2 na ununuzi wa ndege nane Sh. trilioni 1.05.

Rais Magufuli pia ametekeleza mpango wa muda mrefu wa serikali kuhamia Dodoma, huku akijenga barabara kwa kiwango cha lami kwenye mitaa mbalimbali nchini kwa Sh. bilioni 660 na kutoa Sh. bilioni 54 kwa ajili ya uwezeshaji vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Katika miaka minne ya uongozi wake madarakani, Rais Magufuli pia amejenga barabara kwenye majiji, manispaa na halmashauri kwa Sh. trilioni 1.35, zahanati 30, vituo vya afya 352, hospitali za wilaya 67 na kukarabati hospitali za zamani 21 (zote zimegharimu Sh. bilioni 321.6).

Serikali yake pia imenunua vifaa vya afya kwa Sh. bilioni 64, imekarabati shule kongwe 62, imejenga madarasa, maabara na maktaba kwa Sh. bilioni 308.1.

Katika kipindi hicho cha miaka minne, serikali ya awamu ya tano imetoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu Sh. trilioni 1.62 na kugharamia mpango wa elimu bila malipo kwa kuziwezesha shule husika Sh. bilioni 945.97.

Rais Magufuli pia ana mpango wa kujenga uwanja mkubwa wa ndege eneo la Msalato jijini Dodoma na kutekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Km 110 jijini humo kwa Sh. bilioni 410.

Serikali yake pia ina mpango wa kujenga barabara ya Bagamoyo-Pangani na kutekeleza miradi ya maji ukiwamo wa Jiji la Arusha unaotarajiwa kugharimu Sh. bilioni 520.

Rais Magufuli ameendelea kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo, huku serikali yake

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KIMATAIFA

# CUF yamwomba JPM msaada vurugu 'Sauzi'

**Na Mary Geofrey**

CHAMA Cha Wananchi (CUF), kimemwomba Rais John Magufuli, kutumia nafasi yake ya uenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), kufanya mazungumzo na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, kwa ajili ya kutafuta suluhu ya vurugu zinazoendelea nchini humo.

Aidha, wamemtaka kuitisha mkutano wa dharura wa SADC kwa ajili ya kujadili suala hilo linalogharimu maisha ya Waafrika wengi.

Wito huo ulitolewa na Naibu Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Bunge na Sera wa CUF, Mohamed Ngulangwa, juzi jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema Rais Magufuli kwa nafasi yake ya uenyekiti wa SADC, anaweza kufanya mazungumzo na Rais wa Afrika Kusini na kuitisha mkutano huo ili kutuliza ghasia hizo zilizohatarisha maisha ya raia wa Afrika wanaoishi nchini humo.

"Kwa masikitiko makubwa watu zaidi ya 100 wamepoteza maisha Afrika ya Kusini kuteswa, kupigwa na kuchomwa moto, huku Serikali ya Afrika Kusini ikiwa imekaa kimya. Tunamwomba Rais Magufuli atumie nafasi yake ya uenyekiti wa Sadc, kutafuta suluhu na Rais wa Afrika Kusini kwa ajili ya kumaliza vurugu zinazogharimu maisha ya wenzetu," Ngulangwa alisema.

Alisema wapo Watanzania ambao wamekumbwa na kadhia hiyo na Watanzania wamekuwa wakilia kwa kuhofia kupoteza ndugu zao.

Sintofahamu hiyo iliyosababisha vifo vya watu zaidi ya 100, iliibuka Septemba 2, mwaka huu, baada ya kuvamia katika jengo moja mjini Jeppestown.

Watu hao wamevamia maeneo yenye shughuli za biashara na kuchoma moto maduka pamoja na kupora. Nchi hiyo imekuwa ikikumbwa na matukio ya ubaguzi wa rangi kila mara, huku watu kadhaa wakiripotiwa kuuawa na kupata majeraha.

# Serikali, familia wavutana maziko ya Mzee Mugabe

**HARARE,** Zmbabwe

SIKU tatu baada ya Rais wa zamani wa Zimbabwe, Robert Mugabe, kufariki dunia, umetokea mvutano kati ya familia na serikali kuhusu wapi kiongozi huyo atazikwa.

Mugabe (95) ambaye ni mwasisi na Baba wa Taifa la Zimbabwe, alifariki mwishoni mwa wiki akiwa anatibiwa katika moja ya hospitali ya Singapore, ambako alilazwa kwa miezi mitano. Vyombo vya habari nchini humo vimeripoti kuwa familia na serikali inayoongozwa na Rais Emmerson Mnangagwa wako katika mvutano kuhusu sehemu ya kumzika jabari huyo wa Afrika.

Imaelezwa kuwa familia inataka azikwe nyumbani kwake Zvimba, huku serikali ikisema atazikwa eneo malum wanakozikwa mashujaa wa taifa hilo.

Lakini hadi jana, mwili wa Mugabe haukuwa umewasili nchini kutoka Singapore, na kwamba mjane wa Mugabe, Grace, marafiki wa karibu pamoja na maofisa wa serikali nao wamebakia Singapore.

Gazeti la The Obsever lilimnukuu msemaji wa chama tawala cha ZANU-PF, Simon Khaya Moyo, akieleza kuwa Mugabe atazikwa katika makaburi ya mashujaa na shughuli za kuaga mwili wake zitafanyika katika uwanja wa taifa, na kwamba idadi kubwa ya viongozi mashuhuri kutoka Afrika wanatarajia kuhudhuria.

"Eneo la mashujaa ndiyo sehemu nzuri kwa Mugabe kuzikwa, labda familia iamue vinginevyo, lakini mwili haujafika, hivyo hatuwezi kuanza taratibu za mazishi," alisema Moyo na kuongeza:

"Familia wao walishakutana na tayari wameshajadili, ninachojua mimi lazima atazikwa kwenye makaburi ya mashujaa, lakini ni uamuzi wa familia na Mugabe mwenyewe wapi alipotaka, yote hayo tutajua mwili utakapowasili."

Gazeti hilo pia lilimnukuu Grace akieleza kuwa Mugabe atazikwa katika eneo lililopo nyumbani kwake Zvimba, umbali wa maili 60 kutoka mji mkuu Harare. Na idadi ndogo ya watu ndiyo watakaohudhuria.

Mbali na Grace, hata ndugu wa Mugabe nao wanatofautiana kuhusu eneo yatakapofanyika maziko. Mpwa wa Mugabe, Leo Mugabe, alisema': "Maamuzi bado hayajatolewa, lakini mjomba wangu alipokuwa hai hajawahi kutoa maelekezo sehemu ya yeye kuzikwa."

"Tunasubiri kuwasili kwa mwili kabla ya programu yote kufahamika. Hata hivyo, hatujawahi kuzungumza na mjomba kabla hajafariki sehemu atakayozikwa, hivyo bado haijakaa sawa," alisema Leo.

Serikali hata hivyo ilieleza kuwa: "Familia inapaswa kukaa kimya, maziko yanagharamiwa na serikali, gharama zote za matibabu Singapore zimelipwa na serikali, na hadi mwili utakaporudishwa nchini."

"Kulikuwa na mazungumzo ya siri kabla ya tukio hili kutokea, yalifanyika kwa muda wa mwezi mmoja kabla ya taarifa kutolewa kwa wananchi, wanafamilia watano waliokwenda Singapore, hawajarudi na hata waliobaki hapa walikuwa wakishirikishwa katika mazungumzo."

Ijumaa, Rais Mnangagwa alimtangaza Mugabe kuwa ni shujaa wa taifa, na kutangaza siku za maombolezo kabla ya maziko.

Hata hivyo, Rais Mnangagwa hakutangaza wala kutoa maelezo yoyote kuhusu taratibu za maziko, lakini taarifa zinaeleza kuwa amepanga maziko ya Mugabe kufanyika katika makaburi ya Mashujaa.

Pia imeelezwa kuwa kaburi atakalozikwa Mugabe litabuniwa na wataalamu kutoka Zimbabwe na Korea Kaskazini.

Imeelezwa kuwa endapo Mugabe atazikwa katika makaburi ya Mashujaa itawapa uwezo viongozi wapya wa taifa hilo kutoa salamu zao za mwisho kwa mwili wa Mugabe ambaye alitawala taifa hilo kwa miaka 40.



Wafanyausafi barabarani wakiwa wamebeba vifaa vyao vya kazi, tayari kwa kuanza kazi yao, katika eneo la Magomeni Kondoa, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# TRA yazisaka mashine za kamari 10,000

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema imeanzisha operesheni ya kuzisaka mashine za michezo ya kubahatisha zaidi ya 10,000 ambazo zimeingizwa nchini kwa njia ya magendo.

Imesema mashine hizo zimeingizwa kupitia Kanda ya Kaskazini, Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa zikitoka nchi jirani, zimekuwa zikiingizwa bila ya kusajiliwa na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha.

Kaimu Meneja wa TRA Mkoa wa Kikodi Ilala, Steven Kauzen, alisema TRA imepata taarifa ya kuwapo kwa mashine nyingi za michezo ya kubahatisha mitaani ambazo ziliingizwa kimagendo, hivyo kuikosesha serikali kodi.

Kauzen aliwataka wafanyabiashara wote wanaomiliki mashine za michezo ya kubahatisha nchini kuhakikisha wanasajili mashine hizo, kwa kuwa operesheni inaendelea ili kubaini wanaokiuka, na kwamba watakaokamatwa watachukuliwa hatua za kisheria haraka.

Alisema wafanyabiashara wa mashine hizo wamekuwa wakibuni mbinu mpya kila wakati kadri wanavyowakamata, akitolea mfano wa baadhi yao kuingiza mashine hizo vipande vipande tofauti na zamani, lengo lao kuu likiwa ni kukwepa kulipa kodi.

Wakati huo huo, Kauzeni alisema TRA kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama walifanikiwa kukamata vipuri ambavyo vingeunganishwa vingetengeneza mashine za michezo ya kubahatisha 500, na kuikosesha serikali kodi ya zaidi ya Sh. milioni 600 kwa mwaka.

Alisema walizikamata mashine hizo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam zikiwa zimeagizwa bila kufuata taratibu na raia wa China, Wu Dingfeng (31), mwajiriwa wa kampuni ya Bonanza Trade.

"Vipuri hivyo vilikuwa vinaelekea mkoa wa Kilimanjaro ambako vilitarajiwa kupokewa na Dingfeng.TRA kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi Mkoa wa Kilimanjaro waliendelea kufanya uchunguzi, ambapo walifanikiwa kumkamata Dingfeng," alisema Kauzen.

Alisema kukamatwa kwa mfanyabiashara huyo ni matokeo ya operesheni inayoendelea kati ya TRA, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha na vyombo vya ulinzi ili kubaini wale wote wanaofanya biashara hiyo bila kufuata taratibu za usajili mashine na biashara hizo.

Meneja wa TRA upande wa Forodha (JNIA), Wilson Kantambula, alisema kuwa kutokana na kubaini mbinu mbalimbali wanazotumia watu hao tayari wameweka taratibu ikiwamo kutoa elimu ya kutosha kwa maofisa namna ya kuwabaini wale wote wanaokinzana na taratibu hizo.

Naye Meneja wa Ukaguzi na Uthibiti wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Sadiki Elimsu, alisema kwa sasa wapo katika operesheni hiyo nchi nzima ili kukamata wale wote wanafanya biashara hiyo kinyume cha sheria.

# Imani Asia inavyoangamiza wanyamapori Afrika

• Huamini kuvaa vidani vya tembo, kakakuona, faru huongeza utajiri, tiba...



Mwandishi wa ripoti hii akiangalia bidhaa mbalimbali katika Soko la Amulet, Bangkok Thailand, maarufu kwa kuuza bidhaa za wanyamapori ambazo ni halali na haramu. **NA MPIGAPICHA WETU**

**Na Salome Kitomari,** aliyekuwa THAILAND

IMANI na utamaduni wa watu wa Bara la Asia imedaiwa kuwa kichocheo kikubwa cha biashara ya bidhaa za malighafi zitokanazo na wanyamapori ambazo nyingi hutolewa Bara la Afrika, ikiwamo Tanzania.

Licha ya jitihada mbalimbali za kupambana na ujangili ikiwamo kubadilisha sheria, kuunda vikosi kazi na operesheni mbalimbali, bado ujangili umeendelea.

Tukio la hivi karibuni ni kukutwa kwa vipande 339 vyenye thamani ya Sh. bilioni 4.4 eneo la Chamazi, Manispaa ya Temeke.

Idadi ya vipande hivyo vya meno ni sawa na tembo 117 waliouawa. Tayari watu sita wanashikiliwa wakiwamo askari wawili wanaodaiwa kuhusika kwenye tukio hilo.

Tanzania ni miongoni mwa nchi barani Afrika yenye vivutio vingi vya utalii kwa kuwa na wanyama wa aina mbalimbali kwenye Hifadhi za Taifa, Mapori ya Akiba, Mapori Tengefu, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Maeneo ya Hifadhi za Jamii (WMA).

Sekta ya Utalii inaliingizia taifa asilimia 25 ya fedha za kigeni, Pato la Taifa kwa asilimia 17.5, ajira za moja kwa moja zaidi ya 600,000 na zisizo rasmi milioni 1.5.

Ujangili wa tembo na faru ulikuwa tishio kubwa kwa Tanzania miaka ya 2015 na miaka ya nyuma kiasi cha kubaki tembo 530,000, huku faru wakianza kuzaliana baada ya kumalizika kutokana na ujangili.

Mtaalamu wa tembo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Idara ya Zoolojia na Hifadhi ya Wanyamapori, Dk. Elikana Kaumanga, anasema mwaka 1,800 kulikuwa na tembo milioni 24, lakini sasa wamebaki kati ya 470,000 na 530,000.

Alisema soko la meno ya tembo linaendelea kukua kwa nchi ambazo zilikuwa hazifanyi biashara hiyo, na Tanzania imeamua kuunda kikosi kazi kupambana na ujangili huo.Kwa mujibu wa Kaumanga, tembo wengi Tanzania wapo hifadhi za taifa za Serengeti, Mikumi, Ruaha Rugwa, Pori la Akiba Selous, Ngorongoro, Rukwa Katavi na Ziwa Victoria.

Mafanikio ya Tanzania kudhibiti ujangili wa wanyamapori yametokana na kikosi kazi cha taifa kinachojumuisha mamlaka mbalimbali, yenye vikosi katika kila kanda na ngazi mbalimbali za kushughulikia biashara hiyo haramu, kiasi cha kukamatwa kwa mtandao wa ujangili.

Februari mwaka huu, mfanyabiashara wa kichina aliyejulikana kama 'Malkia wa tembo' alihukumiwa kifungo cha miaka 15 jela kwa kosa la kusafirisha zaidi ya meno ya tembo 350 kuelekea Asia.

Mwaka 2017, kiongozi wa mtandao wa ujangili, Boniface Maliango, maarufu kama 'shetani' alihukumiwa miaka 12 jela kwa kujihusisha na ujangili wa meno ya tembo ambayo yalisafirishwa kwenda Asia.

Kwa Bara la Asia nchi zinazotumia bidhaa za wanyamapori zimetajwa kuwa ni China, Thailand na Vietnam, ambazo matumizi yake yamejengwa kutokana na imani na utamaduni wa watumiaji tangu enzi za mababu.

Mwandishi wa habari hii alitembelea Thailand kwenye maeneo ya hifadhi za taifa, maeneo ya kuhifadhia wanyama waliokamatwa nchini humo, Idara ya Forodha Uwanja wa Ndege wa Suvarnabhum na soko la bidhaa ya wanyamapori na kukutana na wataalamu mbalimbali wa taasisi za kimataifa za bara la Asia.

Waandishi wa habari 10 wa nchini Thailand na Tanzania walitembelea nchi hizo (Tanzania na Thailand), kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la watu wa Marekani (USAID Protect Tanzania na USAID Wildlife Asia) kwa kushirikiana na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (Jet).

Lengo la programu hiyo ni kuwawezesha wanahabari kujifunza kuanzia kwenye chanzo cha wanyamapori (Tanzania) na kwa watumiaji (Asia), ili kupambana na ujangili wa wanyamapori.

Nchi ya Thailand inaelezwa kuwa ni kitovu cha usafirishaji wa njia zote za barabara, bahari na anga, huku ikiwa ni lango la bidhaa halali na haramu zinazoingia kutoka kwenye nchi mbalimbali duniani. Nchi hiyo ina idadi kubwa ya watalii na watumiaji wa bidhaa za wanyamapori kutokana na imani na utamaduni.

Nchi hiyo ina ukubwa wa kilomita za mraba 513,120 na watu zaidi ya milioni 69, huku asilimia 30 ya watu wake wakiishi katika Jiji la Bangkok na uchumi wake ukitegemea biashara, usafirishaji, mawasiliano na kilimo.

Kwa ukanda wa Asia, Jiji la Bangkok ndiyo linalotembelewa na idadi kubwa ya watalii duniani, wengi huenda kwenye masoko maarufu ya bidhaa za wanyamapori zilizo halali na zisizo halali, na kwa mwaka 2018 inakadiriwa watalii milioni 22 walitembelea nchi hiyo.

Hifadhi za taifa na hifadhi ya misitu zilianza mwaka 1962, ikiwamo kuwapo kwa sheria mbalimbali za uhifadhi ambazo ziliongeza eneo lililohifadhiwa kutoka asilimia 25 hadi 30.

Utafiti uliofanywa na USAID Wildlife Asia, ulibainisha sababu za kuendelea kwa biashara haramu ya bidhaa za wanyamapori kama tembo, faru, kakakuona na tiger (mnyama aina ya chui) kunatokana na imani na utamaduni wa watu wa bara hilo hususan nchi za Thailand, China na Vietnam, na asilimia 20 ya tembo wa Afrika wanadaiwa kuuawa na kupelekwa kwenye nchi hizo.

"Mtu anatoa zawadi iliyotengenezwa kwa mazao ya wanyamapori kwa familia, marafiki, masuala ya kijamii na mitandao ya kibiashara kwa mazao ya wanyama wote wanne," anasema mtaalamu wa mawasiliano na kubadilisha tabia wa USAID Wildlife Asia, Wenweena Tangsathianraphap.

## IMANI

Mfuatiliaji na mtaalamu wa uthamini na ufuatiliaji USAID Wildlife Asia, Pakprim Oranop, anasema kwa bara hilo mtu kuvaa kidani au kitu chochote kilichotengenezwa kwa kiungo chochote cha mnyama ni ishara kuwa naye atakuwa jasiri kama mnyama aliyetokana na bidhaa hiyo au anajihakikishia ulinzi.

Wapo wanaoamini inaongeza nguvu za kiume au uwezo wa mwanaume kutambulika kuwa rijali, na wengine wakitumia kama dawa ya kuwafanya kuwa imara kama mnyama husika.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na USAID Wildlife Asia ya kwanini watu wanatumia bidhaa za wanyamapori, walibaini kuwa kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya imani, utamaduni na urembo kwa wanaotumia bidhaa za wanyamapori.

"Wengi tulioongea nao waliamini kuwa anapotumia kitu chochote kilichotengenezwa kwa jino la tembo, pembe ya faru au tiger (chui) basi naye atakuwa na matendo ya kishujaa kama huyo mnyama, na ndiyo maana wengi wameendelea kutumia," anasema.

"Upo uhusiano wa moja kwa moja wa kuendelea kwa makosa ya bidhaa za wanyamapori na imani za wakazi wa bara la Asia, kwa kuwa ili mtu ahesabiwe kuwa shujaa ni lazima atumie bidhaa hizo na ndipo ushujaa wake hukamilika," anasema Oranop.

Anasema wapo wanaotumia bidhaa haramu za wanyamapori kwa ajili ya dawa, chakula na mapambo na yote hayo yanaambatana na imani za dini wanazoamini kwa kuamini kuwa mnyama husika ana nguvu ambazo zitawasaidia katika mambo yao.

Tofauti na nchi nyingine ikiwamo Tanzania, wanyamapori wanaruhusiwa kutumiwa kwa matumizi ya nyumbani baada ya mhusika kufuata taratibu zote muhimu.

Mathalani, kwa Thailand mwananchi wa kawaida anaruhusiwa kumiliki tembo na tiger (mnyama aina ya chui) na kila mwaka anapaswa kulipa kodi kwa serikali ikiwamo kumtunza mnyama husika.

## UREMBO

Wanawake wengi wanapenda kuvaa vidani vilivyotengenezwa kwa mazao ya wanyama hao kwa kuwa huashiria urembo, umahiri na kuhesabiwa katika kundi la watu wa hadhi ya juu.

"Wapo tayari kununua kwa gharama yoyote ile ili kuvaa urembo wa wanyama hao, wengi tulioongea nao hawakuwa na sababu za kwanini wanaamini hivyo, lakini wanaamini kwenye umahiri na urembo kwa kutumia bidhaa za wanyama hao," alisema Oranop.

ITAENDELEA KESHO

## HABARI KITAIFA

# Hifadhi za Taifa 3 mpya kuanzishwa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BUNGE leo linatarajia kuridhia mapendekezo ya kuanzisha hifadhi za taifa tatu katika mikoa ya kusini na magharibi mwa Tanzania.

Ratiba ya mkutano wa 16 wa Bunge la 11 unaoendelea bungeni jijini Dodoma, inaonyesha kuwa leo Bunge linatarajiwa kuridhia azimio la ubadilishaji wa hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba Selous kuwa Hifadhi ya Taifa ya Nyerere.

Pori hilo liko mkoani Lindi lakini linaigusa pia mikoa ya Morogoro, Pwani, Ruvuma na Njombe.

Ratiba hiyo pia inaonyesha leo Bunge linatarajiwa kuridhia azimio la kubadilishaji wa hadhi ya sehemu ya eneo la Pori la Akiba Kigosi kuwa Hifadhi ya Taifa ya Kigosi. Pori hilo liko katika mikoa ya Kigoma, Rukwa, Shinyanga na Tabora.

Bunge pia linatarajiwa kuridhia azimio la ubadilishaji wa hadhi sehemu ya eneo la Pori la Akiba Ugalla kuwa Hifadhi ya Taifa ya Mto Ugalla.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, kesho Bunge linatarajia kupitisha azimio la kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kuhusu kulinda haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Pia Bunge linatarajiwa kuridhia Itifaki ya Marrakesh inayowezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona, wenye uoni hafifu au ulemavu unaofanya mtu kushindwa kusoma ya mwaka 2013.

Ratiba hiyo inaonyesha keshokutwa, Bunge linatarajiwa kuridhia mkataba wa Minamata kuhusu zebaki na kupitisha azimio la kuridhia itifaki ya pamoja ya ziada ya Nagoya-Kuala Lumpur kuhusu uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya baioteknolojia ya kisiasa katika kutekeleza Itifaki ya Cartegena.

Alhamisi kutakuwa na Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 6 wa Mwaka 2019 na Ijumaa kutakuwa na taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo.



Gari likiwa limepinduka kwenye Barabara ya Morogoro, eneo la Kimara Korogwe, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Askofu Kilaini apigia debe wanawake kuwa viongozi

**Agnes Shayo,** TUDArCO

ASKOFU Msaidizi wa Jimbo Katoliki la Bukoba, Mhashamu Method Kilaini, amesema, ipo haja kwa sasa wanawake kushika madaraka katika nyanja mbalimbali za uongozi kuanzia ngazi ya vijiji, kata, udiwani, ubunge hadi urais.

Askofu Kilaini aliyasema hayo Kurasini jijini Dar es Salaam, katika warsha ya siku mbili ya Mwanamke na Uongozi wa Kuchaguliwa, yenye lengo la kuwajengea uwezo wanawake wa dini mbalimbali kuingia katika kinyang'anyiro cha uchaguzi wa serikali za mitaa, udiwani, ubunge na urais, liliyoandaliwa na Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA).

"Nchi yetu ilipofikia sasa vinahitajika vionjo vya kinamama katika nafasi za maamuzi kwa sababu wana karama ya kulea, ambapo hata vitabu vya dini zote vinawatambua kwamba kinamama ni nguzo imara katika familia na jamii," alisema Askofu Kilaini.

Aidha, Askofu Kilaini alimpongeza Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jiamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akisema kuwa pamoja na kwamba ni kiongozi wa kisiasa, lakini maamuzi yake yana vionjo vya umama, hivyo uhitaji wa wanawake katika maamuzi ya kisiasa na kiserikali ni muhimu.

Akizungumza kwa niaba ya CCT, Mchungaji wa Kanisa la Mennonite Tanzania, Dayosisi ya Mashariki Upanga Dar es Salaam, Maira Benjamin Migire, alisema kimsingi wanawake wana sehemu kubwa katika maendeleo ya taifa, hivyo ushiriki wao katika nafasi za maamuzi ni muhimu ili kuwezesha maendeleo ngazi ya kaya na taifa.

Akitolea mfano, Mchungaji Maira alibainisha kuwa Rwanda imekuwa nchi ya kwanza Afrika kwa kuwa na maendeleo kutokana na nafasi nyingi za madaraka kushikwa na wanawake, huku Finland ikiwa ya kwanza duniani.

Naye Shekh Othman Zuberi, Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Kiislam kutoka Bakwata, akizungumza kwa niaba ya baraza hilo, alisema viongozi wa dini wana wajibu wa kuzungumzia masuala ya kisiasa nchini kwa kuwa wao ndio wanaowaimarisha watu kiimani ili waje kuwa viongozi wazuri na wema katika taifa lao.

Aidha, aliwataka wanawake wa dini zote nchini kuondoa uwoga, kujenga uthubutu na kutiana moyo pale wanapomwona mwanamke mwenzao ana uwezo wa kugombea.

"Wanawake mnachotakiwa ni kupeana moyo, kuondoa uwoga, na pia pale mwanamke mwenzenu anapopewa nafasi ya uongozi mnapaswa kumpa ushirikiano wa kutosha, ili kuendelea kulisukuma gurudumu la maendeleo, na daima mkiamua mnaweza," alisema Shekhe Zuberi.

## Waziri atuliza wasanii vikwazo kazi hifadhini

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amewahakikishia wasanii nchini kuwa katika kipindi chake cha uongozi ataondoa vikwazo vyote vilivyokuwa vinapelekea wasitumie mandhari ya vivutio vya utalii vilivyopo nchini wakati wa kutengeneza kazi zao.

Pia amewataka wasanii na watu maarufu wapende vitu vya kwao badala ya kuona ufahari wa kuitumia mandhari za nchi za nje ilhali Tanzania imejaliwa kuwa na utajiri wa mandhari za kipekee na zenye mvuto wa hali ya juu.

Akizungumza jana jioni jijini Dar es Salaam kwenye hafla iliyoandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kushirikiana na vijana wa Tanzania Vision 2025 kwa kuwaalika watu maarufu hususan wasanii kwenye chakula cha jioni, Kanyasu aliwataka wasanii hao watumie kalama na ushawishi walio nao katika kuhamasisha utalii wa ndani.

INAENDELEA UK. 8




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Nembo ya mdhamini, TFF isionyeshe udhaifu Yanga

**BAADA** ya msimu uliopita Ligi Kuu Tanzania Bara kushuhudiwa ikimalizika bila mdhamini mkuu, hatimaye Shirikisho la Soka nchini (TFF), mwezi uliopita liliingia mkataba wa miaka mitatu na Kampuni ya Vodacom kudhamini ligi hiyo kwa Sh. bilioni tisa.

Kupatikana kwa mdhamini mkuu kunakwenda kutatua changamoto kubwa za fedha za usafiri na kwa kiasi fulani uchumi wa klabu 20 zinazoshiriki Ligi Kuu nchini.

Tulishuhudia timu nyingi msimu uliopita zikilazimika kutembeza bakuli kuchangishana ili kuweza kujiendesha, huku kwa TFF hususan kitengo chake cha masoko kikitupiwa lawama kwa kushindwa kutafuta wadhamini.

Hata klabu kongwe kama Yanga, licha ya kuwa na udhamini kutoka Kampuni ya SportPesa bado ililazimika kutembeza bakuli kutokana na gharama za kujiendesha kuwa kubwa.

Hivyo, hatua ya Kampuni ya Vodacom kurejea kwa mara nyingine kudhamini Ligi Kuu ni suala la kupongezwa na kushukuriwa, lakini kuthaminiwa na kuheshimiwa kwa mkataba huo kwa TFF na wanachama wake ambao ni klabu.

Tulishuhudia mwaka 2011 wakati TFF ikiwa chini ya uongozi wa Jamal Malinzi, Klabu ya Yanga ikigomea jezi zake kuwa na nembo nyekundu za mdhamini mkuu, Kampuni ya Vodacom kwa kile walichodai kuwa rangi hiyo si utamaduni wao.

TFF wakati huo ililazimika kurudi kuzungumza na Vodacom ambayo iliikubalia Yanga kubadili rangi ya nembo ya mdhamini kutoka nyekundu na nyeupe kuwa kijani.

Hata hivyo, wakati TFF ikitia saini mkataba huo na Vodacom mwezi uliopita, waandishi wa habari walimtaka Rais wa TFF, Wallace Karia, kujua msimamo wa shirikisho hilo kipindi hiki katika suala zima la kuheshimu mkataba huo.

Karia aliweka wazi kwamba katu hawatakubali kuona nembo hiyo ya mdhamini ikichezewa na klabu yoyote itakayofanya hivyo, itakuwa si mwanafamilia wa TFF.

Kwa hakika tunaunga mkono kwa asilimia 100 kauli hiyo ya TFF, kwani kwa ukongwe wetu kama wadau wa soka, ni Ligi Kuu Tanzania Bara tu ndiyo tumeshuhudia klabu ikikataa rangi ya nembo ya mdhamini eti kwa sababu haiendani na rangi ya jezi zao.

Tunachojiuliza kama klabu zote 20 zinazoshiriki ligi hiyo kila moja ikihitaji rangi yake, thamani ya mdhamini itakuwa ni ipi? Ama Yanga ikitumia nembo hiyo nyekundu itapungukiwa na nini?

Umefika wakati kwa Yanga kutambua haipo juu ya kanuni za TFF na tunaamini yapo mambo mengi ya msingi ya kupigania kwa maendeleo ya klabu kuliko kupoteza muda katika hili.


Hatutegemei kuona TFF ikikubali kugeuzwa dhaifu katika hili, aidha tunaona badala ya shirikisho hilo kupoteza muda kwenda kuiomba Vodacom kuiruhusu Yanga kubadili rangi ya nembo, itumie muda huo kuomba klabu hiyo isiwe sehemu ya wanufaika wa udhamini huo.

Lakini tunaamini Yanga inaongozwa na wasomi, hivyo watalifikiria kwa mapana zaidi na kutazama kwingineko duniani namna ilivyo kwenye ligi za wenzetu waliopiga hatua kisoka na kuridhia kutumia rangi ya nembo ya mdhamini kama ilivyo badala ya kuendeleza malumbano katika hilo.

Lengo letu ni kuona Ligi Kuu Bara ikivutia kampuni nyingi zaidi kuidhamini ili kuongeza ushindani, lakini kama TFF itakubali kuwa dhaifu katika hili, hakika itakuwa chanzo cha kukimbiza wadhamini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wanaume kuingia vyoo vya kike Taifa ni kuwakimbiza viwanjani

**MWANZONI** niliona kama ni bahati mbaya. Lakini nilipokuwa nakwenda kwenye mechi mbalimbali Uwanja wa Taifa niliona hali hiyo ikijitokeza tena na tena.

Nilichokuwa nikikishuhudia huwezi kukiona hata kwenye baa za mitaani. Ni kwamba wanaume wanalazimika kuingia kwenye vyoo vya kike. Hii inawapa tabu sana watoto wa kike wanaokuwa uwanjani.

Waliokuwa tayari ndani wanajikuta wakiwa kwenye vyoo pamoja na wanaume. Wale walio nje wakiona midume inaingia, hawaingii tena. Sasa sijajua huwa wanakwenda kujisaidia wapi.

Hii ndiyo hali iliyopo kwenye mechi nyingi nilizopata kwenda kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Si kwamba mashabiki wa kiume wameamua kuingia kwenye vyoo vya kike kwa makusudi, la hasha.

Ni kwamba vyoo upande wa wanaume vinakuwa vimefungwa. Mazingira ya Uwanja wa Taifa kwa yeyote anayeufahamu ni kwamba upande mmoja ni choo cha wanaume na upande mwingine ni wa wanawake. Kwa sababu asilimia kubwa, yapata 80 ya mashabiki wa soka wanaoingia ni wanaume, basi wanapoona lango la vyoo vya wanaume limefungwa, wanaingia upande wa pili kwa sababu wanaona viko vitupu.

Sijajua ni kwa sababu gani mara nyingi vyoo vya upande wa wanaume huwa vinafungwa kuliko wanawake, lakini hii inaleta usumbufu sana kwenye Uwanja wa Taifa na pia si desturi nzuri si kwa utamaduni wetu, lakini pia kibinadamu.

**Sijajua ni kwa sababu gani mara nyingi vyoo vya upande wa wanaume huwa vinafungwa kuliko wanawake, lakini hii inaleta usumbufu sana kwenye Uwanja wa Taifa na pia si desturi nzuri si kwa utamaduni wetu, lakini pia kibinadamu.**

Uchunguzi wangu mdogo tu nimegundua kuwa unaweza kukuta sehemu moja mlango wa choo cha wanaume kimefungwa na upande wa pili choo cha wanawake kiko wazi, halafu ukizunguka tena sehemu nyingine ya uwanja ndipo utakuta vyoo vya pande zote vinafanya kazi.

Hapa nataka kuwakumbusha tu uongozi wa uwanja unavyotakiwa kufanya. Ni kwamba eneo la mlango wa choo cha wanaume kilichofungwa kwa sababu yoyote ile, wawe wanaweka tangazo la kuwaelekeza wapi waende, kwa sababu baadhi ya mashabiki wakishafika hapo na kukuta mlango umefungwa hawajui kama kuna sehemu nyingine tena kuuzunguka uwanja kuna vyoo vingine.

Hii itawafanya wanaume kuacha kuchukua hatua ya kukimbilia kuingia kwenye vyoo vya wanawake kwa sababu wanaona hakuna tena sehemu nyingine ya kupata haja. Vile vile inawezekana kabisa kuweka askari kwenye mlango wa kuingilia choo cha wanawake ili kuwazuia wanaume wasiingie na kuwaruhusu wanaotakiwa kuvitumia tu.

Najua vyoo vya wanaume hasa Uwanja wa Taifa vinakuwa na changamoto nyingi kwa sababu baadhi yao hawajatulia, unaweza kukuta wameng'oa koki na kufanya maji yatiririke hadi nje, na uharibifu mwingine mwingi ndiyo maana huenda hali hiyo inajitokeza, lakini uongozi wa uwanja uhakikishe siku za mechi yoyote ile hasa inayopokea mashabiki wengi vyoo vyote vya wanaume na wanawake vinafanya kazi ili kuepuka adha hiyo kwa mashabiki wanawake.

Kwa sasa mpira wa miguu umepata bahati ya kuanza kupendwa na wanawake na wameshaanza kuwa wanajitokeza kwenda viwanjani, hivyo inabidi wapatiwe huduma zote muhimu zinazohitajika bila kuwabughudhi na kuwaudhi hali inayoweza kusababisha kususa kwenye viwanjani.

Shirikisho la Soka nchini (TFF), linaweza kukaa na uongozi wa Uwanja wa Taifa kuangalia suala hili.

# BARUA & MJADALA

## Tusifumbie macho uhalifu huu

***Mhariri,***

*UKISOMA vitabu vya dini na hata kusikiliza mahubiri na mawaidha ya viongozi wetu wa dini ni dhahiri utapata jinsi ambavyo misahafu na maelekezo ya viongozi hao inavyosisitiza juu ya umuhimu wa kulinda uhai wa binadamu.*

*Inafafanuliwa kwamba uhai wa binadamu ni lazima ulindwe kwa kuwa ndivyo yalivyo maagizo ya Muumba na kwamba hata sheria, kanuni na taratibu mbalimbali katika jamii na makabila zinavyosisitiza juu ya hilo.*

*Ninaandika katika ukurasa huu kuelezea namna ninavyochukizwa na watu ambao hutupa watoto ovyo majalalani ama kwenye vyoo wakati mwingine na hivyo kukatisha maisha ya watoto wasio na hatia.*

*Tatizo hili kimsingi liko sana kwa wasichana ambao matukio mengi yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara juu yao katika vyombo vya habari. Ninaomba kwa serikali yetu tukufu iwachukulie hatua kali watu wa aina hii wasiothamini kabisa uhai wa binadamu.*

***Imran Komba, Songea***

## Wavuta sigara wafuate sheria

***Mhariri Pole na majukumu ya kila siku.***

*NAOMBA unipatie nafasi kwenye gazeti letu linalotupatia fursa sisi wasomaji wake ya kueleza dukuduku na kero mbalimbali zinazotukabili katika jitihada za kuhakikisha kuwa tunapiga hatua kubwa za kimaendeleo kama watu binafsi na taifa kwa ujumla.*

*Kero niliyo nayo kwa leo ni ile ya watu wanaovuta sigara kila mahali hata kwenye sehemu za wazi au za umma ambazo kimsingi haziruhusiwi kwa wavutaji kufanya starehe yao hiyo.*

*Tabia hii kimsingi inakera katika mazingira yoyote kwa sababu inasumbua wengine wasio wavutaji wa sigara, hali inayowasababishia adha isiyokuwa na sababu, eti tu kwa baadhi ya watu kuendeleza starehe zao.*

*Ikumbukwe kuwa kwa mujibu wa utafiti toka vyanzo mbalimbali vya kiafya, inabainishwa kwamba moshi wa sigara unapomfikia mtu asiyevuta, humuathiri zaidi kiafya kuliko hata huyo mtumiaji mwenyewe.*

*Bahati mbaya zaidi hata pale wananchi wenzetu hawa wavutaji wanapokanywa ama kunasibiwa waache kuwakera wenzao, baadhi yao huziba masikio na wengine hutoa majibu yasiyofaa.*

*Ninaomba mamlaka zinazohusika zisaidie kulimaliza tatizo hili sasa kwa kuchukua hatua za kuwakamata na kuwapeleka kwenye vyombo vya sheria wale wote wanaozidi kuvuta sigara sehemu za wazi ama za umma.*

***Joseph Zengo- Malampaka, Simiyu***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




# 'Pensi' ya Zahera ilivyoingiza wadau wa soka kuchimbua kanuni TFF

**Na Adam Fungamwango**

**SASA** hivi kuna mjadala mkubwa unaoendelea kwenye mitandao ya kijamii, mitaani na hata kwa viongozi wa klabu ya Yanga dhidi ya Shirikisho la Soka nchini (TFF) juu ya kufungiwa na kupewa adhabu Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera.

Makosa yake mawili, moja ni kusema maneno yanayoonekana kuituhumu Bodi ya Ligi, lakini lingine ni kuingia uwanjani akiwa na kaptula au kwa jina lililozoeleka zaidi ni pensi.

Kwenye makala haya sitaki kujikita kwenye mijadala hiyo ya alistahili adhabu au hakustahili, ila nataka kujikita kwenye tatizo kubwa ambalo nililiona tangu mwanzo kuwa litatokea.

Nakumbuka, niliwahi kuandika kabla ya Ligi Kuu msimu huu, wakati TFF ilipoalika, au ilitaka wadau wa soka kupeleka mapendekezo ya kanuni mpya za Ligi Kuu msimu wa 2019/20.

Mapendekezo hayo huwa yanatolewa na wadau mbalimbali wa soka, hata waandishi wa habari wa michezo na viongozi wa klabu zote huwa wanatakiwa kupeleka kwa maandishi vitu ambavyo wanaona vinafaa kuwamo kwenye kanuni ama kuondolewa.

Na baada ya kukusanywa kunafanyika mchujo, na baadaye wadau wanaweza tena kuangalia kile kilichomo, kabla ya kufanyiwa marekebisho, kabla ya kupelekwa kwenye Kamati ya Utendaji, hadi kupitishwa rasmi.

Niliwataka viongozi wa klabu, pamoja na wadau kupeleka mapendekezo na hata baadaye kuyasimamia kwenye marekebisho ili baadaye zikianza kutumika kusiwe na malalamiko.

Nilitanabaisha kuwa mara nyingi si wadau wa soka tu, hata viongozi, hawajishughulishi kabisa na kupeleka mapendekezo hayo na pia kuyasoma yaliyopelekwa, lakini wanakuja kushtuka na kuanza kulalamika kanuni zinapoanza kutumika.

Wanavyoshtuka na kulalamika, ndipo utakapogundua kuwa viongozi wengi wa klabu nchini huwa hawana habari kabisa na kanuni, na huwa wanaanza kuzifuatilia zinapoanza kuwabana.

Habari zinasema kuwa ni klabu tatu tu kati ya 20 ndizo zilizopeleka mapendelekezo, tena yale ambayo waliona yatawanufaisha.

Inasemekana klabu hizo ni Simba, Yanga na Alliance FC tu. Wakati Alliance na Yanga wao wakipendekeza mapato yawe sawa kwa wageni na wenyeji, Simba ilitaka wachezaji wa kigeni siyo lazima wachezee timu za taifa za nchi yao.

Hawakuwa na mapendekezo mengine, lakini pia timu zingine 17 hakuna hata moja iliyopeleka.

Leo hii kocha Zahera amehukumiwa kutokana na vifungu vilivyomo kwenye kanuni hii hii, lakini viongozi wa Yanga, pamoja na baadhi ya watu wanapiga kelele kuwa kocha ameonewa, wengine wakidai kanuni kwenye eneo la mavazi haijajitosheleza na inaelea.

Narudi kule kule kuwa viongozi na wadau wengi hawapeleki mapendekezo, hawasomi kanuni hadi pale imetokea kuwabana upande wao, ndiyo zitatolewa kasoro mbalimbali zilizomo kwenye kanuni, wakati zilitakiwa kutolewa kabla ya kuanza kutumika.

Kama kifungu kinamtaka kocha kuvaa nadhifu, sare ya klabu, na unadhifu huo haujafafanuliwa, hii ilitakiwa isemwe au TFF waambiwe kabla, lakini si kusubiri kanuni imeshambana mtu ndipo watu wajitokeze kuanza kusoma kanuni na kuzitoa kasoro.

Na mara nyingi kanuni zinatolewa kasoro pale tu zinapozibana klabu kubwa za Simba na Yanga.

Sijasikia mtu akitoa kasoro kipengele ambacho kimemtia hatiani msemaji wa Ruvu Shooting Masau Bwire cha kuingia uwanjani mara tu baada ya mechi kumalizika.

Nadhani hali ingekuwa tofauti kama msemaji wa Yanga au wa Simba ameingia uwanjani baada ya mechi kumalizika. Kanuni ingeonekana ina kasoro na TFF ingeshutumiwa.

Wakati mwingine kanuni hizi zinapingwa tu kwa sababu mihemko ya mashabiki wa klabu kubwa na si vinginevyo.

Ifike wakati wadau wote wa soka na viongozi wawe na tabia ya kutoa mapendekezo ya kanuni za kila mwaka za ligi, lakini kuzisoma kabla na kuzitoa kasoro kabla hazijaanza kutumika na si kukaa kimya mpaka zianze kufanya kazi ndipo watu wanakurupuka na kuanza kutafuta kanuni zinasemaje, na zikionekana kumewabana wao zinaanza kutolewa kasoro wakati hawakushiriki kwa njia yoyote kuzitengeneza. Huu ni udhaifu mkubwa wa wadau na viongozi wa soka wa Tanzania.

Leo adhabu ya Zahera, ndiyo kila mtu anaanza kuzisoma kanuni na kuzichambua, na nadhani bila hivyo hakuna yoyote ambaye angeshughulika nayo.

**KABWELA** — Na Fadhili Mohammed



# Waziri atishwa kasi dawa za kulevya

**Na Suleiman Rashid Omar,** PEMBA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud Mohame, amesema mapambano dhidi ya dawa za kulevya ni kazi nzito, kubwa na ngumu inayohitaji ujasiri, mbinu na ushirikiano ili kufanikiwa.

Aboud aliyasema hayo alipokuwa akilifungua kongamano la kupiga vita matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya mjini Chakechake.

Alisema udhibiti na ufuatiliaji wa kupiga vita matumizi ya uingizaji wa dawa za kulevya ina ugumu kutokana na kutawaliwa na rushwa kwa baadhi ya watendaji, na kwamba hali hiyo pia inachangiwa na jamii kuoneana aibu katika udhibiti wa dawa hizo.

Kadhalika alisema udhibiti wa dawa za kulevya pia unachangiwa na wauzaji na waingizaji kuwa miongoni mwa watu mashuhuri na wafanyabiashara wakubwa, ambao wakati mwingine inakuwa vigumu hata kuamini kuwa ni wauzaji, hivyo kuwa vigumu kuwakamata.

"Jamani dawa za kulevya zina athari kubwa, tena ni hasara tupu hakuna faida hata moja kwa mtumiaji," alisema Aboud.

Alisema mtumiaji wa dawa za kulevya anaweza kufanya lolote baya kwani baada ya matumizi maadili, mila, silka na utu kwake huwa haupo, hivyo ana kuwa mithiri ya mnyama na hivyo kuleta athari kubwa katika jamii.

Alisema familia zinakuwa zinapata tabu sana kwa kijana ndani ya familia akishajiingiza katika janga hili kwa kuwa vitu vya ndani hakuna kinachobaki.

"Sio tu kuwa familia pekee inaathirika, lakini hata taifa pia lina pata athari," alisema Aboud.

Alielezea kusikitishwa kwake na tabia mbaya na chafu iliyoanza kujitokeza kwa wauzaji kuwarubuni vijana wadogo wa miaka 13 hadi 16 kwa kuwapa bure kuanza kuvuta kwa matarajio akishazoea aweze kuwa na wateja wengi.

Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba, Omar Khamis Othuman, aliwataka masheha kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za watu wanaojishughulisha na dawa za kulevya waliopo katika shehia zao ili kuinusuru jamii kwa kuwa wengi wa wauzaji, wanunuzi na watumiaji wapo katika shehia zao.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Ramadhani Kailima (kulia), akisisitiza jambo wakati alipokagua ujenzi wa jengo la Idara ya Uhamiaji Makao Makuu mjini Dodoma juzi. **PICHA: WMNN**

# Waziri atuliza wasanii vikwazo

INATOKA UK. 5

Amewataka wasanii hao wasijione kuwa wao ni watu wanyonge badala yake wajiamini kwa vile ni watu wenye ushawishi mkubwa katika jamii kupitia kazi zao za sanaa.

Alisema hafla hiyo imelenga kuwatambua na kufungua ukurasa mpya wa kuhamasisha na kuendeleza shughuli za utalii kwa kutumia watu maarufu hususani wasanii.

Aliwaeleza kuwa hakuna haja ya kwenda Afrika Kusini au Dubai kwa ajili ya kutengeneza video badala yake watumie mandhari za nchini hali itakayofanya kazi za sanaa kuwa na vionjo vya kipekee tofauti na kazi nyingine za kisanaa zilizozoeleka.

"Nawahakikishieni msanii yeyote atakayetaka kutengeneza video yake katika hifadhi zetu za taifa hatakumbana na vikwazo vyovyote kama ilivyozoeleka," alisisitiza Kanyasu.

Aliwataka wasanii hao kuitumia nafasi kuziweka picha na video kwenye mitandao ya kijamii wakati wakiwa wametembelea vivutio vya utalii ili kujenga utamaduni wa watu kutembelea vivutio vyetu.

Kwa upande wake, msanii wa kizazi kipya, Peter Msechu, aliwataka wasanii wenzake kuitumia fursa hiyo ambayo walikuwa wakiitamani kwa muda mrefu.

Amesema kupitia fursa hiyo wasanii wataweza kuonesha uzuri wa Tanzania kwa jinsi ilivyojaliwa kuwa na utajiri wa vivutio vya utalii kwa mashabiki wao wa ndani na nje ya nchi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Jaji mstaafu Thomas Mihayo, aliwashauri wasanii hao kuwa wabunifu kwa kuitumia kazi zao za sanaa kwa kutumia mandhari ya vivutio vya utalii.

# Hapa ndipo ilipo miujiza ya JPM

INATOKA UK. 2

ikifanikiwa kwa kiasi kikubwa kudhibiti rushwa na ufujaji wa fedha za umma kwa kuchukua hatua dhidi ya wanaojihusisha na vitendo hivyo na kufanya uhakiki wa watumishi wa umma.

Changamoto kubwa kwa Rais Magufuli na serikali yake kutimiza azma ya kuinua uchumi wa Tanzania kupitia utekeleza wa miradi hiyo mikubwa, ni upatikanaji wa rasilimali fedha.

Ikumbukwe kuwa, wakati Rais Magufuli anaingia madarakani Novemba 5, 2015, nchi ilikuwa inakusanya wastani wa Sh. bilioni 850 kwa mwezi, lakini amefanikiwa kuwa na makusanyo ya wastani wa Sh. trilioni 1.3 kwa mwezi.

Hata hivyo, pamoja na jitihada zinazofanywa na serikali yake kuimarisha makusanyo ya nchi kwa kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato, kiwango kikubwa cha makusanyo kinatumika kulipa Deni la Taifa na mishahara ya watumishi wa umma.

Aprili mwaka jana, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alibainisha kuwa kati ya Sh. trilioni 1.3 zinazokusanywa na serikali kila mwezi, Sh. bilioni 550 hutumika kulipa mishahara ya watumishi wa umma, Sh. bilioni 600 hutumika kulipa Deni la Taifa na kiasi kinachobaki hutumika kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Kwa hiyo, kwenye Sh. trilioni 1.3 umebakiwa na Sh. bilioni 200 ambazo ndizo unatumia kuendesha serikali," Dk. Mpango alisema na kufafanua zaidi:

"Lakini humo namo kuna shughuli nyingine ambazo hazikwepeki. Kwa mfano, askari wetu shupavu wanalala nje, lazima serikali tuwape posho ya chakula, ndipo na sisi tunaweza kuendeleza vurugu huku bungeni, tukabishana, tukalala nyumbani kwa amani.

"Kuna mishahara ya majaji lazima ilipwe na marupurupu yao mengine, kuna viongozi wetu nao hawalali. Niwahakikishie, ni kawaida kabisa kumpigia Rais simu saa nane usiku, saa tisa yuko macho.

"Hawa viongozi wamebeba dhamana kubwa, lazima serikali iwahudumie. Kwa hiyo, unaponiuliza hizi nyingine zinaenda wapi, ninaweza nikaendelea na kuendelea.

"Kwa hiyo, ni rahisi sana kuhesabu hicho kinachoingia mfukoni, lakini ni muhimu kuangalia kinachotoka, zinatoka zinakwenda kwenye nini?

"Ulipaji wa Deni la Taifa inategemea, kwa mwezi inaweza ikatoka Sh. bilioni 600, tumewahi kwenda mpaka Sh. bilioni 900 kutegemeana na madeni hayo yanaiva wakati gani.

"Mwezi huu unaweza ukalipa Sh. bilioni 600 na kidogo, mwezi ujao ukalipa Sh. bilioni 700, ni kwa sababu ya tofauti ya ile mikopo inaiva wakati gani.

"Ukichukua wastani wa Sh. bilioni 550 mishahara, ukaongeza Sh. bilioni 600 kwa ajili ya kulipia Deni la Taifa, tayari Sh. trilioni 1.1 umeitumia kwa hivyo vitu viwili ambavyo huwezi kuvikwepa."

Wakati kiwango kikubwa cha makusanyo ya nchi kinatumika kulipa mishahara ya watumishi wa umma na Deni la Taifa, serikali ya awamu ya tano inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya mabilioni ya shilingi.

Kwa takwimu zilizotolewa na Waziri Mpango, ni dhahiri kwamba kiwango cha fedha kinachobaki kila mwezi baada ya kulipa mishahara ya watumishi wa umma na Deni la Taifa hakifikiki Sh. bilioni 200, lakini serikali imeendelea kutekeleza miradi mikubwa.

HABARI MIKOANI

# Vijana wamwagiwa mil. 300/- mawazo ya ubunifu, biashara

Na Mwandishi Wetu

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH ), kwa kushirikiana na Ubalozi wa Denmark nchini, imekabidhi mtaji wa zaidi ya Sh. milioni 320 kwa vijana washindi 24 ambao wameandaa mawazo bunifu ya kibiashara na kidijitali kwa lengo la kujiajiri.

Hatua hiyo imekuja baada ya Costech kupitia kituo atamizi cha teknohama Dar es Salaam (DTBi) kuandaa programu ya uwezeshaji vijana wabunifu kupitia mfumo wa digitali kwa lengo la kuwapatia mafunzo namna kuandaa mawazo ya kibiashara.

Akizungumza katika hafla ya kuwakabidhi mtaji washindi nane wa awamu ya pili ya mashindano hayo jijini Dar es Salaam juzi, Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alitoa wito kwa vijana kutokata tamaa kwa kuwa serikali inawatafutia fursa za kujikwamua kiuchumi kwa kutumia njia mbalimbali.

Alitoa wito kwa washindi ambao wamefanikiwa kupatiwa mitaji hiyo kufanya biashara kwa ari ili waweze kuwaajiri vijana wenzao.

Alisema vijana wanapoona kuna fursa yoyote wasisite kushiriki kwa kuwa penye ushindani ndipo mshindi hupatikana bila upendeleo.

"Lengo letu ni vijana kujiajiri na kutoa ajira kwa wenzetu kama sehemu ya kufikia uchumi wa kati kupitia viwanda.

Mkurugenzi wa Fedha na Utawala kutoka Atamizi ya Teknohama Dar es Salaam (DTBi), Makange Mramba, alisema katika programu hiyo ya kuwapatia mafunzo vijana wabunifu wa vyuo vikuu, awamu ya kwanza ya mashindano hayo washindi 16 walipatiwa mitaji ya Sh. milioni 205 wakati katika awamu ya pili vijana nane wamepatiwa Sh. milioni 120.

Alisema licha ya washindi hao kupatiwa mitaji kulingana na mawazo yao ya kibiashara, washiriki wengine ambao hawakushinda pia walipatiwa mafunzo ya kuandaa maandiko bunifu ya kibiashara ambapo tangu programu hiyo ianzishwe mwaka jana tayari washiriki zaidi ya 1000 wamepatiwa mafunzo.

"Kwa hakika tumevuka hata malengo yetu tuliyojiweka kwa zaidi ya asilimia 130," alisema.

Naye Meneja Biashara na Maendeleo (DTBi), Gasper Mdee, alifafanua kuwa licha ya vijana wachache kupatiwa mitaji hiyo, lakini mafunzo waliyopatiwa washiriki wote yanawawezesha kuandika maandiko bunifu ya kibiashara yenye ushawishi wa kupata mitaji katika taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Naye Kiongozi wa Sekta ya Maendeleo kutoka Ubalozi wa Denmark, Jema Ngwale, alitoa wito kwa taasisi mbalimbali zinazotoa fursa kwa vijana, kuwapa kipaumbele vijana wa kike ili waweze kujikwamua kiuchumi.

"Pia nawashauri vijana kupanua wigo kwa kubadilishana uzoefu kwa kupitia kwa marafiki ili kukuza wazo lako na kuona namna gani unaweza kuvuka, ili usivuke peke yako," alisema.

Mmoja wa washindi hao, Othuman Waziri alisema: "Wazo langu ni kutengeneza Boxpesa ambayo ni progamu maalumu itakayowasaidia Watanzania kutunza fedha zao kwa njia ya mitandao kwa muda maalum." Wakati Irene Sinare alisema wazo lake kutengeneza mifuko maalumu mbadala ambayo ina uwezo wa kupotea kwenye udongo ndani ya siku 180.




Kiongozi wa Sekta ya Maendeleo kutoka Ubalozi wa Denmark, Jema Ngwale (wa kwanza kushoto), akikabidhi hundi ya Sh. milioni 120 kwa vijana washindi nane wa mawazo bunifu ya kibiashara na kidijitali ambao walipatiwa mafunzo ya kuandaa maandiko bunifu ya kibiashara na Costech kwa kupitia Atamizi ya Teknohama Dar es Salaam (DTBi) kwa ufadhili wa Ubalozi wa Denmark. **MPIGAPICHA WETU**

# Madereva teksi waitwa kujiunga na mtandao nafuu

Na Enock Charles

UMOJA wa madereva wa teksi nchini (UWAMATADA) umewaomba madereva wa teksi kujiunga na mtandao wa magari ya usafirishaji abiria unaofahamika kwa jina la Quatax.

Mtandao huo unaoelezwa ni rafiki kwa madereva na unaojali maslahi na wajibu wao katika kutoa huduma za usafirishaji.

Akizungumza na madereva hao jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Umoja huo, Ramadhani Ashiru, amesema wameamua kujiunga na mtandao huo kwa kuwa unasikiliza kero za madereva na kujali maslahi yao ikilinganishwa na mitandao mingine nchini.

"Madereva teksi kwa miaka yote tangu mitandao hii ya usafirishaji abiria imeingia hatujawahi kujiunga na mtandao wowote... mtandao wa kwanza ni Quatax, ni mtandao wa Mtanzania mwenzetu mzalendo na amaeamua kujitolea baada ya hii mitandao mingine ya Uber," Ashiru alisema.

Alisema mitandao mingine iliyopo imekuwa ikimkandamiza dereva kwa kutokusikiliza madai yao ikiwamo viwango vidogo vya bei za huduma na hivyo kutokuwanufaisha madereva hao.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa kutoa huduma za usafirishaji wa teksi (Quatax), Daniel John, alisema lengo kubwa ya mtandao huo ni kuhakikisha panakuwa na ushirikishwaji wa madereva katika maamuzi yanayofanywa na mtandao huo ili kunufaisha pande zote mbili (dereva na abiria).

"Sisi tutahakikisha panakuwa na maamuzi ya pamoja na linapotokea tatizo madereva wenyewe waweze kuamua na si kuwaamrisha na hatuchagui gari kama wanavyofanya wengine," alisema.

Alisema madereva kulipa ni Sh. 3,500 kwa siku ni kidogo ikilinganishwa na asilimia 25 iliyowekwa na mitandao mingine ambayo alidai ni ukandamizaji kwa madereva hao.

## 'Marufuku kuomba vyoo kwa wahisani'

Na Shaban Njia, KAHAMA

SERIKALI imewapiga marufuku wananchi wa Kata ya Kilago, Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga kuacha tabia ya kuwaomba wahisani kuwajengea vyoo katika shule za msingi na sekondari, badala yake waombe kujengewa vyumba vya madarasa.

Anamringi Macha, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, alitangaza marufuku hiyo jana wakati wa ufunguzi wa kambi 28 za kata za Kilago na Iyenze za kujifunzia kusoma na kuandika kwa wanafunzi wa darasa la kwanza hadi la tatu kwa ufadhili wa Shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania.

Alisema ni marufuku kwa wananchi kuendelea kuwaomba wahisani michango ya kuwajengea vyoo katika shule za msingi na sekondari kwa kuwa wana uwezo wa kuvijenga, hivyo kuwataka kuomba kujengewa vyumba vya madarasa na maabara.

## Waonywa kukurupuka dakika majeruhi

Na Neema Emmanuel, MWANZA

WATANZANIA wamekumbushwa kujenga tabia ya kuwahi kwenye shughuli na masuala mbalimbali, badala ya kupuuza na kusubiri kukurupuka dakika za mwisho.

Aidha, wametakiwa kuachana na tamaduni za kupuuzia vitu kwani wamekuwa wakisubiri dakika za mwisho ndipo wanapojitokeza kufuatilia jambo, mazoea yanayoweza kuwakosesha fursa zinapojitokeza.

Ofisa Habari Mwandamizi Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Agnes Gerald, alisema wakati akizungumza na waandishi wa habari katika maonyesho ya 14 ya Afrika Mashariki yaliondaliwa na Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (TCCIA). Akizungumza katika maonyesho hayo yanaendelea jijini Mwanza alisema, changamoto inayowakabili hususani uandikishaji vitambulisho vya taifa ni wananchi kutoitikia wito mapema.

Alisema wanasubiria siku zinapoisha ndipo wanajitokeza kwa wingi, huku wakihitaji kuhudumiwa kwa wakati huo.

"Maonyesho yameanza tangu Agosti 30 hadi Septemba 8, lakini zikiwa zimebaki siku tatu au ile ya mwisho ndipo wananchi watajitokeza kwa wingi na wote watakuwa wanahitaji kupata huduma mara moja," alisema Agnes.

# TUGHE walia na upandishwaji vyeo

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

SUALA la kutopandishwa madaraja kwa wafanyakazi (watumishi) kwa wakati limegeuka kuwa tatizo sugu ambalo utekelezaji wake umekuwa mgumu, hivyo kuvunjika moyo na kushusha morali ya utendaji kazi.

Hayo yalibainishwa na Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya Tanzania (TUGHE) Mkoa wa Mwanza, Aloysius Mapembe, katika mkutano mkuu wa kazi wa chama hicho, ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Christopher Kadio. Alisema pale mtumishi anapofanyakazi kwa muda mrefu bila kupandishwa cheo, kunapunguza morali ya kufanya kazi kwa ufasihi ila anafanya kwa vile ni ajira.

Katibu wa TUGHE Mkoa wa Mwanza, Amini Msambwa, alisema yameshatolewa matamko mbalimbali ya upandishwaji wa madaraja kwa watumishi, lakini suala hili limekuwa likienda taratibu, wakati fulani limekuwa likileta shida na hali ya ubaguzi.

"Unakuta watumishi hawa hawa ambao walitangulia kuajiriwa hawajapandishwa daraja, huku aliyeanza kazi juzi juzi anapandishwa...mgeni rasmi kwa kuwa wewe ni Katibu Tawala ndio msimamizi wa wakurugenzi," alisema na kuongeza: "Tunaomba utusaidie, tatizo kubwa lipo kwa maofisa utumishi wetu kwani wamekuwa na kasi ndogo na haitoshi."

"Kuna malalamiko mengi mno, nikisema niyakusanye niyalete hapa utapata picha, nafikiri hata ofisini kwako yapo na kwa wakurugenzi pia yapo... agizo la serikali limeshatolewa, lakini hawapandi daraja unajiuliza shida ni nini maana wizarani wanasubiria tu hawa wapeleke jina wamwingize kule," alisena na kuendelea:

"Sasa hapo wanachochelewesha mfumo ni nini wakati walitamka kwenye baraza walikuwapo na wakapitisha maazimio ya watumishi wangapi wanapanda wangapi wanaajiriwa." Naye Katibu TUGHE tawi la Bugando, David Misinzo, alisema, zaidi wanapigania maslahi ya watumishi kuona kama yanatekelezwa ikiwamo la kupandishwa madaraja na mishahara ambalo wameisha lipingia sana kelele,ambalo linawafanya kuvunjika moyo na kutojituma bali. Katibu wa Mkoa Kamati za Wanawake TUGHE, Sekela Anthony, alisema, wanashukuru watumishi kuwatuma katika ofisi za serikali, hivyo aliwaomba wajitume na kufanya kazi.

Hata hivyo, Kadio alisema kama vyama vya wafanyakazi visingekuwapo kungekuwa na hali mbaya, lakini pamoja na kuwapo bado wanapata malalamiko sehemu nyingine za kazi sio katika maeneo ya chama hicho. Pia alikitaka chama hicho kuweka mikakati madhubuti ya utetezi wa wanachama wao.



Mfanyausafi akiondoa takataka kwenye mfereji wa maji ya mvua katika Barabara ya Uhuru, eneo la Shule ya Uhuru, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wafanyabiashara Tabora waeleza udhaifu wao

**Na Halima Ikunji, TABORA**

WAFANYABIASHARA katika Mkoa wa Tabora wengi hawajilipi mishahara kutokana na kazi zao wanazofanya, hivyo kukosa fursa ya kufahamu namna biashara zao zinavyokua au zinavyodorora.

Haya yamebainishwa na Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magese, wakati akizungumza na wafanyabiashara wa mkoa huo, na kubainisha kuwa wengi huwa hawajilipi mishahara na kufanya mahesabu yao kutokuwa vizuri.

"Inashangaza mfanyabiashara anawalipa wafanyakazi wake mshahara lakini yeye akiwa mkurugenzi hajilipi mshahara na pia huchanganya matumizi binafsi na ya biashara jambo amvalo huyumbisha mitaji yao.

Akizungumza katika kikao cha kupokea maoni ya wafanyabiashara juu ya huduma inayotolewa na NMB, Magese aliwaeleza kuwa kupitia mishahara yao ndio matumizi ya binafsi yanaweza kutoka huko na sio katika biashara. Aliwaeleza kuwa benki ya NMB ni benki yao na waitume kwani imejipanga kushirikiana nao katika kukuza uchumi wa Taifa. Mwenyekiti wa wafanyabiashara wenye akaunti benki ya NMB, Ahadi Mviombo, aliwahimiza wafanyabiashara kutenga sehemu ya mauzo yao kwa ajili ya kulipa madeni wanayokopa.

"Kama ukiweza kutenga angalau shilingi elfu tano kila siku kwa ajili ya marejesho mtihani utakuwa umeshinda," alisema.

Mfanyabiashara Mwalimu Mambo, aliipongeza NMB kwa utaratibu wake wa kuwafundisha wafanyabiashara namna ya kuweka mahesabu sawa na kutafuta faida.

"Tunashukuru kwa elimu tunayopewa na benki hii ambayo kwa kweli inatusaidia sana katika biashara zetu," alisema.

Kikao hicho chenye lengo la kupokea maoni kutoka kwa wafanyabiashara ziadi ya 300 wenye akaunti NMB pia kilihudhuriwa na wafanyakazi wa benki hiyo ambao walitoa elimu ya huduma mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo.

## Bunge watoto lahimiza kodi

**Na Elisante John, SINGIDA**

BUNGE la wanafunzi wa shule za msingi 20 katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida, limewataka Watanzania kuacha tabia ya kulalamikia kuwa kodi ni mzigo, badala yake waongeze kasi ya kulipa tozo hilo, ili waweze kupata uhalali wa kuhoji miradi inayotekelezwa na serikali.

Tabia ya jamii kushindwa kulipa kodi, imeelezwa na Bunge hilo, inachangia kudhoofisha mipango mingi ya serikali, hivyo kurudisha nyuma kasi ya kuwaletea wananchi maendeleo yaliyokusudiwa.

Hayo yalibainishwa na Nasra Ali wa Shule ya Msingi Kinyeto na Editer Mtinda wa Shule ya Mtinko, ambao walisema kodi ni ya lazima kwa kampuni, taasisi na raia wote, na kwamba wanalazimika kulipa kwa mujibu wa sheria.

Walisema kwa kufanya hivyo, serikali itapata mapato ya kujiendesha na kutupatia huduma wananchi. Mratibu wa Shirika la Maendeleo na Elimu Mtinko (MEDO), Hassan Rasuli, aliyeliandaa bunge hilo, alisema pamoja na mambo mengine, Bunge la watoto limedhamiria kushirikiana na serikali ya wilaya katika kuboresha elimu wilayani humo.

## Sababu kesi za ukatili kukwama

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZWA kuwa wazazi na walezi kushindwa kwao kutoa ushirikiano kwa polisi dhidi ya matukio ya ubakaji ndiyo sababu inayochangia kesi nyingi kuishia njiani.

Hayo yalisemwa na Jane Dotto, kutoka Kituo cha Polisi Osterybay iijini Dar es Salaam, wakati wa utambulisho wa kampeni ya 1_5_5 namlinda dhidi ya ukatili wa kingono ambayo imeandaliwa na TGNP Mtandao.

Jane ambaye yupo kituoni hapo katika dawati la jinsia, alisema ni wajibu wa wazazi kufuatilia kesi zawatoto wao waliofanyiwa ukatili wa kingono.

"Wazazi kutotoa ushirikiano kwa polisi kumesababisha kesi nyingi za ubakaji kuishia njiani," alisema.

Aliongeza wazazi wanaokaa kimya, huku mtoto kafanyiwa ukatili ni kumuumiza mtoto.

Ofisa Elimu Vielelezo Manispaa ya Ilala Amina Maulidi, alisema mtindo wa maisha nao ni moja ya sababu zinazosababisha kufanyika kwa ukatili.



# Wataalamu nyuklia wajadili mikakati uhifadhi mabaki vyanzo vya mionzi

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WATAALAMU wa teknolojia ya nyuklia kutoka nchi 21 duniani wamekutana kujadili mikakati mbalimbali ya uhifadhi wa mabaki ya vyanzo vya mionzi, ili kuepusha madhara kwa binadamu na mazingira.

Mkuu wa kitengo cha uhifadhi wa mabaki ya vyanzo vya mionzi katika Tume za Nguvu ya Atomiki (TAEC) na mratibu wa mkutano huo wa kimataifa, Mikidadi Swalehe, alisema mkutano huo ulikuwa wa siku tano uliofanyika wiki iliyopita jijini hapa.

Alisema lengo la kujadili mikakati hiyo ili kuboresha usalama wakati wa kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi ili kuepusha madhara. "Pia mkutano huu umekuja nchini kwa sababu Tanzania ina miundombinu mizuri ya jengo la kuhifadhi mabaki ya mionzi, ambalo baadhi ya nchi zingine hasa za Afrika hawana, wanaacha mabaki ya mionzi yanazagaa na kuleta madhara kwa bianadamu na mazingira," alisema.

Mikidadi alisema wanapohifadhi vizuri mabaki hayo, inasaidia kulinda vizazi vijavyo na athari za mabaki ya mionzi na kuwa na taifa imara.

Aidha, alisema Tanzania mbali na kuwa na jengo lenye miundombinu mizuri ya kuhifadhi mabaki hayo, pia TAEC imekuwa mstari wa mbele kutoa mafunzo kwa wahusika wanaotumia vifaa vyenye mionzi kama polisi, Jeshi la Ulinzi, hospitali na maeneo mbalimbali ili wafahamu jinsi ya kuepukana na madhara ya mionzi.

Alitoa wito juu ya umuhimu wa kukutana na wataalamu hao na kusisitiza umuhimu wa kusimamia usalama wa vyanzo vya mionzi sio la taifa moja, bali linahitaji ushirikiano wa nchi zote duniani, kuhakikisha vyanzo vyote vya mionzi, vinakuwa katika mikono salama, ili kuepusha madhara mbalimbali ikiwamo kutumika kwa vyanzo hivyo katika masuala ya ugaidi.

Mwakilishi wa Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) Dk. David Bennet, akitoa salamu za shirika hilo ambalo ni mwangalizi wa kimataifa wa masuala ya matumizi ya teknolojia ya nyuklia, alishukuru Tanzania hususani TAEC kwa kuwa mwenyeji wa mkutano huo na kuahidi kushirikiana na nchi wanachama, kuhakikisha teknolojia ya nyuklia inatumika kwa matumizi salama.

Mkutano huo ulifunguliwa na Mkurugenzi Mkuu wa TAEC, Prof. Lazaro Busagala na washiriki 30 kutoka nchi mbalimbali duniani walihudhuria.



Mbunge wa Jimbo la Simanjiro mkoani Manyara, James Ole Millya (kulia), Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Jackson Sipitieck (kushoto) na Katibu wa CCM wa Wilaya hiyo, Ally Kidunda, wakikagua miradi mbalimbali ya maendeleo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Serikali yataja wawekezaji wanaotakiwa

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

SERIKALI inawahitaji wawekezaji katika sekta ya utalii wenye kutii sheria za nchi ikiwamo kulipa kodi halali na kusaidia jamii inayowazunguka kutokana na faida wanayopata.

Kauli hiyo ilisemwa juzi na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, katika shehere ya miaka mitano ya shirika lisilo la kiserikali la Africa Foundation lililo chini ya kampuni mama ya And Beyond .

Kanyasu alisema wawekezaji wa aina ya kampuni ya And Beyond serikali inawahitaji sana kwa sababu inaisaidia serikali katika mambo mengi muhimu kwa jamii ikiwamo elimu, afya, maji na ujasiriamali, hivyo ni lazima serikali iiunge mkono kampuni hiyo kwa hali na mali.

Alisema And Beyond ina hoteli, lodge na camp site katika hifadhi kadhaa nchini na imeamua kufungua Taasisi ya Africa Foundation yenye malengo mbalimbali ikiwamo kuwasomesha wanafunzi wa elimu ya juu walioomba nafasi lakini wazazi wao hawana uwezo wa kifedha.

Kanyasu alisema kampuni za namna hiyo ndio serikali inazihitaji, kwani wanatumia faida wanazopata kusaidia jamii inayowazunguka tofauti na kampuni nyingine ambazo kwanza hazisaidii jamii inayowazunguka na pili hazilipi kodi na kunakuwa na migogoro mingi isiyokuwa na msingi.

"Serikali inahitaji wawekezaji wa utalii wenye kuisaidia serikali na kampuni ya And Beyond imeonyesha kuwa ni kampuni iliyokuja kuwekeza nchini sio kwa kutaka kujinenepesha tu bali imekuja kuwekeza na faida kuisaidia jamii, hii inapaswa kupongezwa kwa kazi hiyo nzuri na wengine wanapaswa kuiga mfano huo," alisema Kanyasu.

Akiwazungumzia wahitimu waliomaliza elimu ya juu na kupata shahada aliwataka kutumia elimu hiyo kuwahamasisha vijana wengine kusoma na kutumia elimu waliyopata kwenda maeneo waliyotoka kusaidia jamii na sio kukimbilia mjini na kuanza kutembea na vyeti mfukoni kutafuta kuajiriwa.

Aliwasisitiza vijana kutumia elimu waliyoipata kujiajiri mitaani na sio kusubiri kuajiriwa na serikali au taasisi binafsi, kwa kufanya hivyo ni kupoteza muda bure kwani ajira badala ya kuajiriwa tu bali ni kujiajiri na kuendeleza wengine kwa maslahi yao.

Naye Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya kale Zanzibar, Mahmoud Thabiti Kombo, alisema Zanzibar inajua umuhimu wa kampuni ya And Beyond kwani imefanya mambo makubwa kwa jamii inayozunguka miradi ya kampuni hiyo na inapaswa kuendeleza zaidi juhudi hizo bila ya wasiwasi na wasikate tamaa kwa hilo.

# Impala yapigia debe utalii ndani

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

WATANZANIA wamehimizwa kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii nchini ili kukuza utalii wa ndani na kujiweka katika nafasi nzuri ya kuwa mabalozi wa kuvitangaza vivutio vya utalii vya Tanzania kwa wageni.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Hoteli ya Impala ya jijini hapa, Randle Melleo, alipozungumzia mwelekeo wa sekta ya utalii na mchango wake katika kuongeza pato la taifa.

"Ni muhimu kujijengea utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kujieleza kwa wageni juu ya mazuri ya nchi katika sekta ya utalii hali itakayochochea kuongezeka kwa watalii," alisema na kuongeza kwamba Tanzania ni nchi ya pili dunia kuwa na vivutio vingi na vya kipekee vya utalii.

"Utalii wa ndani unapokuwa umeimalika ni rahisi kwa wageni kuzidi kuongezeka kutokana na ushawishi utakaofanywa na wale waliotembelea vivutio vya nchi," amesema na kupendekeza kwamba utalii wa ndani utajengeka kwa kuwapo na mpango wa watoto wa shule kutembelea vivutio angali wadogo, juhudi ambayo itawafanya watoto kufahamu sehemu nyingi za Tanzania na baadaye waweze kuwa mabalozi wa kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini. Alisema uwekezaji mkubwa umefanywa katika tasnia, ni ukarimu kwa wageni na ujenzi wa hoteli ili kuwafanya wageni wakae mahali pazuri na salama ili warudipo kwao watangaze vizuri vivutio vya Tanzania.

**"Ni muhimu kujijengea utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kujieleza kwa wageni juu ya mazuri ya nchi katika sekta ya utalii hali itaka...**



# Wasikitishwa skimu umwagiliaji kutengewa fedha kiduchu

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

WAKULIMA wanaojishughulisha na uzalishaji wa mazao ya chakula katika skimu ya umwagiliaji ya Soko, Wilaya ya Moshi, wameeleza masikitiko yao kuhusu mradi wa uimarishaji wa skimu hiyo kutengewa Sh. milioni 150 ambazo haziwezi kukidhi mahitaji ya kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda.

Skimu hiyo yenye wakulima zaidi ya 270, inahudumiwa na wananchi wa vijiji vya Kiterini, Soko na Kyomu.

Baadhi ya wakulima walitoa dukuduku lao jana, ikiwa ni siku chache baada ya kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Kilimanjaro, kupita eneo hilo la Kata ya Kahe Mashariki na kutoa maelekezo kwa serikali kuongeza fedha zaidi kwa ajili ya kuboresha skimu hiyo ili kuondoa malalamiko ya wakulima.

Mmoja wa wakulima hao Kabanga Ali, alisema kilimo cha umwagiliaji ili kiwe endelevu na chenye tija kuweza kufikia Tanzania ya viwanda, uwekezaji wa miundombinu ya kisasa, mitaji, maofisa ughani na uwezeshwaji kiuchumi wa wakulima ni mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa.

Naye Rehema Mgonja alisema: "Ukitazama kiasi cha fedha ambacho serikali imewekeza nadhani bado ni kidogo, ikilinganishwa na mahitaji ya viwanda vyetu hasa vya kuongeza mnyororo wa thamani mazao ya mpunga, mbogamboga na mahindi. Tunashauri serikali kwa maana ya halmashauri yetu kuongeza fungu la kuimarisha miundombinu ya skimu ya soko."

Greyson Badueli alisema pamoja na uwekezaji huo, bado wakulima wanaomiliki vitalu katika skimu ya Soko, hawajapewa elimu ya kutosha ya kujiunga katika vyama vya umwagiliaji.

Alisema jambo hilo kama litafanywa na watendaji wa serikali, litasaidia wakulima kusimamia na kuihudumia vyema miundombinu ya umwagiliaji ili iwe endelevu kwa kulipia ada za uendeshaji, matunzo na matumizi ya maji.

Juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Kastori Msigala, akizungumza na wakulima hao mbele ya Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, alisema mradi huo unaendeshwa na umoja wa wakulima wa umwagiliaji soko (Uwaso) na una jumla ya wakulima 270.

Sheria ya Umwagiliaji Namba 5 ya mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015, inahamasisha skimu za umwagiliaji kusimamiwa na kuendelezwa na vyama vya umwagiliaji ili ziweze kuwa na ufanisi zaidi.

Alisema chanzo cha maji ya skimu hiyo ni Mto Soko na kwamba zao kuu linalolimwa katika skimu hiyo ni mpunga, mboga, matunda na mahindi.

Alisema eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni hekta 400 na kwamba hadi sasa, eneo lililoendelezwa ni hekta 270 sawa na asilimia 67.5.

## Mil. 900/- kumaliza tatizo la maji Old Moshi

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

TATIZO la maji katika vijiji vya ukanda wa juu wa Kata ya Old Moshi, Jimbo la Moshi Vijijini, linatarajiwa kubaki historia baada ya ujio wa mradi mkubwa wa kusambaza maji wa Tella Mande, kutengewa zaidi ya Sh. milioni 905.4.

Mradi huo unaotekelezwa kwa fedha za serikali na wadau wa maendeleo, utawanufaisha wananchi 5,141.

Katika mahojiano maalum na Nipashe kuhusu utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Kastori Msigala, alithibitisha kuwa mradi huo utamaliza adha ya maji katika maeneo yenye upungufu.

"Hivi sasa tunalitafutia ufumbuzi wa kudumu tatizo kubwa la maji lililopo katika eneo la Old Moshi na maeneo ya jirani na kata hiyo, ambayo hayajawahi kupata maji ya bomba, ninataka niwahakikishie kwamba tatizo la maji sasa litabaki kuwa historia, haijalishi ni vijijini, maeneo ya milima na yasiyo ya milima," alisisitiza.

Katika maelezo yake, Msigala alisema mradi huo wa maji wa Tella Mande ambao ni wa maji ya mtiririko kutoka chemchem ya Masokeni, Kijiji cha Tema, Kata ya Mbokomu, una uwezo wa kuzalisha lita saba kwa sekunde, sawa na mita za ujazo 605 kwa siku.

Alieleza kuwa katika utekelezaji wa mradi huo wamekutana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na wananchi wenye maeneo ambayo kunatakiwa kujengwa matangi ya maji kugoma kutoa maeneo yao.

Changamoto nyingine kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo ni kutopatikana kwa nguvu kazi ya kuchimba mitaro katika eneo la mradi licha ya kuwapo kwa miamba migumu katika eneo la ujenzi.

"Hata hivyo, baada ya kufanyika vikao mbalimbali na kutoa elimu kila mara, wenye maeneo hayo hatimaye wamekubali kutoa maeneo ya kujenga matangi na serikali za vijiji zimeitikia wito na kuhamasisha kila kaya kutoa nguvu kazi ya kuchimba mitaro ili kufanikisha mradi huo," alieleza. Mradi huo utakapomilika utatoa fursa adhimu kwa wakazi wa ukanda huo wa kujikwamua kiuchumi kutokana na kupoteza muda mwingi kila siku kuhemea maji kwa zaidi ya saa mbili hadi tatu katika vijiji jirani.



Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na menejimenti ya Hoteli ya East Point, Manispaa ya Moshi baada ya kuzindua maboresho ya huduma mbalimbali za hoteli hiyo, mwishoni mwa wiki. Kushoto kwake (mwenye suti) ni Mkurugenzi wa hoteli hiyo, Rashidi Adam. **PICHA: JAMES LANKA**

# TRA yaikabili mipaka kukomesha magendo

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

MAMLAKA ya Mapato (TRA), imeongeza makali ya kukabiliana na wafanyabiashara wajanja wanaojihusisha na biashara za magendo katika njia za panya ili kukwepa kuvuka kisheria mipaka ya Tarakea, Holili na West Kilimanjaro.

TRA imesema kuanzia sasa, itawapiga faini ya Sh. milioni nne papo hapo wafanyabiashara watakaokamatwa.

Meneja wa TRA mkoani Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, wakati akifungua semina ya wanachama wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Kaskazini kiitwacho ELCTND Saccos.

"Sisi kama TRA, hatupo tayari kumsamehe mfanyabiashara yeyote atakayekamatwa hajatoa risiti ama mtu yeyote atakayenunua bidhaa bila kudai risiti na kwamba adhabu yake ni kumlipisha faini ama kwenda jela na kutaifisha bidhaa zilizokamatwa.

"Jamani hakuna msamaha kwa atakayekamatwa na mali au bidhaa za magendo, kwa sababu biashara ya magendo inaileteа hasara kubwa serikali kutokana na kukosa mapato yake na vilevile kusababisha wananchi kukosa huduma muhimu."

Kwa mujibu wa Mwangosi, idadi kubwa ya wanaokamatwa kutokana na biashara za magendo ni kinamama ambao hutumia njia za panya kufanikisha mambo yao hasa kukwepa kulipa kodi.

Wiki chache zilizopita TRA ilitangaza mkakati wake mpya wa kupambana na wafanyabiashara wakorofi waliokosa uaminifu, ikieleza kuanzisha zoezi maalumu la kujilipa kodi kutoka katika akaunti za kibenki za wateja wao, kwa kuchukua fedha hiyo moja kwa moja kwenye akaunti ya benki ya mteja mwenyewe.

Utaratibu wa kukata kodi moja kwa moja katika akaunti ya benki ya mteja, inaelezwa kuwa utakuwa ukifanyika kwa wateja wakaidi kulipa kwa hiari.

"Wapo walipa kodi ambao hawalipi kodi kwa wakati na kusababisha kuwa na madeni ya kodi, sasa hivi TRA tutakuwa tukichukua kodi zetu moja kwa moja kwenye akaunti za benki za wateja hao," alisema Mwangosi.

Alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo kwa sasa katika mpango huo wa kuchukua fedha ya kodi moja kwa moja kwenye akaunti ya benki ni baadhi ya walipakodi ambao taarifa zao zipo TRA, zinatofautiana na taarifa za benki.

Pia alisema wapo baadhi ya wateja wanaoandika hundi kwa ajili ya kulipa kodi, lakini wanapofika benki wanakuta fedha hizo hazipo katika akaunti ya mteja na hivyo kusababishia usumbufu maofisa wake.

Kwa sasa maofisa wa mamlaka hiyo, wamekuwa wakipita mtaa kwa mtaa kuwaelimisha walipa kodi kutambua umuhimu wa kulipa kodi kwa wakati pamoja na kusikiliza kero zao zinazowakabili katika masuala ya kodi.

Alieleza kuwa, moja ya changamoto waliyobaini katika utekelezaji wa kutembelea wateja, wapo wafanyabiashara ambao hawajalipa kodi kwa muda mrefu, tangu mwaka 2016 na wengine wakiwa hawatumii mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EfD).

Akitolea mfano hujuma zinazofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu, Mwangosi alisema siku mbili zilizopita, waliwatembelea wafanyabiashara 51 na kati yao, 19 walikutwa wamevunja sheria mbalimbali za kikodi na kutozwa faini.

Nipashe
Spotika



NYOTA 7 WANAOVAA NA KUITENDEA HAKI JEZI NA. 7 UK. 20



## ISIKUPITE

Harry Kane amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga mabao 25 na zaidi (25+), katika mechi 40 za kwanza alizocheza timu ya Taifa ya England tangu Gary Lineker alipofunga mabao 27. Na hat-trick aliyofunga dhidi ya Bulgaria juzi ni ya 13 kwake katika klabu na timu ya taifa (Spurs 11, na England hat-trick mbili).

# FURUKUTA...

Mshambuliaji wa England, Marcus Rashford (katikati), akihaha kumpita beki wa Bulgaria, Nikolay Bodurov kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 iliyopigwa Uwanja wa Wembley na wenyeji kushinda 4-0. **HABARI UK. 30**



# 10-BORA USAJILI KLABU ZA ULAYA

MAGUIRE

**LONDON,** England

KWA kawaida kipindi cha majira ya joto ni muda ambao klabu nyingi zinakuwa bize kwenye kuimarisha vikosi vyao.

**Dirisha la usajili kwa msimu wa 2019-20 lilifungwa Septemba 2, kwa nchi za Italia, Hispania, Ujerumani na Ufaransa, huku lile la Ligi Kuu ya England likifungwa Agosti 8, mwaka huu.**

Klabu za England kwa pamoja ziliongoza kwa kutumia fedha nyingi zaidi kwenye usajili, kwani kiasi cha euro bilioni 1.54 zilitumika.

Juventus, Napoli, Roma, AC Milan na Inter Milan za Italia kwa pamoja zilitumia kiasi cha euro milioni 690 kwenye usajili, huku klabu za Ligi ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern na Dortmund kwa pamoja zilitumia euro milioni 271.

Klabu tatu kubwa za Hispania, Real Madrid, Barcelona, na Atletico kwa pamoja zilitumia kiasi cha euro milioni 806.

Real Madrid ndio ilitumia fedha nyingi zaidi nchini Hispania, kwani kiasi cha euro milioni 307.5 zilitumika.

Hapa tunaangalia usajili wa wachezaji 10-bora uliofanywa na klabu za Ulaya, tiririka nayo...

**10. ROMELU LUKAKU (EURO MIL. 65)**

Lukaku aliondoka Manchester United na kwenda kujiunga na klabu ya Serie A, Inter Milan kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 65. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, raia wa Ubelgiji aliwasili Italia, huku akitoka kufunga mabao 33 kwenye Ligi Kuu ya Ubelgiji akiwa na Anderlecht na mabao 113 katika misimu tisa aliyokaa kwenye Ligi Kuu ya England (Everton 68, Manchester United 28 na West Ham-17).

**9. RODRIGO HERNANDEZ (EURO MIL. 70)**

Hernandez, ambaye anajulikana kama Rodri, ni mchezaji wa tatu kwa thamani kubwa kwenye Ligi Kuu ya England wakati akiwa amesajiliwa kipindi hiki cha majira ya joto. Manchester City ilimsajili Rodri kutoka Atletico Madrid ya Hispania kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, raia wa Hispania alitua England baada ya kucheza kwa misimu minne akiwa kwenye La Liga (misimu mitatu na Villareal na mmoja na Atletico).

**8. FRENKIE DE JONG (EURO MIL. 75)**

'Gogo' huyu mwenye umri wa miaka 22, kiungo wa kati alisajiliwa na mabingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, Barcelona kwa euro milioni 75 baada ya kuwa na msimu wa kuvutia kule Ajax.

De Jong ametua Hispania baada ya kucheza kwa misimu mitano kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, katika klabu za Willem II na Ajax.

**7. NICOLAS PEPE (EURO MIL. 80)**

Pepe alifunga mabao 22 na kutoa pasi za mwisho 11 na amesajiliwa Arsenal iliyoishinda Napoli kwenye mbio za kuwania saini yake kwa euro milioni 80 kutoka klabu ya Lille.

Pepe mwenye umri wa miaka 24, raia wa Ivory Coast ametua England baada ya kucheza Ufaransa kwa misimu mitatu, ambako alifunga mabao matatu akiwa na Angers na mabao 35 akiwa na Lille.

**6.LUCAS HERNANDEZ (EURO MIL. 80)**

Mabingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bayern Munich walimsajili beki huyu wa kati wa Ufaransa kutoka Atletico Madrid kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 80.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ni mshindi wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa alitua Ujerumani baada ya kucheza kwa misimu mitano kule Atletico.

**5. MATTHIJS DE LIGT (EURO MIL. 85.5)**

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 20, raia wa Uholanzia alikuwa nguzo muhimu kwa Ajax wakati wakitoa Juventus kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na wakaishia nusu fainali. Juventus ilitumia euro milioni 85.5 ili kupata huduma yake.

**4. HARRY MAGUIRE (EURO MIL. 87)**

Maguire alijiunga na Manchester United kutoka Leicester City kwa ada ya euro milioni 87 na kumfanya kuwa beki ghali zaidi duniani.

Maguire mwenye umri wa miaka 26, alianza kuichezea Sheffield United kabla ya kutua Hull City na Leicester City na kisha Old Trafford.

**3. EDEN HAZARD (EURO MIL. 100)**

Kiungo huyu mshambuliaji mwenye umri wa miaka 28, alijiunga na Real Madrid akitokea Chelsea kwa ada ya euro milioni 100. Hazard ametua Hispania baada ya kufunga mabao 36 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, misimu mitano akicheza Lille na alifunga mabao 85 kwenye Ligi Kuu ya England kwa kipindi cha misimu saba aliyocheza pale Chelsea, akishinda mara mbili taji la Ligi Kuu, mawili ya Europa, moja la FA Cup na la Ligi.

**2. ANTOINE GREIZMANN (EURO MIL. 120)**

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 28, alisajiliwa na Barcelona kutoka Atletico Madrid kwa ada ya uhamisho ya euro milioni 120.

Akiwa ameanza kucheza La Liga msimu wa 2010-11, Greizmann alifunga mabao 46 katika misimu minne aliyocheza kule Real Sociedad na mabao 94 katika misimu mitano aliyocheza Atletico Madrid.

**1. JOAO FELIX (EURO MIL. 126)**

Raia huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 19, alisajiliwa na Atletico Madrid akitokea Benfica kwa ada iliyoweka rekodi ya klabu hiyo ya euro milioni 126.

Felix alifunga mabao 15 kwa msimu aliocheza pale Benfica na amekuwa akifananishwa na magwiji wa Ureno Rui Costa na Joao Pinto.

**JE, WAJUA?**



England haijawahi kupoteza mechi 42 zilizopita za kuwania kufuzu michuano ya Euro ama Kombe la Dunia (imeshinda 33, sare tisa), tangu ilipopoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Ukraine Oktoba 2009.

MICHEZO

# WAGENI HOI KWA 'KUTUPIA' LIGI BARA



Donald Ngoma, straika aliyeweka rekodi ya kuwa mfungaji kwenye raundi ya kwanza mara mbili 2015/16 na 2017/18, akiwa na Yanga.

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza tangu Ligi Kuu msimu wa 2013/14, ni mchezaji mmoja tu wa kigeni amefunga bao kwenye mechi za raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Baada ya mechi 10 za ufunguzi wa Ligi Kuu msimu huu, straika hatari wa Simba, Meddie Kagere ndiye mchezaji pekee kutoka nje ya nchi aliyefunga goli, huku waliobaki wote wakiwa ni Watanzania.**

Straika huyo wa Simba raia wa Rwanda, alifunga mabao mawili kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu, timu yake ikicheza dhidi ya JKT Tanzania na kushinda 3-1, Agosti 29 kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Rekodi zinaonyesha kuwa hii ni mara ya kwanza tangu msimu wa 2013/14 ambapo mchezaji pekee wa kigeni alipofunga kwenye mechi ya ufunguzi, naye ni Haruna Niyonzima akiwa Yanga.

Baada ya hapo misimu yote iliyofuata kulikuwa na zaidi ya mchezaji mmoja wa kigeni waliokuwa wakifunga kwenye mechi za kwanza za ufunguzi wa Ligi Kuu...

**1. HARUNA NIYONZIMA (2013/14)**

Kiungo huyu ambaye kwa sasa anaichezea AS Kigali ya nchini kwao Rwanda, ndiye mchezaji pekee wa kigeni aliyefunga kwenye mechi za raundi ya kwanza ya Ligi Kuu msimu wa 2013/14.

Ilikuwa ni Agosti 24 kwenye Uwanja wa Taifa, akiichezea timu ya Yanga ambayo aliisaidia kuondoka na ushindi wa mabao 5-1 dhidi ya Ashanti. Mabao mengine yalifungwa na Jerry Tegete, mawili, Simon Msuva, na Nizar Khalfan, la kufutia machozi la Ashanti likifungwa na Shaaba Juma.

**2. DIDIER KAVUMBAVU NA AMISSI TAMBWE (2014/15)**

Ni msimu ambao wachezaji wa kigeni waliongezeka kufunga kwenye mechi za ufunguzi ambapo, mastraika wa Kirundi walifanya vitu vyao wakiwa Bongo, msimu wa 2014/15.

Ilikuwa ni Septemba 20, 2014, wakati Mrundi Didier Kavumbagu alipoweka rekodi ya kufunga bao kwenye mechi ya ufunguzi, timu yake ya Azam FC ikicheza dhidi ya Polisi Morogoro, Uwanja wa Azam Complex. Tambwe alifunga kwenye mechi ya raundi ya kwanza, Septemba 21, 2014, timu yake ya Simba ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Coastal Union.

**3. KIPRE TCHETCHE, HAMISI KIIZA NA DONALD NGOMA (2015/16)**

Msimu wa 2015/16, kulikuwa na wachezaji watatu wa kigeni waliofunga mabao kwenye mechi za raundi ya kwanza ya Ligi Kuu.

Raia wa Ivory Coast, Kipre Tchetche, akiichezea Azam FC, alifunga bao Septemba 12, 2015, timu yake ikiichapa Prisons mabao 2-1, na siku hiyo hiyo, Mganda Hamisi Kiiza akiwa na timu ya Simba alifunga bao pekee, timu yake ikishinda bao 1-0 dhidi ya African Sports kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, na Septemba 13, 2015 Mzimbabwe Donald Ngoma alifunga goli kwenye mechi ya raundi ya kwanza, timu yake ya Yanga ikiifunga Coastal Union mabao 2-0 Uwanja wa Taifa.

**4. LAUDIT MAVUGO, FREDRICK BLAGNON NA HOOD MAYANJA (2016/17)**

Raundi ya kwanza ya msimu wa 2016/17 pia kulikuwa na wageni watatu ambao walifanikiwa kutikisa nyavu. Mzambia Laudit Mavugo alifunga bao Agosti 20, 2016, akiisaidia timu yake ya Simba kuondoka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Ndanda FC kwenye Uwanja wa Taifa.

Kwenye mechi hiyo hiyo, raia wa Ivory Coast, Fredrick Blagnon, aliifunga pia Simba bao kwenye ushindi huo huo dhidi ya Ndanda, huku Uwanja wa Azam Complex, Azam ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya African Lyon. Bao la Lyon lilifungwa na Mganda Hood Mayanja.

**5. EMMANUEL OKWI, YAHAYA MOHAMED NA DONALD NGOMA (2017/18)**

Maproo watatu waliingia kwenye orodha ya wafungaji kwenye mechi za raundi ya kwanza msimu wa 2017/18. Mganda Emmanuel Okwi, alifunga mabao manne kwenye mechi ya ufunguzi wa ligi msimu huo, Agosti 26, timu yake ya Simba ikiifunga Ruvu Shooting mabao 7-0.

Yahaya Mohamed, raia wa Ghana, akiichezea Azam FC, alifunga bao siku hiyo likiwa bao pekee Azam ikiifunga Ndanda FC, huku Agosti 27, Mzimbabwe Donald Ngoma akifunga bao kwenye mechi za raundi ya kwanza, Yanga ikitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Lipuli.

**6. MEDDIE KAGERE NA HERITIER MAKAMBO (2018/19)**


Msimu uliopita, wachezaji Meddie Kagere wa Simba na Heritier Makambo wa Yanga, ndiyo wachezaji wa kigeni waliotikisa nyavu kwenye mechi za raundi ya kwanza ya Ligi Kuu.

Agosti 22, 2018, Kagere akiwa na timu yake ya Simba, Uwanja wa Taifa, alifunga bao pekee, Simba ikiichapa Prisons 1-0 na Agosti 23, Makambo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, akifunga Uwanja wa Taifa, Yanga ikiifunga Mtibwa Sugar 2-1.

**7. MEDDIE KAGERE (2019/20)**

Msimu huu ni Kagere pekee ndiye mgeni aliyefunga bao kwenye mechi ya raundi ya kwanza na kurejea kile cha msimu wa 2013/14 wakati Niyonzima pekee aliyefanya hivyo.

**NJE YA UWANJA**



TANGU alipoanza kuichezea Arsenal kwenye Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza Agosti 2016, hakuna mchezaji yeyote aliyesababisha penalti nyingi kwenye michuano hiyo zaidi ya tano za Granit Xhaka.



# KLABU 4 ZILIZOFANYA USAJILI WA OVYO ULAYA

**LONDON,** England

HUKU msimu mpya wa 2019/2020 ukiendelea, kuna klabu ambazo zimefanya usajili wa maana wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto, huku nyingine zikilamba garasha.

**Dirisha la usajili lilifunguliwa Julai Mosi na kwa England lilifungwa mapema, huku kwa ligi nyingine za Ulaya likifungwa Septemba 2, mwaka huu.**

Makala haya yanakuchambulia klabu ambazo zilifanya usajili wa ovyo zaidi barani Ulaya, twende sasa...

### 4. CHELSEA

Chelsea walijikuta kwenye wakati mgumu baada ya kufungiwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), na hivyo haikuwa na namna yoyote ya kuweza kuongeza wachezaji katika kikosi chake.

Wachezaji pekee ambao waliwaongeza kwenye kikosi chao ni Christian Pulisic na Mateo Kovacic ambao walishasajiliwa kabla ya kufungiwa, huku wachezaji waliokuwa wanacheza kwa mkopo wakilazimika kuitwa kurejea.

Kocha Frank Lampard alitua hapo na kukutana na wakati mgumu baada ya nyota wao Eden Hazard kuondoka na kutua kule Real Madrid.

Hazard alikuwa mmoja wa wachezaji bora wa kikosi hicho kwa kipindi cha miaka saba na hivyo kuondoka kwake kumewaweka Chelsea kwenye wakati mgumu zaidi msimu huu.

### 3. REAL MADRID

Huku ikiwa imetumia zaidi ya euro milioni 300 kwa kusajili wachezaji wapya kipindi cha majira ya joto, lakini inaonekana kwamba, haikuchanga karata zake vizuri.

Los Blancos hao chini ya kocha Zinedine Zidane, wamejikuta bado hawajapata wachezaji bora wa kuleta ushindani kwenye kikosi hicho.

Walijaribu mara kadhaa kutaka kumsajili Paul Pogba kutoka Manchester United, lakini mpango huo ulishindikana, huku pia wakishindwa kuwauza Gareth Bale pamoja na James Rodriguez.

Pamoja na kwamba wamemsajili Hazard kutoka Chalsea, lakini hadi sasa mchezaji huyo hajacheza mchezo wowote wa Ligi Kuu kutokana na kuwa majeruhi.

Safu ya kiungo ya Real Madrid imebaki kuwa na Luka Modric na Toni Kroos, kwani jaribio lao la kutaka kuwasajili viungo, Donny van de Beek na Bruno Fernandes lilishindikana.

Mbaya zaidi ni kwamba wamemtoa Dani Ceballos kwa mkopo ambaye anacheza kule Arsenal ambako ameonesha kiwango kikubwa katika mechi nne alizocheza hadi sasa.

### 2. JUVENTUS

Juventus ilizipiku klabu nyingi Ulaya na kufanikiwa kumsajili Matthijs de Ligt kutoka Ajax.

Hata hivyo, usajili wa Mholanzi huyo wa euro milioni 75 ni utamu mchungu kwani beki na nahodha wao, Giorgio Chiellini ameumia na atakuwa nje kwa muda mrefu, hivyo 'dogo' huyo mwenye umri wa miaka 19, De Ligt atalazimika kubeba mikoba yake.

Lakini kinda huyo bado anahitaji muda zaidi wa kupata uzoefu hasa kutokana na umri wake.

Pia Bianconerri hao waliwasajili Aaron Ramsey na Adrien Rabiot ambao walitua hapo wakiwa wachezaji huru baada ya kumaliza mikataba yao na timu walizokuwa wanazichezea.

Danilo ni mchezaji ambaye ameshindwa kuwa na nafasi ya kudumu katika kikosi cha kwanza, huku wakimruhusu Moise Kean kuondoka.

Mshambuliaji Paulo Dybala ambaye aliripotiwa kutakiwa na klabu kadhaa kipindi cha majira ya joto, msimu uliopita kiwango chake kiliporomoka na hivyo kwenye safu ya ushambuliaji watakuwa wakimtegemea Cristiano Ronaldo pekee chini ya kocha wao mpya, Maurizio Sarri.

### 1. MANCHESTER UNITED

Manchester United imekuwa kwenye kiwango cha ovyo tangu kuondoka kwa kocha, Sir Alex Ferguson.

Klabu hiyo msimu uliopita ilikuwa na kiwango kibovu zaidi na kipindi cha dirisha la usajili la majira ya joto walifanikiwa kuwasajili, Aaron Wan-Bissaka na Daniel James pamoja na Harry Maguire ambaye alisajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia kwa kuwa beki ghali zaidi.

Alexis Sanchez na Romelu Lukaku wametimkia Inter Milan, huku pia Matteo Darmian naye akiondoka pamoja na Chris Smalling ambaye ametua AS Roma kwa mkopo.

Kocha, Ole Gunner Solskjaer amelazimika kuwatumia zaidi wachezaji vijana, huku safu yake ya ushambuliaji akiwatumia zaidi Anthony Martial, Marcus Rashford, Daniel James na Mason Greenwood.

Jesse Lingard ambaye amekuwa hana mchango wowote wa goli tangu mwaka 2018, ameendelea kuwa kiungo mshambuliaji katika klabu hiyo, huku mchango wake ukiwa bado si mkubwa.

Man United katika dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto, haikuweza kufanya usajili mkubwa zaidi, hivyo haina kikosi kipana msimu huu.

Ikiwa imeanza vibaya kwenye mechi za Ligi Kuu ya England msimu huu kwa kushinda mechi moja, kupoteza moja na sare mbili. Msimu huu wanaonekana watakuwa kwenye wakati mgumu zaidi kwani hawana wachezaji wa maana.

Kikosi cha Man United kitakuwa kikiwategemea zaidi wachezaji chipukizi kwenye mbio za ubingwa na mashindano mengine ya Ulaya.

## Nukuu

"Ninawajua Waargentina wazi, na ninamjua [Edinson] Cavani. Na nilikutana na Neymar Jr. Ninajisikia fahari kuwa mchezaji mwenzao. Mimi ni straika, ninapenda kufunga mabao. Itakuwa vizuri kucheza mbele na washambuliaji wa kushangaza katika kikosi hiki," **Mauro Icardi baada ya kutua Ligue 1, kuitumikia Paris Saint-Germain.**



"Kwanza tuangalie kile nitakachokifanya Roma na mwisho wa msimu nafikiri nitaangalia uwezekano wa kubaki au kwenda sehemu nyingine, kwa sasa sijui, siwezi kusema chochote kuhusu majaliwa yangu, tuangalie kwanza mechi zinazokuja," **Henrikh Mkhitaryan akizungumzia mustakabali wake baada ya kutua Roma akitokea Arsenal.**




"Kocha anatakiwa kuchagua timu ambayo itapigania ubingwa na kama hatashinda yeye ndiye atabeba mzigo wa lawama. Nimekuwa kwenye soka kwa muda mrefu, nimecheza mechi zote katika klabu kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita," **kiungo wa Manchester United, Nemanja Matic, akimtupia dongo kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer.**



# WACHEZAJI WALIOREJEA NYUMBANI MSIMU HUU


HARUNA SHAMTE

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara imekamilika kwa timu zote 20 kucheza mechi za kwanza, kuna baadhi ya mambo mbalimbali yamejitokeza, huku ikishuhudiwa baadhi ya wachezaji wakizichezea timu zao za zamani baada ya kurejea tena.

**Wachezaji hao zamani walikuwa kwenye timu hizo, lakini waliondoka kwa sababu mbalimbali, ikiwamo viwango vyao kushuka, kukosa namba za kudumu au kutafuta maisha, lakini kwa msimu huu wa Ligi Kuu 2019/20 wamerejea tena kwenye timu hizo...**

1. Benedict Tinoco- Kagera Sugar

Amerejea tena Kagera Sugar. Ni golikipa wa zamani wa timu hiyo, kabla ya kuihama mwaka 2015 na kujiunga na Yanga.

Alikaa kwenye timu hiyo kwa msimu mmoja, lakini hakuwa na msimu mzuri, kabla ya kutolewa kwa mkopo Mtibwa Sugar.

Huko alikuta kipa mkongwe Shaaban Kado, lakini akapambana hadi kuwa kipa namba moja, akionyesha uwezo wa hali ya juu, mpaka kusababisha timu hiyo kutwaa Kombe la FA na kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho msimu wa 2017/18.

Hata msimu uliopita alikuwa kwenye kiwango cha hali ya juu, kiasi cha klabu yake ya zamani Kagera Sugar ikamezea mate na kumrejesha nyumbani msimu huu.

**2. MOHAMED SAID NDUDA- MTIBWA SUGAR**

Msimu huu Nduda ameanza kuichezea klabu yake ya zamani, Mtibwa Sugar. Amerejea nyumbani akitokea kwenye klabu ya Ndanda FC.

Alikuwa kwenye klabu ya Mtibwa Sugar kabla hajasajiliwa na Simba mwaka 2017, lakini alidumu kwa msimu mmoja tu kabla ya klabu hiyo haijamtoa kwa mkopo kwenda Ndanda FC.

Msimu huu amemaliza muda wake wa mkopo na kuwa huru. Akaamua kurejea kwenye klabu yake ya zamani, Mtibwa Sugar.

**3. HARUNA SHAMTE- SIMBA**

Shamte amerejea tena kwenye klabu hiyo baada ya miaka mitano. Beki huyo wa kulia, alijiunga na klabu ya Simba mwaka 2008 na kuichezea kwa mafanikio hadi 2014, alipoondoka na kujiunga na klabu ya JKT Ruvu ambayo kwa sasa inajulikana kama JKT Tanzania. Mwaka 2016 aliondoka na kwenda kujiunga na Mbeya City, hadi 2018 alipochukuliwa na Lipuli.

Akacheza kwa mafanikio makubwa msimu mmoja tu, kabla ya Simba kumrejesha tena nyumbani msimu huu.

**4. SHAABAN CHILUNDA- AZAM**

Straika Chilunda naye ni mmoja wa wachezaji waliorejea nyumbani kwenye klabu yake ya Azam FC. Tofauti na wengine ambao walikuwa kwenye klabu za hapa nchini, yeye alikuwa nchini Hispania akicheza soka la kulipwa.

Aliondoka nchini mwaka juzi kwenda kujiunga na CD Tenerife. Hakuwapo kwenye Ligi Kuu msimu uliopita. Hatimaye msimu huu amerejea tena Azam FC, klabu ambayo alijiunga nayo tangu mwaka 2012.

**5. MIRAJI ATHUMANI- SIMBA**

Ni mmoja kati ya vijana waliolelewa na kupandishwa kutoka kwenye kikosi cha pili cha Simba 2013.

Hata hivyo, hakuna mchezaji aliyeweza kupata namba kwenye kikosi cha kwanza, hivyo 2015 winga huyo asilia, anayemudu kucheza pande zote kushoto na kulia akaondoka kwenda kuichezea klabu ya Toto African ya Mwanza.

Mwaka unaofuata akaondoka na kwenda kujiunga na Mwadui FC, kabla ya msimu uliopita kuichezea Lipuli FC.

Alicheza kwa mafanikio makubwa kiasi cha kuwavutia tena Simba, iliyoamua kumsajili na kumrejesha tena nyumbani alikoondoka miaka sita iliyopita.

**6. ERICK KYARUZI- KAGERA SUGAR**

Kagera Sugar imemrejesha tena kundini beki wake wa kati, Erick Kyaruzi ambaye msimu uliopita alichezea Mbeya City.

Alijiunga na Mbeya City 2017, baada ya mkataba wake na Kagera Sugar kumalizika. Kabla ya hapo alikuwa amesimamishwa na klabu ya Kagera Sugar kwa madai ya kuihujumu timu hiyo ilipocheza dhidi ya Yanga msimu wa 2016/17 na kufungwa mabao 6-2.

Akiwa Mbeya City alionekana kuwa kwenye kiwango cha hali ya juu kiasi cha waajiri wake wa zamani kusahau yaliyopita na kuamua kumrejesha ili kuanza upya.

**7. DOTTO SHAABAN- PRISONS**

Prisons imemrejesha tena kiungo wake za zamani Dotto Shaaban baada ya kumshuhudia akitamba na kuwa mmoja wa wachezaji nyota kwenye Ligi ya Mabingwa wa Mkoa wa Dar es Salaam, akiichezea timu ya Magereza Dar.

Mchezaji huyo aliichezea Prisons msimu wa 2017/18, lakini alipata majeraha yaliyomweka msimu mzima nje, na alipopona akaenda kujiunga na Magereza Dar. Uwezo wake alioonyesha ulimfanya kukumbukwa tena na waajiri wake wa zamani na kumrudisha kumpa nafasi nyingine.

**8. JABIR AZIZ- JKT TANZANIA**

Ni kiungo mbunifu mwenye uwezo mkubwa ambaye msimu huu anaichezea JKT Tanzania, timu ambayo alishawahi kuichezea mwaka 2014, wakati huo ikiitwa JKT Ruvu.

Ni mchezaji mkongwe ambaye safari yake ya soka ilianzia klabu ya Ashanti FC 2007, kabla ya kijiunga na Simba 2008 na kuitumikia kwa miaka miwili, 2010 akatimkia Azam FC.

Baada ya hapo ndipo alipojiunga na JKT Ruvu, kabla ya kwenda Mwadui, Ruvu Shooting na Ndanda, lakini msimu uliopita alikuwa akiichezea timu iliyoshuka daraja ya African Lyon na kufanya makubwa kiasi cha JKT Tanzania kuamua kumrejesha nyumbani.

**NAJUA WAJUA**



Kieran Trippier (Atletico Madrid) amekuwa mchezaji wa kwanza anayecheza soka klabu ya Hispania kuichezea timu ya Taifa ya wanaume ya England tangu David Beckham (Real Madrid) alipofanya hivyo Juni 2007.

SOKA

# SOLSKJÆR NA MKAKATI WAKE MAN UNITED



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjær amesema licha ya wachezaji wake kuanza wakiwa 'wamepoa' msimu huu, ana imani kwamba watawasha moto siku zijazo, hasa eneo la ushambuliaji.

**Solskjær akasema kwamba wapo vi zuri kama timu, lakini bado washambuliaji wanatakiwa kuongeza kasi na ubunifu, hasa katika kumalizia mipira nyavuni kama alivyokuwa akifanya yeye zama akicheza hapo Old Trafford.**

Akasema kwamba washambuliaji wanatakiwa kujinoa na kuwa na kiu ya kumalizia mabao na kwamba kama timu hawajakosa kujiamini licha ya mwanzo usiokuwa mzuri sana wa msimu kwao. Anataka washambuliaji wake, ambao ni chipukizi wasiokuwa na mchezaji mwandamizi kuwaongoza, wafanye kazi yao na ana imani watafanikiwa.

Baada ya kuwatoa Romelu Lukaku na Alexis Sanchez kwa Inter Milan ya Italia, Man United sasa wanaongozwa kwenye mashambulizi na Marcus Rashford, Anthony Martial na Mason Greenwood.

Walianza vema Ligi Kuu ya England (EPL) kwa kuwakung'uta Chelsea mabao manne, lakini mechi zilizofuata wakatoa sare mbili na kufungwa moja hadi wakienda kwenye mapumziko kupisha mechi za kimataifa.

Solskjær anakiri kwamba kikosi chake ni chepesi kwenye ushambuliaji, lakini baada ya muda si mrefu vijana watakuwa wameiva kwa majukumu yao. Martial hakusafiri kwa ajili ya mechi ya wikiendi iliyopita walikoambulia sare dhidi ya Southampton kutokana na majeraha, lakini Greenwood (17) alicheza vyema akitoka benchi, huku Daniel James (21) akiwa ndiye mfungaji wao.


"Tunatengeneza nafasi, tunatengenezea wapinzani wetu shinikizo, sasa ni juu ya yale mabao ya kushtukiza. Tunao wachezaji wadogo na wanatakiwa kujifunza namna ya kufunga mabao yale ya kuudhi kama nilivyokuwa nafanya," akasema kocha huyo.

Anaongeza kwamba ana uhakika Rashford na Martial wataendana na shinikizo lilelo juu yao kwa ajili ya kuipatia klabu mabao kutokana na kutokuwapo wale washambuliaji waandamizi. Anasema wana miaka mingi kwenye klabu hiyo tangu wakiwa wachanga na hivyo anawatarajia kuwa nyota.

Solskjær anasema wachezaji wanaona na wanajua kipi kinahitajika kutokana na hali waliyokuwa nayo uwanjani kwenye mechi tatu zilizopita. Kwamba wamekuwa wakitawala mechi hizo, lakini sasa cha muhimu ni kuwa wanapata ushindi na wajue jinsi ya kufanya hivyo.

Beki wa kati Mwingereza aliyesajiliwa msimu huu Old Trafford, Harry Maguire, alikubaliana na kocha wake, akisema wanatakiwa sasa kuonyesha ukali kwenye ushambuliaji kwa sababu tayari kwenye ulinzi wapo vizuri, isipokuwa mbele kuki-haribika wapinzani wao wanatumia fursa hiyo kuwaadhibu.

**NDANI YA 18**



TANGU alipoanza kucheza Ligi Kuu England ('Premier League') kwa mara ya kwanza Aogsti 2010, kiungo wa Manchester City, David Silva, ametoa pasi za mwisho 87 ambazo ni 27 zaidi ya mchezaji yeyote katika ligi hiyo.

Nipashe Spotika



HUKU msimu mpya wa 2019/2020 ukiendelea, kuna klabu ambazo zimefanya usajili wa maana wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha majira ya joto, huku nyingine zikilamba garasha.

Uk. 16&17




# NYOTA 7 WANAOVAA, KUITENDEA HAKI JEZI NA. 7

**LONDON,** England

KABLA ya msimu wa 2019/20 haujachanganya, hapa tunawaangalia wacheza saba bora wanaovaa jezi namba saba ambao wapo kwenye kiwango bora zaidi. Jezi namba saba imekuwa ikiwaibua nyota wakubwa zaidi wa soka duniani, kuanzia kina David Beckham hadi Cristiano Ronaldo.

**Makala haya yanakuchambulia wachezaji saba bora kwa sasa ambao wanavaa jezi namba saba, shuka nayo...**

**7. JOSE CALLEJON**

Mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid amekuwa na kiwango cha kuvutia pale Napoli na alianza chini ya kocha, Maurizio Sarri na sasa akiwa na kocha mpya, Carlo Ancelotti.

Amekuwa nguzo muhimu tangu ajiunge na Gli Azzurri hao mwaka 2013 na amefunga mabao 79 na kutoa pasi za mwisho 69.

**6. JADON SANCHO**

Akiwa anacheza katika klabu ya Borussia Dortmund, kinda huyo amekuwa na kiwango cha kuvutia kwani amefunga mabao 15 kwenye Ligi Kuu ya Ujerumani na kuweka rekodi ya mchezaji kijana zaidi kwenye ligi hiyo kufunga idadi hiyo ya mabao, rekodi ambayo ilidumu kwa kipindi cha miaka 52.

**5. N'GOLO KANTE**

Licha ya kuwa anacheza kiungo mkabaji, lakini Kante amekuwa akiitendea haki jezi namba saba. Tangu alipojiunga Chelsea, amekuwa na wakati wa kuvutia zaidi kwa kiwango chake kuendelea kuimarika.

**4. SON HEUNG-MIN**

Tottenham Hotspur mara zote imekuwa haina historia ya kupata mawinga bora. Na wakati Gareth Bale anaondoka hakuna aliyejua kama Spurs itapata winga bora, Son Heung-min raia wa Korea Kusini.

Amekuwa akitendea haki jezi namba saba, huku akifunga mabao 20 na kutoa pasi za mwisho 10 katika mashindano yote msimu uliopita akichezea Spurs.

**3. RAHEEM STERLING**

Manchester City ina moja ya safu bora zaidi ya ushambuliaji kwenye Ligi Kuu ya England na Ulaya. Na mmoja wa wachezaji ambaye anayeunda safu hiyo ya kikosi hicho cha kocha Pep Guardiola ni Sterling.

Nyota huyo alifunga mabao 17 na kutoa pasi za mwisho 10 kwa msimu wa 2018/19 akicheza mechi 34.

**2. KYLIAN MBAPPE**

Akiwa na umri wa miaka 20 nyota huyu wa klabu ya Paris Saint-Germain tayari ana mafanikio makubwa kwenye mchezo wa soka. Katika umri wake wachezaji wengi wanakuwa na ndoto ya kushinda mataji makubwa mbeleni.

Lakini tayari Mbappe ana taji la Kombe la Dunia alilolitwaa akiwa na kikosi cha Ufaransa mwaka jana. Msimu uliopita alifunga mabao 33 na alizidiwa na Lionel Messi katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora Ulaya. Messi alikuwa na mabao 36 akimzidi Mbappe kwa matatu tu.

**1. CRISTIANO RONALDO**

Huyu ndiye unaweza kusema mchezaji bora zaidi kuvaa jezi namba saba duniani. Kwa sasa akiwa na umri wa miaka 34, lakini kiwango chake bado kinaonekana kuwa bora zaidi na hata muda wa kucheza unaonekana kuwa bado kwake.

Akiwa ameanza kucheza soka kule Benfica nchini Ureno, akatua Manchester United akicheza kwa mafanikio makubwa, kabla ya kutimkia Real Madrid ambako nako ameacha alama kubwa kwenye Ligi Kuu ya Hispania.

Akiwa Real Madrid, Ronaldo aliweka rekodi ya kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo kabla ya kuamua kutimkia katika klabu ya Juventus ya nchini Italia ambako anacheza hadi sasa,

Katika mahojiano yake ya hivi karibuni, Ronaldo alisema anataka kucheza hadi afikishe umri wa miaka 40, kwani anaamini ana uwezo huo.

**USILOLIJUA**

Frank Lampard ndiye anayeshikilia rekodi ya kufunga penalti nyingi timu ya Taifa ya England (penalti tisa) akifuatiwa na Harry Kane aliyezamisha kimyani mikwaju nane (mbali na alizokosa).



## Wadhalilishaji wanawake, watoto kukiona cha moto

**Na Grace Mwakalinga, CHUNYA**

SERIKALI wilayani Chunya Mkoa wa Mbeya imewaonya watu watakaobainika kutekeleza vitendo vya mauaji, ubakaji, ulawiti dhidi ya wanawake na watoto ambavyo vinahusishwa na imani za kishirikina, kuchukuliwa hatua kali.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Marryprisca Mahundi, aliyasema hayo juzi wakati wa kikao na waandishi wa habari wanawake wa Mkoa wa Mbeya waliofika ofisini kwake kupongeza jitihada zake za kupambana na vitendo hivyo ambavyo kabla ya uongozi wake vilishamiri.

Alisema vitendo hivyo vya mauaji, ulawiti na ubakaji kwa wanawake na watoto vinahusishwa na imani za kishirikina kutoka kwa wachimbaji wa dhahabu ambao huamini kufanya hivyo kutawaletea utajiri na kupata madini mengi ya dhahabu.

Alisema serikali imejipanga vyema kukabiliana na vitendo hivyo kwa kushirikiana Jeshi la Polisi, madiwani na wananchi na mpaka sasa vitendo hivyo vimeanza kupungua kwa sababu ya kuripotiwa na wahusika kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Katika kipindi cha mwaka 2018 matukio ya ubakaji, mauaji na ulawiti yaliripotiwa saba na kwa mwaka huu hadi kufikia mwezi Julai yalikuwa mawili, tunaamini ni hatua kubwa katika kukabiliana navyo, tunaendelea kupambana ili kuhakikisha vinatokomea kabisa," alisema Marryprisca.

Alieleza kuwa mikakati waliyoipanga ili kutomeza vitendo hivyo ni kufanya mikutano ya hadhara na kutoa elimu kwenye kata zote 20 za wilaya hiyo kuhusu athari za vitendo hivyo na kuachana na imani za kishirikina.

Alilipongeza Jeshi la Polisi wilayani Chunya kwa utendaji kazi wake katika kupambana na vitendo hivyo kwa kuwa wanafuatilia na kuwakamata watuhumiwa wote wanaoripotiwa kuhusika na vitendo hivyo.

Katika ziara yake mwishoni mwa mwezi Aprili mwaka huu, Rais John Magufuli akiwa wilayani Chunya aliagiza uongozi wa wilaya kuhakikisha wanatoa elimu kwa wananchi dhidi ya mauaji ya watoto na wanawake pamoja na kuwakamata wahusika wa matukio hayo.

**"Katika kipindi cha mwaka 2018 matukio ya ubakaji, mauaji na ulawiti yaliripotiwa saba na kwa mwaka huu hadi kufikia mwezi Julai yalikuwa mawili, tunaamini ni hatua kubwa katika kukabiliana navyo, tunaendelea kupambana ili kuhakikisha vinatokomea kabisa," alisema Marryprisca.**

# Afagilia kilimo cha maparachichi kwa ukombozi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MKULIMA wa maparachichi wa Kijiji cha Njelenje, Kata ya Mshewe Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Boniface Mwandandila (62), amewashauri wananchi kujikita kwenye uzalishaji wa zao hilo ili kupata kipato cha uhakika.

Mwandandila alitoa ushauri huo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na Nipashe shambani kwake juu ya namna kilimo cha parachichi kilivyomnufaisha pamoja na changamoto zinazomkabili.

Alisema zao hilo limekuwa msaada kwa familia yake kwa sababu ana uwezo wa kupata mahitaji muhimu na anasomesha mtoto wake chuo kikuu bila mkopo.

Aliwahamasisha wakulima kulima zao hilo kwa kuwa lina faida kubwa na lina soko la uhakika la ndani na nje ya nchi kutokana na kuwa na matumizi mengi ikiwamo chakula. Aliliambia Nipashe kuwa kabla ya kuanza kilimo hicho alipata elimu kutoka kwa wataalamu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (Tari), Kituo cha Uyole cha jijini Mbeya ambao walimshauri kutumia miche inayoendana na hali ya hewa na eneo analolima.

Alisema baada ya kupata elimu hiyo, mwaka 2016 alianza kupanda miche 600 ambayo alianza kwa kulipa kidogo kidogo kutokana na hali ya kiuchumi.

"Nafurahia maisha yangu ya kustaafu katika kilimo hiki cha parachichi kwa sababu nina uhakika wa maisha nanunua soda, nyama ninavyotaka, lakini pia namsomesha mtoto wangu chuo kikuu ambaye hana mkopo bila shida, nawahamasisha wengine kulima zao hili," alisema Mwandandila.

Aliongeza kuwa kwa sasa mti mmoja wa parachichi unatoa magunia matatu na kwamba ana uhakika na soko kwa sababu ya ubora wa maparachichi yenyewe, watu kutoka maeneo mbalimbali ikiwamo Wilaya ya Songwe na Chunya, hufika shambani kwake kununua.

Alisema kwa sasa amelima hekta saba na nusu na matarajio yake ni kulima hekta 20 akipata mtaji wa kutosha.

Mtafiti wa matunda kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Uyole, Daud Mbongo, ambaye alimtembelea mkulima huyo, alisema walipanda miche aina saba za miparachichi shambani kwa mkulima huyo kama eneo la majaribio kwa sababu alionyesha jitihada na uhitaji katika kilimo hicho.

Mbongo alisema aina za miche walizozipanda shambani ni Hass, Fuerte, Weisal, Ikulu, Simmonds, Booth 7 na Uyole, ambayo ni aina mpya iliyo kwenye majaribio.

Alisema miche hiyo inayafanya vizuri sana kwa sababu inastawi na kutoa matunda mengi katika shamba hilo na kwamba mara kwa mara humtembelea mkulima huyo kumpa elimu ya namna ya kutunza zao hilo la parachichi.

Alisema tangu watoe miche hiyo ni miaka mitatu sasa na tayari mkulima huyo ameanza kufaidi matunda ya maparachichi na kwamba kila msimu hukusanya matunda na kuyauza.

"Kilimo cha parachichi kinafanya vizuri sana kipindi hiki na kuwaingizia faida kubwa wakulima wetu katika kuhakikisha tunaendelea kuwasaidia tunaendelea kubuni miche mipya ambayo ni rafiki kwa mazingira ya joto na baridi na kutoa elimu ya kilimo chenye tija na hii imesaidia wengi kufika ofisini kununua miche hiyo," alisema Mbongo.

Aliwashauri wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kutumia Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Tari - Uyole, ili kupata ushauri wa kitaalamu katika kuongeza tija kwenye mazao yao na kwamba wataendelea kushirikiana na maofisa ugani ili waweze kuwatambua wakulima na kuwatembelea.



Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, John Palingo (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na wahitimu wa mafunzo ya jeshi. **PICHA: RAHIM YUNUS**

# Teknolojia kilimo hifadhi yasambazwa kwa wakulima

**Na Ashton Balaigwa, MBEYA**

KUTOKANA na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira nchini, watafiti kutoka Tari- Uyole, iliyopo mkoani Mbeya wameamua kueneza kwa wakulima teknolojia kilimo hifadhi ili kuwasaidia walioathiriwa na kuongeza uzalishaji wa chakula katika maeneo hayo.

Akizungumza katika mahojiano maalumu na gazeti hili, Mratibu wa Utafiti na Ubunifu wa Tari-Uyole, Dk. Ndabhemeye Mlengera, alieleza kuwa wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwamo, Rukwa, Iringa, Mbeya na Katavi tayari wameshaanza kuona mafanikio yake.

Dk. Ndabhemeye, alisema kilimo hicho kinachozingatia uhifadhi wa rasilimali udongo na mazingira kwa kuwa kanuni zake ni kusumbua udongo kwa kiasi kidogo na kufunika ardhi wakati wote kwa kuacha masalia shambani au kupanda mazao funika.

Alisema kuwa pia kilimo hicho kinafuata kanuni kwa kulima kilimo cha mzunguko cha mazao ya nafaka na mikunde ambayo yamekuwa yakiongeza mbolea na uhifadhi wa udongo katika shamba.

Alisema, Tari - Uyole, imeamua kuhimiza kwa wakulima hao kilimo hifadhi kwa sababu kinaongeza uzalishaji kwenye maeneo yenye ukame, pia kina wahakikishia wakulima usalama wa chakula pamoja na kupunguza gharama za uzalishaji na hivyo kuongeza kipato kwa mkulima.

Mafanikio mengine kupitia kilimo hicho ni kusaidia kupunguza muda wa kufanya kazi shambani, hivyo mkulima anapata muda wa kufanya shughuli nyingine za maendeleo pamoja na kudhibiti mmomonyoko wa udongo na kumudu mabadiliko ya tabia nchi.

Hata hivyo, Dk. Ndabhemeye alisema moja ya changamoto ya kilimo hifadhi ni pamoja na uhaba wa wataalamu wa kilimo wenye elimu ya kilimo hifadhi, huku akieleza eneo linalolimwa kilimo hicho ni dogo mpaka mwaka 2012 ni ekari 62,500 pekee ndizo zilitumia teknolojia hiyo.

Alishauri wadau mbalimbali kuwekeza kwenye matumizi ya zana bora za kilimo ili kuongeza tija ikiwa ni pamoja na kupewa kipaumbele kwa ustawi wa jamii na uhifadhi wa mazingira.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Tari-Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema mpaka sasa wana teknolojia 46 ambazo wanazipeleka kwa wakulima lengo likiwa ni kuongeza kipato, mazao mengi na kukuza ajira katika kilimo.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Tari, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema ili kufikia uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo mwaka 2025, Tanzania inapaswa kutumia teknolojia mbalimbali zinazotoa majibu chanya kwa ajili ya kutatua changamoto zilizopo katika jamii.

Alisema TARI imejipanga kuhakikisha teknolojia zinazozalishwa zinasambazwa na kuwafikia wakulima na wadau wengine wa kilimo ili kuweza kuongeza uzalishaji wa malighafi zinazotokana na kilimo zinazohitajika katika uchumi wa viwanda.





# DC Shekimweri awaasa wahitimu jeshini

**Na Ibrahim Joseph, MPWAPWA**

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, amewataka vijana wanaohitimu mafunzo ya kijeshi kujiepusha na vitendo vya kihalifu watakaporudi katika jamii.

Kauli hiyo aliitoa mwishoni mwa wiki wakati alipozungumza kwenye kufunga mafunzo ya kijeshi kwa miezi mitatu kwa wanafunzi waliomaliza kidato cha sita kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kikosi cha 826 Mpwapwa, wilayani humo.

Aliwataka vijana hao kujenga nidhamu na kujiepusha kujiingiza kwenye vitendo vya kihalifu kwa tamaa ya kutaka mali watakaporudi katika jamii.

"Vijana wangu mmekuwapo hapa kwa muda wa miezi mitatu kujifunza mambo mbalimbali, nawaomba mtakapotoka hapa kuendeleza nidhamu hii nzuri na kujiepusha na vitendo vya kihalifu mnaporudi kwenye maeneo yenu," alisema.

Aliwataka wawe walinzi wa amani kwa wale watakaochaguliwa kujiunga na vyuo pamoja na wengine watakaorudi katika jamii.

"Nendeni mkayafanyie kazi mafunzo mliyofundishwa wakati mkiwa kambini ili muweze kujiajiri na kujiongezea kipato," alisema.

Alishauri taasisi za serikali kutumia fursa ya uwapo wa kambi hiyo katika wilaya hiyo kusaidia ujenzi wa miradi ya jamii kutokana na kujenga kwa gharama nafuu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kikosi hicho, Luteni Kanali Mohamed Karuma, alisema mafunzo hayo yalianza Juni 17, mwaka huu yakiwa na wanafunzi 600.

Karuma alisema kati hao wavulana walikuwa 462 na wasichana 138, huku 12 wakishindwa kumaliza kutokana na maradhi pamoja na utoro.

Alisema wakiwa kambini wanafunzi hao walijengewa ujasiri na ukakamavu, ari ya kupenda kazi na mbinu za awali za kivita.

Aliongeza kuwa vijana hao walifundishwa masomo ya ujasiriamali, ufundi wa aina mbalimbali, ulinzi na usalama wa taifa pamoja na kujengewa uwezo wa kupenda nchi yao.

Alisema vijana hao wameonyesha utii wa hali ya juu walipokuwa kambini hapo na wanategemea kuwa watakapotoka hapo wataisaidia jamii na familia wanapotoka.



Baadhi ya wanafunzi waliomaliza kidato cha sita mwaka huu, wakipita kwa mwendo wa haraka wakati wa kufunga mafunzo yao ya kijeshi Kambi ya 826 Mpwapwa JKT mkoani Dodoma jana, wanafunzi hao walihitimu mafunzo ya miezi mitatu kwa mujibu wa sheria.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watumishi watakiwa kubadilika kiutendaji

**Na Mwandishi wetu, MPWAPWA**

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, anayeshughulikia afya, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka watumishi wa Kituo cha Afya Kibakwe, kuondokana na utendaji kazi wa mazoea kutokana na kuteuliwa kuwa kituo cha mfano.

Kituo hicho kimeteuliwa kuwa cha mfano wa utekelezaji wa mabadiliko katika utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana katika ziara yake ya kutembelea vituo vya kutolea huduma Halmashauri ya Mpwapwa kujionea maendeleo ya utoaji wa huduma za afya kwa jamii, pamoja matayarisho ya vituo hivyo katika kutoa huduma za afya kinga.

Alisema mwelekeo wa OR -Tamisemi ni kuwa na vituo bora vya afya ambavyo watumishi wake wanawajibika kwa mwelekeo mpya unaopimika kwa kadri ya rasilimali walizonazo ili utoaji wa huduma uwe bora na kuvutia wananchi kujiunga na bima ya afya.

"Kama vile CHF iliyoboreshwa ili kuimarisha uchumi wa sekta ya afya na kupunguza utegemezi kwa serikali kuu," alisema.

Dk. Gwajima alieleza kuwa dhamira ya serikali ni kuwa na watumishi wenye kufanya kazi kwa ubunifu na kuvithamini vituo hivyo kama wanavyothamini mali zao, kwa kuweka mikakati ya uwajibikaji na kupimika kuanzia mtumishi mmoja mmoja hadi timu nzima kama ilivyowezekana kwenye Kituo cha Afya Makole jijini Dodoma.

"Tunataka vituo vyote vya kutolea huduma nchini viwe na nguvu ya kiuchumi siyo kwa kutegemea watu waugue bali wananchi wenye afya bora wanaothamini kuchangia bima ya afya, ili pale wanapohitaji huduma wazipate zilizo bora, kwa gharama nafuu tena karibu na makazi yao," alisema.

Awali Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Dk. Archard Rwezahura, alisema kituo cha Kibakwe kimeteuliwa kuwa kituo darasa kama ilivyofanyika kwenye Kituo cha Afya cha Makole, jijini Dodoma kutokana na fursa kubwa zilizopo sasa katika kituo hicho zinazotokana na maboresho makubwa ya miundombinu yaliyofanywa.

Alisema kuwa kituo hicho kimefanyiwa marekebisho makubwa ya miundombinu ikiwamo majengo ya upasuaji, wodi ya mama na mtoto, maabara, na chumba cha kuhifadhia maiti, hivyo fursa kubwa ya kuvutia wateja kwa kuinua uwajibikaji wa watumishi ili maboresho hayo ya wanufaishe wateja na serikali kwa ujumla.

Alitaja baadhi ya vigezo vilivyotumia katika kuteua kituo hicho ni pamoja na uwapo wa miundombinu bora, watumishi wenye sifa, kituo kuwa karibu na kufikika kwa urahisi, dawa na vifaa tiba vinavyohitajika na uwezekano wa kufanya ufuatiliaji wezeshi kwa urahisi.

Naye Mganga Mkuu wa Kituo hicho, Dk. Pius Mramba, aliahidi kufanyia kazi maagizo yote yaliyotolewa na watahakikisha wanafanya kazi kwa kasi inayotakiwa ili kuingia kwenye ushindani wa ubora wa huduma na kupimwa.

## Waislamu wahimizwa kuchangia maendeleo

**Na Peter Mkwavila, DODOMA**

WAUMINI wa dini ya Kiislamu wametakiwa kuchangia shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo ya kielimu badala ya kuitegemea serikali kila kitu.

Wito huo ulitolewa na Katibu wa Baraza la Waislamu Tanzania (Bakwata) Chang'ombe jijini hapa, Hussein Bashuru, katika maadhimisho ya elimu yaliyoambatana na uchangiaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Madrasa ya Shamsiya Nguzo Mbili Ngamiani.

Alisema serikali imekuwa ikifanya juhudi kubwa katika kuchangia huduma mbalimbali hivyo hata kwa upande wa waumini wa dini ya Kiislamu wanatakiwa kuunga mkono harakati hizo za kimaendeleo.

"Changamoto kubwa iliyopo kwa waumini wa dini ya Kiislamu hawashiriki katika shughuli za kimaendeleo badala yake wamekuwa wakinun'gunika na kubeza shughuli za kimaendeleo zinazofanywa na serikali," alisema.

Kwa upande wake, Shehe Mohamed Mwakaluwa kutoka Tanga, aliwataka vijana kuweka jitihada kwenye masomo ili waweze kuwa viongozi watakaokuwa na hofu na rasilimali za watu na Mungu.

Alisema tatizo lililopo kwa vijana wengi wapo kwenye malalamiko ambayo yanayowafanya kukosa huduma mbalimbali, huku wakijua hawana elimu ya kutosha kwa uzembe wao.

Naye Mwalimu wa Madrasa ya Najah Islamin Centre Chang'ombe, Dodoma, Idd Shabani aliwataka wazazi kutokuwa chanzo cha mmomonyoko wa maadili kwa watoto wao kwa kuwakosesha haki ya kimsingi ya elimu ya dunia na kiroho.

Alisema kuwa watoto wengi wamekuwa wakikosa maadili ya kiroho na dunia kutokana na wazazi kutowapatia haki ya kupata elimu.



## HABARI ZANZIBAR

# Rais Shein awataka waandishi kutafuta fursa kimataifa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka waandishi wa habari kuchangamkia fursa za kufanyakazi katika vyombo mbalimbali vya kimataifa ikiwamo redio na magazeti, hatua aliyosema itafanikiwa kwa kujiimarisha na kuwa na weledi katika kuandika na kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha.

"Nakuhimizeni mchangamkie fursa mbalimbali za ajira, katika wakati huu vyombo vya habari vinavyotumia lugha ya Kiswahili vimekuwa vikiongezeka na lugha hiyo kuzidi kukua," alisema Dk. Shein wakati akifunga Mkutano Mkuu wa Muungano wa Klabu za Waandishi wa Habari (UTPC), uliofanyika mjini hapa.

Alisema vyombo vya habari vina jukumu la kuendelea kuikuza na kuieneza lugha ya Kiswahili ulimwenguni kwa kutumia lugha fasaha.

Alisema mkutano wa wakuu wa nchi za SADC uliofanyika hivi karibuni umeridhia Kiswahili kuwa lugha ya jumuiya hiyo, hivyo ni jukumu la waandishi wa habari kusisitiza utumiaji wa Kiswahili fasaha na kuepuka matumizi ya maneno yasio rasmi.

Hata hivyo, alisema kunahitajika matumizi sahihi na mazuri ya lugha katika uandishi, ili taarifa ziweze kukubalika bila kuleta hitilafu.

"Nataka msisitize juu ya kutumia lugha kwa ufasaha katika kusema na kuzungumza, namna ya kuchagua maneno mazuri katika maandishi," alisema.

Aliwataka waandishi wa habari nchini kuondokana na utamaduni wa kufanya kazi kwa mazoea, kwa kuwa sio sifa ya uandishi na utoaji mzuri wa habari.

Alieleza kuna umuhimu kwa waandishi kubadilika kwa kuzingatia kuwa taaluma ya habari inahitaji mawazo mapya, ubunifu na ushindani wenye tija.

Alisema ili mawazo mapya yaweze kupatikana, kunahitajika ufuatiliaji na utafutaji wa habari kutoka katika vianzio vinavyoaminika pamoja na kufanyiwa utafiti.

"Habari bora sio tu ile ambayo inavutia wateja kuisoma, bali ni lazima iwe ya kweli na inayoandikwa kwa lugha sahihi inayokubalika," alisema. Dk. Shein aliwataka waandishi wa habari hususan wa magazeti kuwa makini na kutoelemea zaidi katika biashara na badala yake kuangalia sifa na ubora wa habari zinazohitaji kuchapishwa.

Alisema wananchi wanapaswa kuelewa changamoto zinazoikabili serikali katika utekelezaji wake wa kazi, hususan pale malengo yasipofikiwa na kuvikumbusha vyombo hivyo kutoa habari kwa jamii.

Alisema katika uandishi kalamu inaweza kuwa nyenzo nzuri yenye kuinua hadhi ya mwandishi na kuleta tija iwapo atatumia kwa uangalifu, lakini pia inaweza kumuweka mwandishi katika nafasi asiyoridhia, pale asipoitumia vyema.

Aliwataka waandishi wa habari kufanya kazi zao kwa weledi na kuzingatia maadili yanayokubalika katika taaluma hiyo, bila ya kukiuka mila, silka na utamaduni kwa kuzingatia matumizi bora ya kalamu zao na ulimi.

Katika hatua nyingine, Dk. Shein, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikichukua kila juhudi kuimarisha sekta ya habari kwa kuviimarisha vyombo vya habari vya serikali kwa kuvipatia vifaa vya kisasa pamoja na mafunzo kwa watendaji wake.

Naye Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahamoud Thabit Kombo, alisema uamuzi wa UTPC kufanya mkutano wake mkuu Zanzibar ni uthibitisho kwa kiasi gani jumuiya hiyo inavyolenga kuimarisha Muungano.

Alisema UTPC imefanya kazi kubwa ya kuunganisha klabu za habari katika mikoa yote, hivyo akaiomba jumuiya hiyo kuangalia uwezekano wa kufanya Pemba mkutano mkuu ujao, pamoja na gharama kubwa za uandaaji.

Naye Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Anders Sjoberg, aliipongeza UTPC kwa kuwa kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi nchini.



Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, George Joseph Kazi, akizungumza katika mkutano uliowakutanisha viongozi na watendaji wa sekta ya sheria, uliojadili taarifa ya utafiti ya uwezekano wa kuanzisha jukwaa la pamoja kwa wahusika wa sheria Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Jukwaa sekta ya sheria kuunganisha wadau

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIBU Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, George Joseph Kazi, amesema kuundwa kwa jukwaa la wadau wa sekta ya sheria kutasaidia kuwaunganisha na kuleta maendeleo endelevu kwa maslahi ya taifa

Aliyasema hayo kwenye mkutano uliowakutanisha viongozi na watendaji kutoka sekta ya sheria, uliojadili taarifa ya utafiti wa uwezekano wa kuanzisha jukwaa la pamoja kwa wahusika wa sheria Zanzibar.

Aliwataka wajumbe hao kutoa michango na mawazo yao na kufanya upembuzi ili kuona mahitaji muhimu yatakayosaidia kufahamu sekta ya sheria kwa kutambua kuwa sheria ndio kiini katika masuala yote ya maendeleo ya nchi.

Alisema Zanzibar kumekuwa na ongezeko kubwa la wanasheria, lakini kilichokosekana ni kutokuwa na jukwaa la pamoja linalowaunganisha wanasheria hao.

Alisema uwapo wa jukwaa hilo utasimamia na kuangalia maendeleo ya sekta ya sheria hali ilivyo na jinsi gani itakuwa na uratibu ambao utasaidia kujua mambo mengi na matatizo yanayoikumba sekta ya sheria kwa ajili ya maendeleo chanya ya sekta ya hiyo.

Vile vile, alisema sekta ya sheria inaendelea kukua kwa kasi, hivyo wizara imeona ipo haja ya kuwa na chombo kitakachosaidia kuzidisha kasi ya uwajibikaji ili kila mmoja atimize wajibu wake.

"Muhimu kujielewa kama wanasheria kufahamu jukumu walilonalo na kazi wanazofanya ikiwamo kufanya tathmini ya kile wanachokifanya badala ya kufanya kazi kwa mazoea, hii itasaidia kuleta chachu katika sekta ya sheria kujenga utamaduni wa kujisomea na kufahamu mambo mapya yanayotokea, hivyo jukwaa hili litatusaidia tuweze kujitambua," alisema.

Alisema kupitia jukwaa upo uwezekano wa kufanya utafiti na kufahamu kiwango cha ongezeko la wanasheria, mawakili na mahakimu na kuona sekta ya sheria imekuwa kwa kiwango gani na kama wamebobea kuwa wataalamu wanaofikia kiwango na vigezo vinavyohitajika katika kada ya sheria.

Washiriki wa mkutano huo kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Mohammed Khamis na Mussa Kombo, walisema lengo la kuwa na chombo hicho ni kusaidiana mawazo na ushauri ili kuona uwajibikaji unaimarika na sio kuingilia majukumu ya vyombo vya kisheria, pia kuondoa migongano ya kisheria baina ya taasisi na kutekelezwa kwa vitendo mawazo na ushauri utakaotolewa.

Naye Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Ibrahim Mzee Ibrahim, aliainisha mambo manne ambayo yakitekelezwa ipasavyo yatakuwa chachu ya maendeleo ikiwamo vyombo vya mashtaka kufahamu majukumu yao ya kiutendaji, pia kufuatwa kwa maadili na taratibu zake, usimamizi pamoja na suala la uwajibikaji na ushirikiano baina ya vyombo vya sheria vilivyopo nchini.

Alisema kinachounganisha taasisi hizo zote za sheria ni mwongozo wa taasisi na kila chombo kinamamlaka yake na imewekewa sheria hivyo kuwapo kwa jukwaa hilo kutasaidia kuondoa baadhi ya misuguano na kuwa na sauti ya pamoja katika utekelezaji wa masuala ya utoaji haki.

## Waziri awaasa wahitimu kidato cha sita

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka wanafunzi waliomaliza kidato cha sita kushughulikia zaidi masomo yao watakapofika vyuo vikuu ili kupata mafanikio mazuri baadaye.

Akizungumza katika mahafali ya tano ya kidato cha sita katika Shule ya Sekondari ya Al-ihsani Girls, Mwanakwerekwe Mjini Unguja, alisema katika vyuo wanaweza kukutana na vishawishi mbalimbali ambavyo vinaweza kuwapotezea mwelekeo wa masomo yao.

Alisema ni vyema kujitambua na kutajitathmini kwa kufuata masomo na kuachana na masuala ya mapenzi ambayo yatawaharibia mustakbali mwema wa maisha yao kutokana na umri walionao.

Alisema kuna baadhi ya walimu wa shule na hata wa vyuo vikuu wamekuwa wakiwataka kimapenzi wanafunzi na kuwatishia kuwafelisha kimasomo, hivyo ni vyema kuwa makini na walimu hao.

"Itakapotokea mwalimu yeyote atakewataka kimapenzi msikae kimya mripotini katika sehemu husika ili kukomesha vitendo vya udhalilishaji kwa wanafunzi," alisema.

Aliwataka wanafunzi kuendeleza maadili mema waliyojifunza shuleni kwa kujiheshimu hasa katika suala la mavazi yanayoendana na mila na utamaduni wa nchi, kwa kuwa hali hiyo itawasaidia kuwa raia wema.

Pia aliwataka wazazi na walezi kushirikiana na walimu katika suala la elimu kwa kuwa maendeleo ya elimu yatafikiwa endapo kutakuwapo ushirikiano kati ya wazazi na walimu pamoja na wanafunzi.

Akisoma risala ya wahitimu wa shule hiyo, mwanafunzi Fatma Said Suleiman, alisema ni faraja kwao kuweka historia kwa shule yao kwa kuwa ni mara ya kwanza kuwa na ufaulu wa daraja la kwanza hali ambayo haijawahi kutokea. Waliushukuru uongozi wa shule yao pamoja na Shirika la Misaada ya moja kwa moja Direct AID, kwa juhudi wanazochukua kuhakikisha changamoto zilizokuwa zikiwakabili kuzifanya kuwa fursa na hatimaye kufaulisha wanafunzi wote katika madaraja mbalimbali.

# Wanawake walengwa Tasaf wafunguka ndoa

**Na Elizabeth Zaya, SINGIDA**

WANAWAKE walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), wamesema ndoa zao zimeimarika baada ya kuwezeshwa na mfuko huo, kuanzisha biashara ndogondogo za kujiongezea kipato

Wakizungumza na baadhi ya maofisa wa Tasaf na waandishi wa habari waliotembelea miradi inayotekelezwa na walengwa hao, kwenye vijiji vya Wilaya ya Singida Vijijini, walisema fedha kidogo wanazopata kwenye mpango huo wanazitumia kuanzisha miradi midogo.

Farida Rajab wa Kijiji cha Kibaoni Kata ya Mudida wilaya hiyo, alisema hivi sasa heshima imerudi kwenye familia yake baada ya kumudu kufanya biashara ya mboga, kuku, mbuzi na kujenga nyumba ya bati kupitia malipo ya kazi za muda kwenye miradi ya Tasaf na ruzuku anayopokea kila baada ya miezi miwili.

"Ukiwa maskini watu wanakudharau, mume wangu alikuwa ananiona mzingo maana kula yetu ilikuwa ya kuvizia, watoto hata shule walikuwa hawaendi kwa kukosa sare na daftari," alisema.

"Nimeingia Tasaf nikapewa Sh. 20,000 nikafundishwa namna ya kutunza akiba hadi ya Sh. 1000 na namna ya kutumia kuanzisha biashara ndogo, nilijinyima nikaweka mpaka nikanunua kuku watatu na iliyobaki nikaenda kulangua nyanya na mboga za majani," alisema Farida.

Kwa mujibu wa mlengwa huyo, tangu 2014 alivyoingia Tasaf hadi sasa watoto wake wanne wanaenda shule vizuri, familia yake ina uhakika wa milo mitatu, amejenga nyumba ya bati na biashara zake zinaendelea huku akisisitiza kwamba amejiunga kwenye kikundi cha kuweka na kukopa.

Akieleza namna alivyookoa ndoa yake, mlengwa mwingine, Hajra Jumanne alisema ufukara aliokuwa nao ulimfanya akatengwa na ndugu huku mume akimtelekeza na watoto wanne.

"Sikufikiria kulala kwenye kitanda, chakula kilikuwa cha kubabaisha watoto hawaeleweki lakini ulipokuja mpango wa Tasaf, huwezi kuamini maisha yamebadilika kabisa, najiona mtu katika watu.

"Wanangu wanakwenda shule ni wasafi kama wengine, tunao uhakika wa milo mitatu na biashara yangu ya pombe inaendelea kwa mtaji wa Sh. 30,000 nilizopewa kwenye mpango huu. Nimewekeza mabati dukani yamefika 16 nataka yafike 30 nimeanza kujenga nyumba ya tofali za kuchoma.

"Sasa hivi mume wangu ananiambia nakupenda mke wangu, wakati kipindi cha nyuma alikuwa ananinyanyasa wakati tukiwa na maisha magumu, sasa tunasaidiana kulea watoto familia ina furaha," alisema Jumanne.

Mratibu wa Tasaf Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini, Piyazis Tindikali, alisema kila mlengwa wa mradi huo anapewa elimu sahihi ya ujasiriamali mdogo ili kujiongezea kipato na kuondoka chini ya mstari wa umaskini.



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), anayeshughulikia Afya, Dk. Dorothy Gwajima, akikagua kitabu cha kuingizia dawa katika Zahanati ya Ipala iliyopo katika kijiji cha Mwinyi, Halmashauri ya Jiji la Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Shule 40 kunufaika vita dhidi mimba za wanafunzi

**Na Dege Masoli, KOROGWE**

SHULE zaidi ya 40 za wilayani Korogwe mkoani Tanga, zitanufaika na mradi wa kuhamasisha mapambano dhidi ya kupiga vita mimba kwa wanafunzi yanayoendeshwa na Shirika la kizalendo la New Rulal Children Foundation NRCF chini ya udhamini wa Japan kupitia JICA.

Akitoa taarifa fupi kwa wajumbe wa umoja wa wanafunzi wazalendo waliyosoma Japan (JATA) walipotembelea miradi inayofadhiliwa na Jica wilayani humo, Mkurugenzi wa NRCF, Nicholaus Shemsanga, alieleza kuwa jumla ya shule 43 zimepata mafunzo hayo.

Shemsanga alisema elimu hiyo imeleta mabadiliko kwa wanafunzi kujitambua na hivyo kujenga ujasiri wa kukabiliana na watu wenye nia mbaya na ndoto za maisha yao, hivyo kupunguza kama siyo kuondoa kabisa tatizo hilo kwenye shule hizo.

"Pamoja na mafunzo hayo huduma nyingine tunazozitoa sambamba na elimu hiyo, kwenye shule hizo ni kuhamasisha usomaji na kuondoa kero ya nishati kwa kuweka huduma ya umeme wa jua katika shule za mradi," alieleza Shemsanga.

Alisema mradi huo uliyoanza Januari 2017 unaendeshwa sambamba na Shirika la C4E na uliibuliwa na utafiti uliyobaini changamoto mbalimbali katika shule za msingi na sekondari ikiwamo mimba, ukosefu wa umeme, miundombinu mibovu na wanafunzi kutopenda kusoma.

Aidha, alisema baada ya kuanza kwa mradi huo shule zilizofikiwa ni 43 kati ya 45 zilizokusudiwa na 13 kati ya hizo ni za sekondari.

"Kazi yetu ya kwanza ilikuwa ni kuhamasisha usomaji shuleni na ya pili kuweka solar katika shule mradi na tatu kuhamasisha vita dhidi ya mimba kwa wanafunzi...tumepata mafanikio makubwa kupitia mradi huu," alisema Shemsanga.

Alieleza kuwa jumla ya shule 22 kati ya 43 zimeshawekwa umeme wa solar wenye thamani ya Sh. mil. 47, huku huduma nyingine kama vile vitabu vya ziada na kiada.

Akielezea namna shule yake ilivyonufaika na mradi huo mbele ya wajumbe hao, Mkuu wa Sekondari ya Kwamndolwa, Jumaa Shazi, alisema tangu kuwe na umeme wa jua vitabu vya ziada na kiada wamepata mabadiliko makubwa kwa wanafunzi kupaona ni mahala salama.

Shule zilizotembelewa na ujumbe huo kati ya 22 ni Shule ya Msingi ya Antakae na Sekondari ya Kwamndolwa zilizopo Korogwe Vijijini na Korogwe Mji.

# DC amtega bosi Tarura

**Na Dege Masoli, HANDENI**

MKUU wa Wilaya ya Handeni, Gondwin Gondwe, amemuweka njia panda kigogo wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura), baada ya kumpa siku mbili kujieleza kwa kile alichodai kushindwa kumsimamia mkandarasi anayetengeneza barabara ya kuingia kambi ya Mgambo JKT hadi Kabuku.

Gondwe alitoa agizo hilo baada ya kupotea malalamiko kutoka kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya operesheni 'Makao Makuu Dodoma' kwa mujibu wa sheria ambao waliitaja kama moja ya changamoto inayokwamisha ufikaji wa haraka kambini hapo.

Hatua ya Mkuu huyo wa Wilaya imetokana na kutoridhishwa na maelezo ya Mhandisi Lusubilo William wa Tarura Wilaya ya Handeni ambaye maelezo yalikuwa na utata juu ya hatua zilizochukuliwa dhidi ya mkandarasi huyo ambaye licha ya kuwa nje ya muda, pia ofisi yake haijachukua hatua zozote.

"Kwa kuwa maelezo yako yanajikanyaga, nataka ndani ya siku mbili uje na maelezo kamili ofisini kwangu ya hatua ulizochukua kwa mkandarasi huyu ambaye ameshindwa kazi aliyopewa," alisema Gondwe.

Akihutubia mahafali hayo, Gondwe aliwahimiza vijana wanaohitimu mafunzo hayo kuwa njia na alama bora kwa jamii ikiwamo kuepuka kutumika vibaya na watu wenye nia ovu na taifa lao, na kwamba kufanya hivyo ni kuyatendea haki mafunzo hayo.

Aliwataka vijana hao kuunda vikundi ili waweze kupata fedha zilizotangazwa na serikali za asilimia kumi ya vijana na kinamama kwenye halmashauri zao, huku akiahidi kushughulikia tatizo la maji ambalo alisema limeshapata mwarobaini baada ya mradi mkubwa wa maji wa HTM kutengewa Sh. bilioni moja kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa miundombinu yake.

Awali wahitimu hao waliishauri Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kuanzisha kilimo cha umwagiliaji katika makambi ili kuzalisha vipindi vyote na hivyo kuongeza tija.

HABARI KIMATAIFA

# Utafiti: Wanaopona ebola wanasumbuliwa na figo

**KINSHASA, CONGO**

UTAFITI wa waatalamu wa afya uliofanywa nchini Guinea unaonyesha kuwa, watu wengi waliopona baada ya kupata chanjo ya ebola, afya yao ilidhoofika baada ya kuanza kusumbuliwa na figo.

Watafiti katika ripoti yao iliyochapishwa katika jarida la afya la Lancet, wamesema wamethibitisha hilo baada ya kuwafanyia uchunguzi watu 1,100 waliopona wakati wa mlipuko wa ugonjwa huo katika nchi za Afrika Magharibi miaka miwili iliyopita.

Aidha, ripoti hiyo inaeleza kuwa watu 59 walifariki dunia, mwaka mmoja baada ya kupewa chanjo na tiba ya ebola, na asilimia 62 ya vifo vyote vimeelezwa ni kutokana na kuathiriwa kwa figo zao.

Imeeleza kuwa kinachoshangaza ni kuwa, idadi kubwa ya watu wanaopoteza maisha, ni wale waliokaa hospitalini muda mrefu.

Wataalamu wa afya wanasema, uchunguzi wa kina unastahili kufanywa ili kubaini ni kwanini watu hao waliokuwa wamepata matibabu na kuaminiwa kupona, walikuwa wanafariki dunia kutokana na matatizo ya figo.

Ripoti hiyo imekuja, wakati huu ebola ikiendelea kuzua wasiwasi Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambako kwa kipindi cha mwaka mmoja, watu zaidi ya 2,000 wamepoteza maisha na zaidi ya 3,000 kuambukizwa virusi vya ugonjwa huo hatari.

*RFI*



Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, akiwa na Waziri Mkuu wa China, Li Keqiang alipozuru nchini China. **PICHA: ALLIANCE**

# Idadi waliofariki kwa kimbunga yafikia 43

**NASSAU, BAHAMAS**

IDADI ya watu waliofariki dunia katika mafuriko Bahamas wamefikia 43 na kunauwezekano wa kuongezeka zaidi, maofisa wa ngazi ya juu wamesema.

Hata hivyo, timu ya waokoaji bado inaendele uokoaji na kuzifikia jamii za watu wa nchi hiyo ambao wametengwa na mafuriko na vifusi vya nyumba zao baada ya kimbunga Dorian kupiga eneo hilo.

Waziri wa Afya, Duane Sands, amesema kuwa vifo zaidi ya 13 vimethibitishwa mbali ya vile 30 vya hapo awali, na kwamba huenda idadi hiyo ikaongezek.

Waziri wa Usalama, Marvin Dames alisema vyombo vya usalama bado vinafanya bidii ya kumfikia kila mtu, lakini timu hizo haziwezi kusonga mbele kutokana na vizuizi vya miti iliyoanguka na vifusi vingine kwa sababu inawezekana kuna miili ambayo bado haijagunduliwa.

"Tumewahi kupitia janga kama hili siku za nyuma, lakini siyo katika kiwango hiki cha uharibifu. Huu ni wakati mgumu sana na pia hali tete sana," alisema Dames.

Hata hivyo, alisema anaelewa kwa nini wananchi wanalalamika na wanapaza sauti kuomba msaada baada ya maisha yao kuharibika kutokana na kimbunga Dorian.

Lakini alitoa wito watu wawe wavumilivu wakati serikali ikifanya juhudi ya kuwafikishia msaada wa dharura.

"Hakuna kinachoweza kufanyika kwa siku moja. Hisia kwamba juhudi za haraka lazima zifanyike ni kawaida, tupelekeni kila kitu kinachohitajika mara moja, lakini ukweli ni kwamba unaweza tu ukapeleka msaada wa kiwango fulani kwa wakati mmoja," alisema Dorian.

Juhudi za kutafuta waathirika na walionusurika ziliendelea kwa siku tano. Kimbunga hicho kilikuwa kinasafiri maili 185 (kilomita 295) kwa saa ambacho kiliangamiza nyumba zisizo kuwa na hesabu.

Maofisa walisema watu 43 wamethibitishwa kupoteza maisha lakini walitahadharisha kuwa idadi hiyo inaweza kuongezeka.

Taasisi, nchi na kampuni mbalimbali, ikiwamo Umoja wa Mataifa (UN), Serikali ya Marekani, Jeshi la Ufalme wa Uingereza, Shirika la Ndege la American Airlines, Ufalme wa Caribbean, kwa pamoja wamepeleka chakula, maji, majenereta, vifaa vya kuezeka nyumba, tochi na mahitaji mengineyo.

Seneta wa Marekani, Marco Rubio wa Florida alisema Shirika la Misaada la Marekani limeitaka Wizara ya Ulinzi kutoa ndege zenye uwezo wa kubeba mizigo mizito ili kupeleka mahitaji hayo Bahamas. *VOA*

## Trump afuta mazungumzo Taliban, Afghanistan

**WASHINGTON, MAREKANI**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesitisha mazungumzo ya amani baada ya kundi la wanamgambo la Taliban kudai kuhusika na shambulio la mjini Kabul ambalo lilisababisha vifo vya watu 12, akiwamo mwanajeshi wa Marekani.

Rais Trump alisema amevunja mazungumzo ya amani ya kundi la wanamgambo la Afghanistan la Taliban Jumamosi usiku.

Katika akaunti yake kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter, Rais Trump alisema alikuwa amepanga kukutana na Rais wa Afghanistan pamoja na viongozi wa Taliban nchini Marekani Jumapili.

Rais Trump ameandika kwamba alivunja mazungumzo hayo baada ya Taliban kudai kuhusika na shambulio la mjini Kabul lililosababisha vifo vya watu 12, akiwamo mwanajeshi wa Marekani.

"Ni watu wa aina gani ambao wako tayari kuua watu wengi ili waonyeshe msimamo imara katika majadiliano?" Aliandika Rais Trump katika ukurasa wa Twitter.

"Kama hawawezi kukubali kusitisha mapigano katika mazungumzo haya muhimu ya amani, na wanaweza hata kuwaua watu wasio na hatia 12, hawawezi kuwa na nguvu ya kujadili makubaliano ya kuelewека," aliongeza Rais Trump.

Endapo mkutano huo ungefanyika ingekuwa ni siku chache kabla ya kutimiza miaka 18 tangu Septemba 11, 2001, yalipotokea mashambulizi ya kigaidi yaliyosababisha vifo 3,000 nchini Marekani.

Kundi la Taliban liliwahifadhi wanamgambo wa kundi la al-Qaeda kabla na baada ya kufanya mashambulizi hayo ya kigaidi dhidi ya Marekani.

Duru ya tisa ya mazungumzo iliyomalizika hivi karibuni kati ya Taliban na Marekani mjini Doha, Qatar, ilitoa matumaini ya kufikiwa makubaliano kati ya pande hizo mbili kumaliza vita vya miaka 18 nchini Afghanistan.

Ziara iliyopangwa ya Rais wa Afghanistan, Ashraf Ghani kwenda mjini Washington, Marekani ingeweza kuwa hatua moja ya mbele katika kufikia makubaliano hayo.

Makubaliano na Taliban yangehakikisha kuondoka kwa salama kwa maelfu ya wanajeshi wa Marekani katika miezi ya hivi karibuni, katika taifa hilo lililoharibiwa kwa vita.

Wanamgambo wa Taliban kwa upande wao wangehakikisha kwamba maeneo yaliyo chini ya udhibiti wao hayatumiki dhidi ya Marekani na washirika wake.

Kundi la Taliban limeongeza kasi ya mashambulizi Afghanistan hivi karibuni, kuonyesha nguvu yao kwenye uwanja wa vita.

Kamanda mwandamizi wa Jeshi la Marekani alisema kuongezeka kwa mashambulizi hakusaidii juhudi za amani nchini humo. **DW**

# Waya za simu kwenye nyumba za mabalozi D'Salaam zaibwa

**Na Beatrice Moses**

WIZI wa waya za shaba(coper) za kuwezesha mawasiliano umetajwa kusababisha nyumba kadhaa za mabalozi zilizopo Msasani na Masaki kukosa huduma za simu za mezani.

Meneja wa Mtandao na matengenezo wa Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Kaneth Makanyanga, alimwambia Waziri wa Muungano na Mazingira George Simbachawene, kuwa wizi huo unatokana na soko kubwa lililopo ndani na nje ya nchi kwenye biashara ya vyuma chakavu.

Makanyanga aliyasema hayo juzi wakati Waziri huyo kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais alipokutana na wafanyabiashara wa vyuma chakavu ambavyo pia hutajwa kama taka hatarishi, alipokea maoni mbalimbali kuhusu changamoto zilizopo katika biashara hiyo kubwa duniani.

"Wakusanyaji wa coper waache kuhujumu miundombinu ya serikali, wanunuzi wawe makini, hujuma ni kubwa zimesababisha nyumba hizo za mabalozi kukosa huduma za simu za mezani kwa sababu waya zimeibwa," alisema Makanyanga.

Alisema kutokana na hali hiyo ndiyo sababu kuna kipengele kinachowataka wafanyabiashara kutaja mahali waliponunua ama kuzipata bidhaa zao za vyuma chakavu, ikilenga kuwanasa wanaohujumu miundombinu ya serikali.

"Kwa wanunuzi wa betri TTCL tunazo nyingi ambazo tumekuwa tunazitumia katika maeneo yetu tofauti baada ya muda wa matumizi yake kuisha tunazihifadhi tu, hivyo Baraza la Mazingira lituunganishe na wanunuzi ili tufanye biashara," alisema.

Mfanyabiashara Samson Daniel alisema licha ya kuwapo kwa changamoto nyingine lakini ukosefu wa elimu kuhusu vyuma chakavu ni shida inayozua mengi, hivyo serikali ione umuhimu wa kuandaa mafunzo rasmi yatolewe mjini hadi vijijini.

Alibainisha kuwa elimu hiyo inapaswa kutolewa hadi kwa polisi kwa kuwa wapo ambao wamekuwa wakiwasumbua wanapowakuta na waya za aina yoyote ikiwamo za kwenye compressor.

"Serikali itutambue ione hii ni ajira kama nyingine, itutumie sisi kusaka wezi, hivyo itutengenezee mfumo mzuri hata kwenye soko dalali asiwe na nguvu ya kuzuia muuzaji kumfikia mnunuzi bila kuunganishwa naye, kwa kuwa huoni urasimu ambao unatuumiza," alisema Daniel.

Waziri Simbachawene alisema uharibifu wa mundombinu wa nyaya za simu ni tishio hivyo coper haiwezi kuruhusiwa kutoka kwenda nje ya nchi hadi serikali itakapojiridhisha kwa kufanya utafiti kuhusu vyanzo vya upatikanaji wake.

"Vyuma vinginevyo kama dogo chuma zinaruhusiwa sasa kusafirishwa na kuuzwa nje ya nchi kwa kuwa hakuna viwanda vyenye uwezo wa kurejeleza, lakini coper hapana kwenda nje tunaendelea kutafakari kwanza," alisema Simbachawene.

Alisema biashara hiyo imekuwa ikifanywa katika hali ambayo inaacha mianya ya vitendo vya uhalifu na udanganyifu, ikiwamo tishio la kutumika kusafirisha dhahabu au silaha, ndiyo sababu serikali imeamua kuisimamia kwa karibu zaidi.

Alisema kuwa pikipiki au magari huingia nchini kama bidhaa lakini baada ya hapo zinazochakaa zinakuwa ni malighafi hivyo kuruhusu ziuzwe tena nje ya nchi ni kujihujumu na kusababisha viwanda vya ndani hasa vya kutengeneza nondo.

Alisisitiza kuwa wafanyabiashara hao ni watu muhimu katika utunzaji wa mazingira, kuingiza fedha za kigeni na kutoa ajira kwa vijana kadhaa.



Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule (kushoto waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na Rais wa Taasisi ya Foundazione Same ya nchini Italia, Fransisco Carozza (katikati waliokaa), baada ya kukabidhi msaada wa baiskeli 40 na trekta moja kwa ajili ya kusaidia elimu, wilayani humo, mkoa wa Kilimanjaro juzi. **PICHA: GODFREY MU**

# CRJE yajivunia miaka 50 ujenzi jengo la Nyerere

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Kimataifa ya Ujenzi ya CRJE (East Africa Ltd) ya nchini China, imejivunia miaka 50 ya uwepo wake nchini, huku ikiutumia mradi wa ujenzi wa jengo la Mwalimu Nyerere Foundation square (MNF) lililozinduliwa mwishoni mwa wiki na Rais John Magufuli pamoja na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni, kama kilele cha uthibitisho wa mafanikio ya kampuni hiyo katika kipindi hicho.

Ikiwa ni mwelekeo wake mpya katika masuala ya uwekezaji, mradi huo uliojengwa kwa thamani ya Dola za Kimarekani milioni 150 kutoka Shirika la Kimataifa la Fedha la International Financial Corporation unahusisha uwekezaji wa pamoja baina ya kampuni hiyo ya CRJE (East Africa Ltd) na Taasisi ya Mwalimu Julius Nyerere.

Wakizungumza wakati wa uzinduzi huo, marais wote wawili waliipongeza kampuni pamoja na Mfuko wa Mwalimu Julius Nyerere kwa mradi huo unaenda sambamba na maadhimisho ya miaka 20 ya kifo cha Mwalimu Julius Nyerere.

"Sote tunatambua na kushukuru mapenzi aliyokuwa nayo Hayati Mwalimu Julius Nyerere kwa Watanzania na Waafrika katika kupigania usawa, haki na uhuru. Ni wajibu wetu sote kuendeleza jitihada ili kumuenzi kwa vitendo, alisema Rais Magufuli.

Alisema Watanzania sasa wataweza kujifunza masuala mengi kuhusu Mwalimu Nyerere kupitia taarifa na kumbukumbu muhimu zitakazopatikana katika jengo hilo ikiwamo vitabu, hotuba na vyanzo vingine.

Kwa upande wake Rais Museveni alibainisha amekuwa mfuasi mkubwa wa Mwalimu Nyerere tangu mwaka 1963 wakati wa jitihada za kutafuta uhuru wa Afrika Mashariki sambamba na jitihada zake katika kukitangaza Kiswahili.

Balozi wa China nchini, Wang Ke, alisema uzinduzi wa jengo hilo ni kumbukumbu nzuri kwa Hayati Mwalimu Nyerere na uwapo wake unaongeza alama ya uhusiano wa muda mrefu katika ya nchi hizo mbili za Tanzania na China.

Jengo hilo lenye ghorofa 30, limejengwa kwenye eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 63,000 na lihahusisha hoteli ya kisasa yenye hadhi ya nyota tano ikiwa na vyumba 256, ofisi, maduka, kumbi za mikutano pamoja na sehemu za kupaki magari.

Kwa mujibu wa Rais wa kampuni ya China Railway Construction Engineering Group ambayo ni kampuni mama ya CRJE (East Africa Ltd), Guo Junliang, tangu enzi za ujenzi wa reli ya Tazara miaka ya 1960, shirika hilo limekamilisha miradi mikubwa ya ujenzi zaidi ya 130 hapa nchini ikiwamo ujenzi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lililopo jijini Dodoma, Daraja la Nyerere, Ukumbi wa Mikutano wa Dodoma yaani Dodoma Convention Center, Hoteli ya Hyatt Regency Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma.

# Onyo vyandarua visivyo na dawa

**Na Mwandishi Wetu, BAGAMOYO**

WATANZANIA wameonywa dhidi ya matumizi ya vyandarua visivyo na dawa vinavyouzwa mitaani kwa sababu haviwezi kudhibiti maambukizi ya ugonjwa wa malaria kikamilifu.

Akizungumza na waandishi wa habari, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani mwishoni mwa wiki, wakati wa mkutano wa wadau wa masuala ya afya ambao walikuwa wakijadili mwelekeo wa ugonjwa wa malaria nchini, Mkurugenzi wa Mradi wa VectorWorks, Waziri Nyoni, alisema sio kila chandarua ni sawa kwa matumizi ya kujikinga na mbu bali chandarua chenye dawa kinakuwa na kinga madhubuti.

Nyoni alisema sifa ya vyandarua vyenye dawa vinavyosaidia kufukuza mbu, kuzuia mbu kung'ata na dawa iliyopo katika chandarua inauwezo wa kumuua mbu.

"Watu wanapaswa kutumia vyandarua hivi venye dawa kwani vimethibitishwa kisayansi na Shirika la Afya ulimwenguni na vyandarua hivyo havina madhara yoyote kwa binadamu," alisema Nyoni.

Aidha, alisema jamii inapaswa kuacha dhana potofu juu ya vyandarua hivyo kwani tayari shirika limeshavithibitisha kwa matumizi ya binadamu kwa lengo la kujikinga na maambukizi ya malaria.

"Nawasisitiza Watanzania kuwa matumizi ya vyandarua yatumiwe kila siku, watu wazingatie kulala kwenye vyandarua vyenye dawa ili viwakinge na maambukizi ya malaria," alisema na kuongeza kuwa

"Kwa Tanzania mradi huu tunafanya kazi katika maeneo matatu kwa upande wa sera tumeangalia kama kuna sera zinazosapoti mradi huu, utekelezaji wa ugawaji wa vyandarua kama upo hivyo tulikuwa tunaangalia vyandarua vinapatikana katika vituo vya afya na maeneo mengine, tunaimani kumalizika kwa mradi huu serikali na taasisi zake zitaweza kuendeleza mambo yaliyofanywa na mradi huu ambao umemalizika Agosti mwaka huu."

Msimamizi wa Kitengo cha Kupambana na Malaria (NMCP), Winfred Mwafongo, alisema chandarua kinatakiwa kutumika sehemu ya kulala binadamu kwa lengo la kujikinga na malaria na si kwa matumizi mengine.

Mradi wa Vector Works upo chini ya Shirika la Johns Hopkins Center for Communication kwa ufadhili wa Shirika la Msaada la Marekani (USAID) kupitia mfuko wa Rais wa Marekani wa kudhibiti maralia (PMI).

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NAFASI ZA KAZI**

**PROJECTS GENERATE INCOMES AND CREATE EMPLOYMENT**

* Learn DESIGNING projects
* Find DONORS
* Establish NGO

0784505108
0769505108

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


## KUPOTELEWA NA CHETI



**Deus Ngelanizya** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne, shule ya sekondari Geita chenye Index namba **S/386/40** kilichotolewa na baraza la mtihani la Taifa Mwaka 1982 Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi au apige simu namba **0753 350725**
Taarifa ya Polisi **RPT/RB/1227/93**

215409502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi 63/2019**

**Ombi la ABDULHAMID SALUM kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu SALUMU HASSAN JABIRI**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 20/9/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 5/09/2019.

COURT SEAL URBAN COURT DODOMA DISTRICT

Sahihi ya Hakimu
PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

215409402

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

REGINA LEONARD LUBAGO. Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya Boxer, yenye Namba MC113BAF, chasis No.MDZDDCWZZSWKI6343, Engine No. DUMBSK43549. Kadi ilipotea, na aliripoti kituo cha polisi cha Bukoba tarehe 28/06/2019 na kupewa No: KAG/BUK/RB/91933/2019.

Kwa yeyote atakayeiona haipeleke kituo cha polisi kilichoko karibu naye.

Au awasiliane naye.
No: 0764213340.

115409802


*Uza, Chenye Thamani Kubwa*

*Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0767 223311*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# OWEN AMCHAMBUA RASHFORD

**LONDON, England**

GWIJI wa soka wa England, Michael Owen, amesema kwamba mshambuliaji, Marcus Rashford wa Manchester United hana yale makali ya kuua anapokuwa mbele ya goli la wapinzani.

Owen alisema kwamba mshambuliaji ambaye asili yake ni kufunga, kitu kama hicho cha hisia ya kumaliza mechi kwa maana ya kufunga mabao kwa nafasi chache anazopata kinakuwa kwenye damu yake na si kama alivyo Rashford, anayehitaji nafasi nyingi kufunga mara moja.

Rashford amefunga mabao 47 katika mechi 174 alizoichezea Man United tangu alipoanza kwenye nusu ya pili ya msimu wa 2015-16.


Kwa msimu huu, fowadi huyo mwenye umri wa miaka 21, amefunga mara mbili kwenye mechi nne alizocheza kwenye Ligi Kuu England, lakini nafasi za kufunga alizopoteza kwenye mechi za karibuni, zimefanya wengi kuzungumza kuhusu Man United kumtegemea mchezaji huyo kama mfungaji wao.

Owen, mwenye mabao 150 kwenye Ligi Kuu England, amekuwa akimkubali sana Rashford, lakini sasa amehoji kuhusu uwezo wake wa kufunga.

"Sidhani kama kufunga mabao ni kitu unachoweza tu kwenda kukiota kitandani," alisema Owen.

"Yeye anakontroo nzuri na ufundi kwenye mpira, mimi sikuwa nawezi hivyo, lakini linapokuja suala la kuua mechi ni tofauti. Wapo wachezaji wenye hiyo kitu kama Robbie Fowler, Sergio Aguero au Harry Kane, watu wanaopagawa na mabao."

Owen alifunga mabao 17 katika mechi 52 alizochezea Man United katika kipindi cha miaka mitatu aliyodumu Old Trafford.



# SEMENYA
## AJIUNGA NA TIMU YA SOKA

GAUTENG, Afrika Kusini

BINGWA mara mbili wa Olimpiki katika mbio za mita 800, Caster Semenya amejiunga na timu ya soka ya wanawake nchini Afrika Kusini.

Mwanariadha huyo mwenye umri wa miaka 28, hawezi kushiriki katika mbio za mita 800 bila kutumia dawa za kupunguza homoni za kiume mwilini mwake kwa mujibu wa sheria mpya iliyoidhinishwa na Shirikisho la Riadha Duniani (IAAF).

Hatua hiyo inamaanisha kwamba hawezi kutetea ubingwa wake wa mita 800 mjini Doha mwezi ujao, ingawa bado anapigania kubadilishwa kwa sheria hiyo kupitia mahakama.

Kwa sasa amejiunga na klabu ya soka ya wanawake iliyopo Gauteng kwa jina JVW.

Bingwa huyo mara tatu alitangaza Julai kwamba hatotetea ubingwa wake katika mbio za mita 800 kwa kuwa hawezi kuanza kuichezea JVW hadi msimu wa 2020, baada ya kujiunga na timu hiyo nje ya dirisha la uhamisho.

"Ninatazama kuanza safari mpya, nashukuru mapenzi na uungwaji mkono niliopata kutoka kwa timu hii," Semeya alinukuliwa na mtandao wa klabu hiyo.

JVW FC, ilianzishwa mwaka 2013 na nahodha wa timu ya Taifa ya Wanawake nchini Afrika Kusini Janine van Wyk, akitaka kuwatambua, kuwaimarisha na kuwafichua wachezaji wa kike.

Klabu hiyo ni miongoni mwa klabu kubwa katika ligi mkoa wa Gauteng - Ligi Kuu ya Wanawake nchini Afrika Kusini imegawanyika katika makundi manane ya kimkoa. Mmiliki wa klabu hiyo, Van Wyk aliambia BBC kwamba Semenya hajaacha kukimbia.

Alisema: "Yuko katika mapumziko kwa wakati huu ndio maana ana muda wa kufanya kitu tofauti.

Ameshiriki mazoezi mara mbili na timu hii na unaweza kuona kwamba anajua kucheza soka, lakini bado ni sharti kumsaidia kidogo kwa kuwa uchezaji ni tofauti na riadha.

Kumuona katika ligi hii ni jambo jema na nadhani wasichana wadogo watapata msukumo mkubwa kutoka kwa Caster.

Semenya si mwanariadha wa kwanza kujiunga na kandanda - baada ya kustaafu mwaka 2017, Usain Bolt alifanya mazoezi na klabu moja ya Norway Stromsgodset na nyingine ya Australia Central Coast Mariners, lakini hakupata mkataba.

Semenya pia anafuata nyayo za Maria Mutola wa Zambia ambaye alijiunga na kandanda baada ya riadha.

IAAF iliamua kuweka sheria hiyo kwa madai kwamba wanariadha wanawake walio na homoni nyingi za kiume wana uwezo zaidi ya wenzao wa kike.

Wanariadha hao wametakiwa kutumia dawa ili kupunguza viwango vya homoni hizo ili kuweza kushiriki katika mita 400 hadi 1500 la sivyo waingie katika mbio nyingine ndefu.

**GOFU...**



Mchezaji wa timu ya Benki ya NMB, Lukundo Toroka, akipiga mpira mwishoni mwa wiki wakati wa michauno ya gofu ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania (NMB CDF Cup 2019) yaliyodhaminiwa na benki hiyo. **MPIGAPICHA WETU**

# BARCA KUTOMSAJILI TENA NEYMAR

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona haitamsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain, Neymar wakati wa kipindi cha dirisha dogo la usajili Januari, kwa mujibu wa Rais wa mabingwa hao wa Hispania, Josep Maria Bartomeu.

Barcelona walijaribu msimu wote huu kuzungumza kuhusu mkataba wa kumsaini kiungo huyo wa Brazil ambaye alihamia Ufaransa kwa dau lililovunja rekodi ya dunia la pauni milioni 200 mwaka 2017, lakini klabu hizo mbili hazikukubaliana.

Alipoulizwa iwapo kulikuwa na uwezekano wa Barcelona kumsaini Neymar Januari, Bartomeu alisema kwa sasa hapana.

Mshambuliaji huyo amefunga mabao 34 katika misimu miwili akiichezea miamba hiyo ya Ufaransa, ingawa majeraha yaliathiri kampeni yake katika misimu yote miwili.

Bartomeu alipinga mapendekezo hayo kwamba klabu hiyo ilikuwa ikimlenga Neymar msimu huu akiongeza kwamba uwezekano wa kumsaini lilikuwa suala la ziada tu.

Akizungumza katika mtandao rasmi wa runinga ya klabu hiyo aliongeza: "Barca tayari imepanga kikosi chake. Fursa ya kumsaini Neymar ni mojawapo iliojitokeza katika soko. Usajili wake ungekuwa wa ziada, haukupangwa."

## HABARI MICHEZO




# GUARDIOLA kakataa usajili wa Coutinho

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola ameripotiwa kwamba alisitisha mpango wa kumsajili kiungo wa Barcelona, Philippe Coutinho wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Gazeti la Marca limeripoti kwamba kocha huyo wa Manchester City, Guardiola alifuatwa na mabosi wa Barcelona wakimtaka amchukue Mbrazil huyo wakati walipokuwa wakitaka kumwondoa kwenye kikosi chao.

Coutinho, ambaye aliachana na Liverpool kwenda Nou Camp kwa ada ya pauni milioni 140 Januari 2018, aliambiwa akusanye mabegi yake atafute pakwenda baada ya Barcelona kutumia pauni milioni 105 kumnasa fowadi wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann.

Mabosi wa Barca waliamini kwamba Guardiola angeshawishika juu ya kumchukua staa huyo wa Kibrazil ili akakipige Etihad, lakini mambo yamekuwa tofauti na kocha huyo hakuhangaika licha ya kwamba staa wake Leroy Sane ameumia na atakuwa nje ya uwanja kwa kipindi kirefu.

Baada ya dili hilo kukwama, Barcelona wameamua kumpeleka Coutinho kwa mkopo huko Bayern Munich, huku kukiwa na makubaliano ya Wajerumani hao kumchukua jumla mwakani kama watafurahishwa na huduma yake.

Dirisha la usajili England lilifungwa mapema tofauti na nchi nyingi za Ulaya, jambo ambalo limewafanya kushindwa kutimiza baadhi ya dili.

Bayern wamelipa pauni milioni 7.5 kwenye mkopo huo wa Coutinho, huku wakiwa na makubaliano ya kumchukua jumla kwa pauni milioni 107 hapo mwakani.

# Nike kumtajirisha zaidi Ronaldo

**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo, atapata dola milioni 139 katika mkataba wake mpya na kampuni ya kutengeneza vifaa vya michezo ya Nike.

Hiyo imebainika katika nyaraka za Football Leaks zilizokaririwa na jarida la michezo la Der Spiegel lililotoka Ijumaa.

Mkataba wake mpya, pia unajumuisha bonasi ya dola milioni nne kwa kushinda tuzo binafsi, kwa mujibu wa mkataba wa awali.

Ronaldo, ambaye alijiunga na Juventus mwaka 2018, baada ya kuichezea Real Madrid na Manchester United katika kipindi kilichompatia vikombe kadhaa, amekuwa na mkataba na kampuni kubwa ya nguo ya Marekani tangu mwaka 2004 ambao ulimhakikishia ada ya euro milioni 3.65.

"Kwa kadri Ronaldo anavyochezea klabu ya Daraja A, anatakiwa alipwe euro milioni 16.2 kila mwaka," jarida hilo la Ujerumani limesema.

Nike ilijibu taarifa ya jarida hilo kwa kusema: "Hatuzungumzii mikataba ya wanamichezo."




# ARSENAL YAJIPA MATUMAINI KWA AUBAMEYANG KUSAINI



**LONDON, England**

KLABU ya Arsenal inajiamini kwamba mshambuliaji wake, Pierre-Emerick Aubameyang, atasaini mkataba mpya na kuendelea kukipiga kwenye kikosi chao kwa muda mrefu.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Gabon amekuwa kwenye kiwango bora huko Arsenal tangu alipojiunga akitokea Borussia Dortmund kwenye dirisha la Januari 2018 - akifunga mabao 44 katika mechi 69 alizoitumikia klabu hiyo ya London.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, ameshafunga mabao matatu katika mechi nne za Ligi Kuu England alizochezea Arsenal msimu huu, huku mabao hayo likiwamo la kusawazisha dhidi ya mahasimu wao Tottenham Hotspur kwenye mchezo wa London 'dabi' wikiendi iliyopita.

Dili la sasa la Aubameyang huko Emirates litafika tamati Juni 2021, lakini Manchester United kuna wakati walitajwa kuwa na mpango wa kunasa saini yake.

Hata hivyo, gazeti la Daily Mail limeripoti kwamba kikosi hicho kinachonolewa na kocha Unai Emery kina imani kubwa kwamba mshambuliaji wao atasaini mkataba mrefu wa kuendelea kubaki kwenye kikosi chao.

Aubameyang alifunga mabao 141 katika mechi 213 alizoicheza Dortmund kabla ya kutua zake Arsenal kwa ada ya pauni milioni 56 kipindi hicho timu ilipokuwa chini ya kocha Arsene Wenger.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KANE APIGA HAT-TRICK, AWEKA REKODI ENGLAND

Ni wakati wakiinyuka Bulgaria 4-0, sasa amekuwa mchezaji wa kwanza England kufunga...

**LONDON, England**

ENGLAND imeendelea kuwa na mwanzo mzuri wa asilimia 100 wa kufuzu kwa michuano ya Euro 2020 wakati mabao matatu 'hat-trick' ya Harry Kane yaliisaidia kupata ushindi wa 4-0 dhidi ya Bulgaria kwenye Uwanja wa Wembley juzi Jumamosi.

Kikosi hicho cha kocha, Gareth Southgate kilipata ushindi wake huo wa tatu mfululizo kwenye kundi lake la A na tangu mwanzo walionekana kuwa kwenye nafasi nzuri baada ya bao la uongozi la Kane la dakika ya 24. Nahodha huyo wa 'Simba Watatu' aliongeza la pili kwa mkwaju wa penalti, kabla ya kumtengenezea Raheem Sterling aliyefunga la tatu kisha Kane akafunga bao la nne dakika ya 73 na kufikisha mabao yake matatu kwenye mchezo huo.

Baada ya mchezo huo kuanza Kane alikuwa kwenye nafasi nzuri ya kupata bao la uongozi kwa timu yake katika dakika ya 19, kabla hajaifikia pasi ya Raheem Sterling, alionekana ameotea, lakini dakika tano baadaye alitumia vizuri makosa ya golikipa Plamen Iliev aliyeutema mpira, akafunga bao lake la 23 kwa England.

Jordan Pickford alicheza vizuri na Marcus Rashford ambaye alikuwa kwenye nafasi nzuri ya kufunga kabla ya kufanyiwa madhambi na Nikolay Bodurov na kuzaa penalti iliyofungwa na Kane.

England kwa sasa wanaongoza kwenye msimamo wa kundi lao kwenye michuano hiyo ya kufuzu michuano ya Ulaya. Kwa sasa wanaongoza kundi hilo wakiwa wamecheza mechi tatu za kufuzu.

England haijafungwa kwenye mechi 11 dhidi ya Bulgaria sawa na Finland na Uturuki. Simba hao watatu hawajafungwa katika mechi zake 42 za kufuzu kwa michuano ya Ulaya na Kombe la Dunia, tangu walipopoteza 1-0 kwa Ukraine Oktoba 2009.

Aidha, Kane amekuwa mchezaji wa kwanza wa England kufunga mabao 25 au zaidi katika mechi 40 tangu Gary Lineker alipofunga mabao 27 na 'hat-trick' ya juzi ilikuwa ni ya 13 kufunga kwenye klabu na nchi yake (amefunga hat-trick 11 kwa Spurs na mbili kwa England.

Kwa upande wa Sterling, amehusika katika mabao tisa kwenye mechi saba alizoichezea England (akifunga mara saba na kutoa pasi za mwisho mbili katika mechi 33).

Naye mchezaji wa Atletico Madrid, Kieran Trippier ni mchezaji wa kwanza kuichezea England akiwa anacheza kwenye Ligi Kuu ya Hispania tangu David Beckham (Real Madrid) Juni 2007.

## KWA UFUPI

**JUVE YAMGEUKIA DE GEA**
Juventus itafungua mazungumzo na kipa wa Manchester United, David de Gea, 28, katika dirisha la Januari, na klabu yake tayari imeshaanza kuandaa warithi wa Mhispania huyo. ***(Sunday Express)***

**MBAPPE KIPORO MADRID**
Real Madrid itajaribu kumsajili straika Mfaransa Kylian Mbappe, 20, kutoka Paris St-Germain majira ya joto yajayo. ***(Sport - in Spanish)***

**NEYMAR LULU WACHEZAJI BARCA**
BAADHI ya wachezaji wa Barcelona walitoa ofa ya fedha zao binafsi kuchangia dau la kumnunua mshambuliaji wa PSG, Mbrazil Neymar, 27, majira haya ya joto. ***(Marca)***

**GUARDIOLA AMTAKA SKRINIAR**
Manchester City itatoa ofa kwa beki wa kati wa Inter Milan na Slovakia, Milan Skriniar, 24, katika dirisha la Januari, na kocha Pep Guardiola anahitaji kutatua tatizo la majeruhi kwenye safu ya ulinzi. ***(Sunday Express)***

**VAN DER SAR KUULA UNITED**
MANCHESTER United ipo katika hatua za mwisho kukamilisha kumteua kipa wao wa zamani, Mholanzi Edwin van der Sar kuwa mkurugenzi wa soka. ***(Sunday Mirror)***

**VAN DIJK KUJIFUNGA MIAKA 6**
Virgil van Dijk, 28, amekubali mkataba mpya wa miaka sita na Liverpool baada ya klabu hiyo kufanyia kazi suala la kumbakiza ikiepuka asije kupandiwa beki kama ambavyo Manchester United ilivyofanya kwa Harry Maguire kumnunua kwa pauni milioni 80 kutoka Leicester City. ***(Sunday Mirror)***

**SEVILLA IMEITIBULIA WEST HAM**
MSHAMBULIAJI wa Mexico, Javier Hernandez, 30, angeweza kubaki West Ham kwa kipindi kilichobaki katika mkataba wake kama Sevilla isingetoa ofa kwake wiki ya mwisho kabla ya dirisha la usajili kufungwa. ***(Football.London)***

**NDOMBELE AKOMALIA KIINGEREZA**
KIUNGO wa Tottenham, Mfaransa Tanguy Ndombele, 22, amekuwa akijifunza Kiingereza ili kuweza kuzoea vema maisha ya London baada ya kujiunga na klabu hiyo majira haya ya joto akitokea Lyon. ***(Football. London)***

**DZEKO AMSOMA MKHITARYAN**
MSHAMBULIAJI wa Roma, Edin Dzeko anatazama namna ya kuweza kufanya kazi na mchezaji mwenza, Henrikh Mkhitaryan, 30, baada ya kiungo huyo wa kimataifa wa Armenia kujiunga na miamba hiyo ya Serie A akitokea Arsenal kwa mkopo majira haya ya joto. ***(Corriere Dello Sport - in Italian)***

**CUADRADO KUMKIMBIA SARRI**
WINGA wa Juventus, Juan Cuadrado, 31, atasitisha mazungumzo ya mkataba na mabingwa hao wa Italia. Nafasi ya kucheza kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, imekuwa finyu chini ya kocha mpya, Maurizio Sarri. ***(Goal)***

**KISA NKETIAH KUTIMKA ARSENAL**
MSHAMBULIAJI wa England U-21, Eddie Nketiah, 20, amechagua kutimkia Leeds United kwa mkopo akitokea Arsenal ili kujipa nafasi nzuri ya kuweza kuchomoza kikosi cha kwanza hapo Gunners kwa mbeleni. ***(Mail on Sunday)***

**LOPETEGUI AMTAJA FERNANDEZ**
kocha wa Sevilla, Julen Lopetegui alitaka kumsajili beki wa Hispania, Nacho Fernandez, 29, kutoka kwa wapinzani wao wa La Liga, Real Madrid majira haya ya joto. ***(Marca)***



# AUSSEMS: MZAMIRU ANAIBEBA SIMBA SC

**Na Somoe Ng'itu**

KIUNGO mzalendo wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Mzamiru Yassin, ametajwa kuwa mmoja wa wachezaji muhimu katika kikosi hicho, ambao hufanya kazi kubwa kusaidia ushindi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, alisema Mzamiru ni mmoja wa wachezaji wanaojituma na kutimiza majukumu yake kwa kiwango cha juu.

Aussems alisema kiungo huyo hupata pointi nyingi katika kila mechi anayocheza na kwake anamfananisha na "mashine" muhimu katika kikosi chake.

"Ni mchezaji mzuri, hufuata maelekezo na hucheza kwa hesabu, anajua kucheza katika eneo lake, kwa kumwangalia kiufundi, nasema ni mchezaji muhimu," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

Pia amemtaja ni mchezaji anayependa kufanya mazoezi wakati wote na ushindani wa kuwania namba katika kikosi cha kwanza umesaidia kumuimarisha.

"Kila mmoja anapenda kuwapo katika kikosi cha kwanza, na kama upo, utaona hakuna mchezaji anayezembea kwa sababu hawataki kuona wanaanzia benchi, kurudi katika kikosi hicho huitaji nguvu ya ziada, kwa kifupi nafurahishwa naye na kazi anayoifanya," Aussems aliongeza.

Mzamiru alijiunga na Simba misimu miwili iliyopita akitokea Mtibwa Sugar ya Manungu, Morogoro sambamba na Mohammed Ibrahim "Mo" na Shiza Kichuya, ambao wote wameshaondoka kwa 'Wekundu wa Msimbazi' hao na kujiunga na klabu nyingine.

**POOL...**



Mkurugenzi wa TBL, Philip Redman, akionyesha umahiri wa kucheza pool wakati wa uzinduzi wa timu ya kampuni ya mchezo huo katika hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki Kiwanda cha Ilala jijini Dar es Salaam, ambapo pia alikabidhi meza mbili za pool kwa timu hiyo. Wengine pichani ni wachezaji wa timi hiyo. **MPIGAPICHA WETU**

# Yanga yaikomalia TFF pensi ya Zahera

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Klabu ya Yanga umemkatia rufani kocha wake Mwinyi Zahera kupinga kufungiwa kutokana na madai ya kutoa lugha chafu kwa Bodi ya Ligi.

Bodi ya Ligi ilimfungia Zahera kutoitumikia timu yake kwa mechi tatu na kupigwa faini ya laki tano (500,000) kutokana na kutovaa nadhifu.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema jana kuwa, tayari wameshaka rufani na wamepeleka barua Bodi ya Ligi na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) ili waweze kutoa maamuzi.

"Maamuzi mbalimbali ya TFF na Bodi ya Ligi hayapo sahihi, kuna mambo mawili ambayo yamejitokeza ya kumfungia kocha wetu kutocheza mechi tatu na penalti aliyoipata ya kutakiwa kulipa Sh. 500,000 kutokana na madai ya kutovaa kwa unadhifu.

"Ukiangalia kanuni suala nadhifu linaangalia usafi, uvae nguo ambayo ni safi. Hivyo suala la kuvaa pensi ni la kawaida kwani tumeweza kushuhudia wachezaji, waamuzi, na hata duniani kote pensi ni vazi la kawaida hivyo tumeangalia kwa ujumla wake na tumeona kama klabu tumekosea wapi.

"Tumelikatia rufani tuone tumekosea wapi tumepeleka malalamiko yetu kwenye Bodi ya Ligi na TFF kwa kuwapatia barua ili waweze kupitia na kutoa maamuzi sahihi na kutoa tafsiri ya unadhifu."

# Mchenga yatinga robo fainali Sprite Bball Kings

**Na Sabato Kasika**

BINGWA wa Sprite Bball Kings 2018, timu ya kikapu ya Mchenga Bball, imetinga robo fainali kwa kuichapa Temeke Heroes vikapu 114 - 92, katika mwendelezo wa kumsaka bingwa wa michuano hiyo mwaka huu.

Timu nyingine zilizotinga robo fainali ni Dream Chaser ambayo iliichapa Yo Street vikapu 109-90, huku Tamaduni ikiiondoa Nothing But Nets katika mashindano hayo kwa vikapu 87- 76.

Katika mwendelezo wa mechi hizo zilizochezwa Jumamosi kwenye viwanja vya Don Bosco, jijini Dar es Salaam, Water Institute iliifungisha virago Stylers kwa vikapu 76-70.

Timu nyingine zilizotinga robo fainali kwa mechi za jana, Jumapili ni Ukonga Hitmen ambayo iliizamisha JK Ballers kwa vikapu 107- 69, kisha KG Dallers nayo ikawatupa nje Wagalatia kwa vikapu 79- 76, wakati TMC ikiwabebesha Weusi vikapu 120- 75.

Baada ya kumaliza mzunguko huo uliozikutanisha timu 16, msemaji wa mashindano hayo Goza Chuma, alisema robo fainali itaendelea Septemba 15, mwaka huu baada waaandaaji watakapokutana kupanga ratiba. Chuma alisema mashindano hayo yanaandaliwa na East Africa Televisheni na East Africa Radio kwa kushirikiana na kinywaji cha Sprite ili kuibua vipaji vya mpira wa kikapu nchini.

"East Africa Televisheni na East Africa Radio ni chombo cha habari kinachoziunganisha nchi za Afrika Mashariki kikiwalenga zaidi vijana kuanzia miaka 18 hadi 35 ili kuwahabarikisha, kuwaburudisha na kuwaelimisha kupitia vipindi mbalimbali," alisema Chuma.

# Jafo aipongeza Pete Tamisemi

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, ameipongeza timu ya mpira wa pete ya Tamisemi iliyokuwa ikishiriki mashindano ya Ligi Kuu Tanzania Bara, kwa kufuzu kushiriki mashindano ya Ligi ya Muungano yatakayofanyika Novemba mwaka huu visiwani Zanzibar.

Jafo alitoa pongezi hizo jana jijini hapa wakati alipokuwa akizungumza na wachezaji pamoja na uongozi wa timu hiyo ambayo imeshika nafasi ya nne na kukataa tiketi ya kushiriki mashindano ya Ligi ya Muungano Zanzibar Novemba mwaka huu.

Alisema akiwa kama waziri mwenye dhamana ya Tamisemi, anajivunia timu hiyo kwa kufanya vizuri katika mashindano hayo pamoja na changamoto mbalimbali walizokuwa nazo.

"Niwapongeze sana kuwa sisi kama Tamisemi tunayo timu nzuri sana, hivyo kinachohitajika ni maandalizi ya kutosha ili katika mashindano ya Muuungano Zanzibar tuweze kufanya vizuri zaidi," alisema Jafo.

Aliutaka uongozi wa timu hiyo kuyafanyia kazi mapungufu waliyoyabaini katika mashindano hayo yaliyokwisha ili watakapo kwenda katika michuano ya Muungano wasipate vikwazo.

"Kama ipo haja kusajili wachezaji wengine ili kuongeza nguvu fanyeni hivyo ili tunapokwenda Zanzibar tuwe tofauti na tuliyokuwa hapa Dodoma," alisema Jafo.

Aidha, katika kuwapatia motisha wachezaji wa timu hiyo Jafo ameagiza itafutwe fedha kiasi kisichopungua Sh. 500,000 hadi milioni moja kwa kila mchezaji ili kuwaongezea morali ya mchezo.

# Michezo

Jumatatu Septemba 9, 2019

Nipashe




Kane apiga hat-trick, aweka rekodi HABARI UK 30



Mbwana Samatta na Simon Msuva wakishangilia. **PICHA: MTANDAO**

# STARS YAFYEKELEA MBALI WARUNDI

## ●●●Kaseja azidi kuwa shujaa, sasa watinga hatua ya makundi kuwania kufuzu Kombe la Dunia Qatar 2022 huku…

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya soka ya Tanzania, Taifa Stars imefanikiwa kutinga hatua ya makundi kuwania kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia mwaka 2022 litakalofanyika nchini Qatar, baada ya kuifyekelea mbali Burundi kwa mikwaju ya penalti 3-0.

Katika mechi hiyo hiyo iliyopigwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana, shukrani kwa mara nyingine zimemwendea kipa Juma Kaseja baada ya kuanza kucheza mkwaju wa kwanza wa penalti ya Burundi mbali na kuwafanya kupiga zilizofuata kwa presha, ukiacha kazi kubwa aliyoifanya katika dakika 120 za mechi hiyo.

Mechi hiyo ni baada ya ile ya Jumanne iliyopita nchini Burundi, timu hizo zilipotoka sare ya bao 1-1 na jana ndani ya dakika 120 kumalizika kwa matokeo kama hayo ya awali, hivyo changamoto ya mikwaju ya penalti kuchukua nafasi yake.

Kwa Kaseja hiyo ni mara ya pili mfululizo tangu arejeshwe Stars, kuibeba timu hiyo baada ya mwezi uliopita kucheza tena mikwaju ya penalti wakati wakiitoa timu ya Taifa ya Kenya, Harambee Stars kwenye kinyang'anyiro cha kuwania kufuzu fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

Erasto Nyoni, Himid Mao na Gadiel Michael ndiyo waliofunga mabao ya kipa Jonathan Hahimana anayeichezea KMC ya Kinondoni, aliyeingia dakika za mwishoni kwa ajili ya kudaka penalti, lakini zikamshinda.

Omari Ngando, Saedo Berahino na Gael Bigirimana walikosa penalti zao, huku Kaseja akiwa shujaa kwa kuokoa penalti moja ya Ngando, zingine mbili zikitoka nje.

Mechi ilianza kwa kasi kwa timu zote kushambulia kwa zamu ili kupata bao dakika za mwanzoni, lakini washambuliaji wa timu zote hawakuwa makini.

Ilikuwa ni dakika ya 29, Stars ilipofanikiwa kupata bao la kwanza lililowekwa wavuni na Mbwana Samatta, baada ya kona iliyochongwa na Hassan Kessy kutoka magharibi mwa uwanja, kabla hajaiunganisha na kusindikizwa na mmoja wa mabeki wa timu ya Burundi.

Wakati kila mmoja akiamini kuwa Stars ingekwenda mapumziko ikiongoza kwa bao moja, Fiston Abdulrazak aliisawazishia Burundi baada ya kufanya shambulizi la nguvu.

Shuti lililotemwa na kipa Juma Kaseja lilileta kizaazaa, kabla mfungaji hajapatiwa pasi safi na kuujaza wavuni.

Kipindi cha pili Stars ilifanya mashambulizi mengi kwenye lango la wapinzani wao, huku Simon Msuva akikaribia kuiandika bao la pili dakika ya 54 alipopiga shuti kali akiwa na kipa Justin Ndikumana, lakini liliishia mikononi mwa kipa huyo.

Dakika ya 85 na 89, Shaaban Chilunda aliyeingia kipindi cha pili, alikosa mabao ya wazi akibaki yeye na kipa Ndikumana.

Nusura Burundi wafunga bao la pili dakika za majeruhi, lakini kipa Kaseja alionyesha umahiri mkubwa kwa kupangua na kuwa kona tasa.

Ziliongezwa dakika 30, kwani matokeo ya jumla yalikuwa ni mabao 2-2, zikitoka sare ya bao 1-1 kila mechi kwa nyumbani na ugenini.

Kwa matokeo hayo, Stars inaingia kwenye makundi yatakayopangwa baadaye kwa ajili ya kusaka tiketi hiyo, Afrika zikitakiwa timu tano tu kwa ajili ya fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

## Molinga aamsha mzuka Yanga SC

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya juzi kufanikiwa kufunga bao lake la kwanza tangu ajiunge na Yanga, mshambuliaji David Molinga, anatarajiwa kuanza kufanya mambo "matamu" kwa timu yake katika msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, imeelezwa.

Molinga alifanikiwa kuisawazishia Yanga bao dakika za majeruhi katika mchezo wa kirafiki dhidi ya Pamba FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza uliochezwa juzi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Wenyeji Pamba ndio walikuwa wa kwanza kupata bao kupitia kwa mshambuliaji wao, Saad Kipanga, aliyetikisa nyavu za Yanga dakika ya 37 ya mchezo huo ambao ulikuwa maalumu kwa mashabiki wa Kanda ya Ziwa.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, alisema bao hilo litaamsha morali na litamwongezea nguvu mshambuliaji huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ambaye huu ni msimu wake wa kwanza tangu asajiliwe klabuni hapo.

Zahera alisema sasa Molinga hatakuwa na wasiwasi kama alivyokuwa katika mechi zilizopita, na anatarajia ataanza kuonyesha makali yake ya kufunga mabao ambayo anayafahamu kwa muda mrefu. "Ingawa amekosa kufunga nafasi nyingine mbili, lakini hili bao litamfanya awe anajiamini tofauti na siku za nyuma, mchezaji anapofunga, akili na mwili wake hutulia zaidi katika mchezo unaofuata, tusubiri mambo mazuri zaidi kutoka kwa Molinga," alisema Zahera.

Aliongeza kuwa matokeo ya sare kwake ni mazuri, lakini kikubwa kikosi chake kimepata mazoezi mazuri kuelekea mchezo wao wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zesco FC unaotarajiwa kuchezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Taifa jijini.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, amewapongeza mashabiki na wanachama wa klabu hiyo kwa kufanikisha Tamasha la Siku ya Mwananchi Kanda ya Ziwa.

Msolla alisema kuwa malengo yao yametimia na anaamini mwakani, watakuwa na tamasha bora zaidi huku pia uongozi ukifikiria kupeleka mechi zake za kimataifa katika jiji hilo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002